

# Kuza Imani Yako

Mwongozo kutoka  
Maandiko Matakatifu


RICHARD A. BENNETT amekuwa na huduma ya kufunza Maandiko Matakatifu makanisani, katika mikutano, katika vyuo vya Biblia huko Marekani, Canada, Ulaya na katika bara la Afrika kwa zaidi ya miaka 45. Na kwa muda wa miaka 20, mafunzo yake kutoka Maandiko Matakatifu yamesikika hewani kupitia Trans World Radio na Far East Broadcasting Corporation. Wakitumia mbinu mbali mbali za kueneza injili, Richard pamoja na mkewe Dorothy wamekuwa na hamu kuu ya kuwasaidia watu ili wamjue Yesu Kristo kwa njia bora zaidi.

“Endapo una hamu ya kufaidika kiroho, ni sharti upate chakula chakiroho. Nacho chakula hiki lazima kiwe kitoweo ambacho kinaingiamwilini na hapo ndipo kitakufaidi. Katika kitabu hiki, Dkt Bennett atuonyesha wazi jinsi vile chakula cha kiroho hukuzi imani.”

Dkt Stephen F Olford



ISBN 9966-7074-1-7



9 789966 707413

CROSS CURRENTS INTERNATIONAL MINISTRIES

Bennett

# Kuza Imani Yako

Kudza Imani Yako



Richard  
A. Bennett

CCIM



## ***Maombi:***

Ibaada, Sala au maombi hutoka katika moyo wa yule ambaye ameangaza macho yake na mawazo kwake Bwana wetu aliye hai Yesu Kristo jinsi amefichuliwa kwetu kuitia Maandiko Mataktifu. Na pale tunapoomba kwa njia hii, basi sisi tutajikuta tumenyenyekea mbele yake na kujitoa kwake kabisa ili tumsifu.      –*kurasa 100*

## ***Kushuhudia:***

Kazi ya kueneza injili huendelea pale yule amabye anaafnya kazi hii ye ye mwenyewe amejazwa na Roho Mtakatifu. Na wakati wa kushuhudia kwa njia hii, ye ye kweli huwa ni mfano ulio wa haki kabisa kwamba Kristo yu hai ndani yake.      –*kurasa 130*

## ***Mapambano ya Kiroho:***

Unapoomba kulingana na jinsi vile Maandiko Matakatifu yanatutaka tuombe, basi maombi yako yatakuwa ni maombi ya mapenzi yake Bwana; na fahamu kwamba ni nia yake Mungu uweze kumshinda shetani.      –*kurasa 102*



*Kuza  
Imani  
Yako*

**[www.ccim-media.com](http://www.ccim-media.com)**



*Kuza  
Imani  
Yako*

**Huu ni Mwongozo**  
**wa Maandiko Matakatifu wa kukusaidia kudumisha**  
**na kuimarisha uhusiano wako na Mungu.**

*Richard A. Bennett*

CROSS CURRENTS  
INTERNATIONAL MINISTRIES

*Mkurugenzi*

Trans World Radio - Kenya  
P.O. Box 21514 (00505)  
Nairobi, Kenya  
e-mail: info@twr.co.ke



Kuza Imani Yako ni Tafsiri ya Kitabu *Food For Faith* ambacho kimeandikwa na Richard A. Bennett.

### **Food For Faith – Swahili Version**

Copyright ©1994, 1998, 2009, Cross Currents International Ministries.

Haki zote zimechifadhiwa. Hakuna sehemu ya Kitabu hiki ambayo yakubaliwa kunakiliwa au kuchapishwa kwa njia yoyote, au kuenezwa au kusambazwa pasipo ruhusa kutolewa kkupitia barua kutoka Cross Currents International Ministries.

ISBN: 9966-7074-1-7

Kuras za Maandiko Matakatifu ni kutoka **The Holy Bible In Swahili Union** version ambayo imechapishwa na Bible Society of Kenya, pamoja na Bible Society of Tanzania kama **Maandiko Matakatifu** mwaka wa 1994

Endapo ungependa kupokea msaada zaidi wa Kiroho baada ya Kusoma kitabu hiki, tuandikie Barua.

Anuani yetu ni:  
**Mkurugenzi**  
**Trans World Radio**  
**Sanduku La Posta 21514 code 00505**  
**NAIROBI**  
**Kenya**

*Trans World Radio ni shirika la kutangaza injili kupitia Redio. Endapo ungependa maelezo zaidi kuhusu Trans World Redio, au una hamu ya kupokea ratiba ya vipindi yetu, basi andika barua ukitumia anwani hiyo ya Mkurugenzi wetu hapa Trans World Radio.*

Tuna nakala chache ya kitabu hiki *Kuza Imani Yako*. Unaweza kupokea nakala yako ikiwa utatutumia barua ukitumia anwani hiyo yetu ya Trans World Radio.

Pia endapo ungependa kusoma kitabu cha kwanza cha ndugu Bennett, *Kiu Cha Kumtafuta Mungu*, tumia anwani hiyo hapo juu kutuandikia barua.

Picha kutoka Trans World Radio Africa

Printed in Kenya



## **SHUKRANI**

Katika jina la Bwana yetu Yesu Kristo, kitabu hiki kinachapishwa kama njia moja ya kuwashukuru na kuwapa ahsante wote ambao tumefanya nao, pamoja na mke wangu katika huduma ya kueneza Injili ya Cross Currents International Ministries.

Toleo la Kiingereza la kitabu hiki tayari imepigwa chapa katika lugha kadha kama kazi ya kimishonari ya Cross Currents International Ministries. Kazi zaidi ya kutafisiri kitabu hiki katika lugha mbali mbali na kukichapisha bado yaendelea.



# *Yaliyomo*

<b>Dibaji</b>	11
<b>Utangulizi</b>	13
<b>1. Furaha ya Kila siku</b>	21
<b>2. Kichwa na Moyo</b>	33
<i>Kichwa</i>	36
<i>Moyo</i>	39
<b>3. Kujiandaa na Maombi</b>	49
<i>Piga Magoti</i>	52
<i>Jiweke Wazi Mbele ya Bwana</i>	55
<i>Jinsi Nionav yo Mbinguni</i>	70
<i>Shida Yangu Hapa Duniani</i>	76
<b>4. Wakati wa Kuwa Pamoja na Mungu</b>	87
<i>Kuitikia Kwa Utiiifu</i>	90
<i>Kujitwalia Imani</i>	93
<i>Ukweli wa Sala</i>	98
<i>Silaha ya Neno</i>	100
<b>5. Umuhimu wa Imani</b>	113
<b>6. Wakati wa Kufichua Siri</b>	127
<i>Kujazwa na Hamu Ya Kueneza Injili</i>	132
<b>7. Tunda au Moto</b>	143
<i>Kurasa Nyeupe</i>	147
<i>Miaka ya Hasara</i>	148
<i>Mwanga wa Milele</i>	151
<b>8. Karibu Mezani</b>	155
<b>(Appendices)</b>	176
a. Masomo la Biblia	176
b. Wakati wa Kuwa Pamoja na Mungu	177
c. Mwongozo wa Maombi ya Kila Siku	178





# *Dibaji*

Ni heshima kuu kwangu kupata nafasi hii ya kusema machache kuhusu kitabu hiki cha Dr. Richard Bennett *Kuza Imani Yako*. Kitabu hiki kinafaa sana kikiwa cha kufuata kile cha kwanza, *Kiu Cha Kumtafuta Mungu*. Mwanadamu hawezi kuja kwa Mungu pasipo kupiti imani (*Ebr. 11:6*); na hawezi kumuishia Mungu pasipo kuwa na imani (*Rum. 1:17*). Kwa hivyo basi, ni sharti Roho apate chakula kutoka siku ile na wakati ule wa kupokea wokovu (*Rum. 10:17*) na hata baadaye (*1 Pet. 2:1-3; Ebr. 5:12-14*). Bwana wetu Kristo alitilia mkazo jambo hili aliposema, *mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu* (*Mt. 4:4*). Awali, nabii Yeremia alitilia mkazo wazo hili alipoandika *Maneno yako yalioneekana, nami nikayala; na maneno yako yalikuwa ni furaha kwangu, na shangwe ya moyo wangu; maana nimeitwa kwa jina lako, Ee Bwana, Mungu wa majeshi* (*Yer. 15:16*).

## KUZA IMANI YAKO

Ili kupokea msaada huu Yeremia anataja hapa, chakula cha kiroho lazima kitengenezwe, kitumi we kama chakula na kiingie mwilini na kuwa sehemu yako wewe unayekitumia. Katika kitabu hiki, Dr. Bennett anatuonyesha jinsi haya yote hutokeea. Yeye amefafanua kwa undani kuhusu jambo hili katika sura ya tisa yenye kichwa **Kuwa Pamoja Na Mungu**. Katika siku hizi ambapo watu wanatilia mkazo sana mambo ya utu (humanism), mkristo wa kawaida anajikuta anazoeshwaa kuamini eti anaweza kuishi maisha ambapo hamtegemei Mungu kiroho, na hakuna haja Kristo kuishi ndani yake. Kitabu hiki, *Kuza Imani Yako* ni sawa na ujumbe kutoka juu mbinguni kwetu sisi sote kuhusu haya na mengine mengi ya kukujenga na kukuendeleza kiroho.

Katika siku hizi ambapo watu wanatilia maanani sana tamaduni na mienendo ya ki-utu, enzi hii ambapo wakristo wa kawaida wamefanywa kuwa na mawazo kwamba wanweza wakaishi maisha ya kiKristo pasipo **kumruhusu na kumpa nafasi** Kristo aishi ndani yao jinsi vile imeandikwa katika (*Wagalatia 2:20*), Kitabu hiki kinapowaendea wasomaji.

Dr. Stephen F. Olford

## ***Utangulizi***

**K**uza Imani Yako ni kitabu ambacho kinafuata kile cha kwanza *Kiu Cha Kuntafuta Mungu*. Na hiki ni kitabu ambacho nilikiandika pale mimi na mke wangu Dorothy tulipokuwa tunakaribia mwaka wa 25 tangu tufunge pingu za maisha. Wakati ule, tulikuwa na hamu ya kufa nya jambo ambalo lingekuwa njia yetu sisi kumshukuru kwa ajili ya wema wa ke kwetu tangu tufunge ndoa. Tuliamua kuandika, kuchapisha na kugawa nakala hizi ambazo zilikuwa na maelezo ya n ayohusu Maandiko Matakatifu.

Tulichapisha pale mwanzo nakala 25,000 ya kitabu hiki *Kiu Cha Kuntafuta Mungu*. Baada ya hapo, Mungu akabariki huduma yetu hii ya uch apishaji kwa njia ya ajabu kabisa.

Leo hii, karibu nakala milioni mbili zimechapishwa, na kupewa wasomaji pembe mbali mbali duniani, na katika lugha 50. Wale wanaohitaji kitabu hiki wamezidi kuonge zeka. Lile ambalo limetutia moyo sana ni kupokea habari kuhusu wale

## KUZA IMANI YAKO

ambao wamempokea Kristo baada ya kusoma kitabu hiki.

Baada ya muda, tulikaribia wakati wa kushehere kea mwaka wa 35 tangu tufunge ndoa! Baada ya muda, milango imefunguka kuwezesha kuenezwainjili na kuchapishwa nakala zaidi za kitabu hiki *Kiu Cha Kumtafuta Mungu*. Matokeo ni kwamba tumeona haja ya kuweza kumshukuru Mungu kwa ajili ya wema wake kupitia uchapishaji wa kitabu hiki kipywa, *Kuza Imani Yako*. Ni ombiletu kwamba sawa na jinsi vile Mungu ametumia kitabu cha kwanza *Kiu Cha Kumtafuta Mungu*, yeye atawezekutumia pia kitabu hiki, *Kuza Imani Yako* ili kiwe cha msaada kwa wale ambao wanamjua Kristo katika nchi mbali mbali duniani .

Hata hivyo, *Kuza Imani Yako* si kitabu ambacho kinafuata tu kile chakwanza. Dorothy pamoja nami tunaamini kwamba kitabu hiki kitakuwa cha msaada mkuu kwake yejote yule aliye na imani na hamu ya kuishi maisha ya utukufu na kuwa karibu sana na Mungu. Kitabu hiki kimeandikwa na ombikuu kwamba kila mwenye kukisoma atapata msaada na kutiwa moyo katika maisha yake ya Kikristo.

***Kuza Imani Yako si kitabu cha kusomwa kama kile kingine chochote na kuwekwa kando. Baada ya kusomwa kwa makini, ni jambo bora kiwekwe mahali ambapo kitawezekutukuliwa na kusomwa ili wewe unayesoma ujiendeleze. N pale mwongozo uliomo unapotumiwa maishani, sisi tutajifunza jinsi ya kujiendeleza kwa njia bora zaidi katika juhudzi za kumjua Mungu.***



## *Utangulizi*

Kitabu hiki hakistahili kusomwa bila kutiliwa maanani. Pia kitabu hiki si kitabu cha kusomwa na kuwekwa kando. Baada ya kusomwa, kitabu hiki kinafaa kuwekwa karibu ili kiweze kurudiwa na yale yaliyomo kuzingatiwa katika maisha ya kila siku. Na pale maelezo yaliyomo yanapotumiwa katika maisha ya Mkristo, utajifunza jinsi ya kutembea na Kristo ukiongozwa na Mungu kila siku.

Wengi wetu huona kuwa ni jambo labusara sana wakati fulani kwenda kwa daktari ili atufanyie ukaguzi. Kwa kufanya hivyo, sisi hutumia kiasi fulani chapesa na hata muda wetu. Uchunguzi wa kiafya na matibabu yatakayofuata yote hutegemea ni maswali gani daktari anatuuliza. Sawa na haya, ni jambo labusara pia mkristo kujiuliza maswali fulani kuhusu afya yake ya kiroho. Kile kinachohitajika hapa ni kujibu maswali haya na ukweli. Pia unahitajika kutenga wakati fulani kuwa na Mungu. Baada ya kila kurasa, yako maswali ambayo unastahili kuyajibu. Maswali haya yamechaguliwa yawenjia moja ya kujipima hali yako ya afya kiroho. Baadhi ya maswali haya huenda yakakuletea uchungu. Kumbuka, sawa na wakati ule daktari anakukagua, sehemu ile ya mwili ambayo huwa na uchungu ndio sehemu iliyo na shida. Kwa hivyo, swali lile ambalo litakutia uchungu ndilo swali linalohitaji kushughulikiwa kwa undani sana.

Wakati wa kuandika kitabu hiki, nakumbuka kisa kimoja ambacho niliwhi kusimuliwa na mwenzangu ambaye hivi sasa ni marehemu Daktari J. Edwin Orr. Alisema kwamba kuna siku ambapo mhudumu

## KUZA IMANI YAKO

mmoja mashuhuri alialikwa kuhudhuria mkuutano pamoja naye na viongozi mbali mbali mashuhuri nchini. Kusudi la mkuutano huu lilikuwa ni kuombea taifa. Hata hivyo mhubiri huyu alikataa ombi hilo, akasema hana wakati wa kujiunga na wenzake katika maombi hayo marefu. Hata hivyo, aliongeza katika kumaliza barua yake kwamba ana ujumbe maalum kuhusu maombi ambayo angependa aje awape washiriki wa mkuutano huu katika siku za baadaye. Yeye aliyokuwa anasema ni kwamba hata hawa wahudumu wa kueneza injili walihitaji maombi sawa na taifa lao. Naelewa vyema jinsi vile lililo jambo rahisi kuhubiri na kuandika kuhusu maombi kuliko kushiriki katika maombi yenye. Kwa hivyo, wakati huu wa kuandika kitabu hiki, naandika sio kama yule mtaalam; wala ni kama mmoja aliye na njaa ya maombi ambaye anawaandikia wale walio na njaa wenzake na kuwaeleza jinsi ya kupata mkate wa siku.

Mke wangu Dorothy amekuwa wa msaada kwangu wakati wa kuandika kitabu hiki. Isitoshe, yeye amenitia moyo na kunihimiza kuweza kutenga wakati fulani ili niwe peke yangu na Mungu. Nakumbuka vyema kabisa jinsi vile niliwahi kusoma katika baadhi ya maandishi ya C.T. Studd kuhusu maombi, na hasa kuhusu ombi fulani ambalo nilikuwa nalo kabla sijakutana na mwenzangu huyu katika ndoa, Dorothy. Ombi lenyewe ni hili: "Mungu, kama umenitengea mke, na awe kama chuma iliyoshika moto mpaka kuwa nyekundu ili pale ninapojikuta sina nguvu, anaweza kutumia moto huo kunielekeza mbele." Ni baraka kuu kwangu kwamba



## *Utangulizi*

niweze kupata mke kama huyu. Bwana asifiwe!

Sasa ni karibu miaka 50 tangu baba wangu katika imani Dr. Stephen Olford aniongoze kumpokea Kristo kuwa mwokozi wa maisha yangu. Ninashukuru sana kwamba wakati huo, Stephen pia alinionyesha umuhimu wa kutenga muda fulani kwa ajili ya kusoma Maandiko Matakatifu na kuomba.

Idadi kubwa ya mawazo ambayo yako katika kitabu hiki yanatoka katika yale nimeyaona na kuwaza kuhusu Maandiko Matakatifu. Mengi pia yanetoka kati-ka mafunzo kuhusu Maandiko Matakatifu kutoka kwa wahudumu wa Bwana amba Mungu ametuwezesha tukutane na kushiriki pamoja nao katika hudu-ma ya bwana. Na ingawa wahudumu wa Mungu hawa ni wengi mno, na siwezi kuwataja moja kwa moja kwa ajili ya kukosa nafasi katika kitabu hiki kidogo, nawashukuru wote na kusema “Bwana Asifiwe!”

Na sasa tunapochapisha kitabu hiki, *Kuza Imani Yako*, nachukua nafasi hii kutilia mkazo yale mtume Paulo alimweleza Timotheo *kwamba: mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine* (2 Tim. 2:2).

Ingawa kitabu hiki kiliandikwa ili kiwasaidie wakristo waweze kufurahia ushirika wao na Mwokozi wetu Yesu Kristo, sina shaka huenda kukawa na mtu fulani ambaye anasoma kitabu hiki huku hajaweza kupokea utamu ule unao-tokana na kujua kwamba amepokea msamaha wa dhambi, na kuwa na uhaki-ka kwamba ana uzima wa milele. Kama



## KUZA IMANI YAKO

wewe ni mmoja wa wale walio katika kikundi kama hiki, nakusihi hebu soma yale yaliyo katika Yohana Mtakatifu:

*“Lakini hizi zimeandikwa ili mpate kuamini ya kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu; na kwa kuamini mwe na uzima kwa jina lake” (Yn. 20:31).*

— R.A.B.



*Kuza  
Imani  
Yako*



*Mausia yako ni matamu sana kwangu, kupita asali  
kinywani mwangu. (Zab. 119:103). Ndiyo maana  
nimeyapenda maagizo yako, kuliko dhahabu, naam,  
dhahabu iliyo safi. (Zab. 119:127)*

# *Furaha ya Kila Siku*

Juzi, mama mmoja wa kupendeza na pia mkristo alijitokeza na ombi hili: "Tafadhali niweke katika maombi yako ili niweze kuwa na uhusiano wa karibu sana na Mungu." Kwa kweli uhusiano kati ya wanadamu huwa ni wa viwango mbali mbali. Sawa na uhusiano huu kati ya wanadamu; uhusiano wetu na Mwokozi Yesu Kristo huwa ni wa viwango vinavyotofautiana kabisa kati ya wanadamu.

Na hata katika uhusiano kati ya wanadamu, hali ile ya kuelewa na hunawiri tu pale kuna masikilizano na ushirikiano; na hata kuwa na mambo fulani ambayo yanawashirikisha pamoja wale ambao wanaelewana. Uelewano hutokana na watu kuzungumza pamoja bila kuwa na siri kati yao. Uelewano pia hutokana na watu kuwa na mawazo yaliyo sawa.

Kwa mfano, mimi na mke wangu Dorothy juzi tulipokea barua ambayo ilitujaza furaha kubwa. Barua hii ilitoka katika bara la Afrika. Nayo ikasema: "Jana tulimleta nyumbani mtoto Dorothy kutoka hospitalini. Na sawa na yule ambaye ana jina kama lake, mtoto Dorothy alifika wakati tuliomtarajia.

## KUZA IMANI YAKO

Mtoto Dorothy aliwasili salama akiwa na uzito wa kilo tatu.

Lilikuwa ni tukio la kufurahisha sana kwa wale wazazi wa mtoto huyu pamoja na familia yao yote. Ni jambo lililo rahisi sana kuelewa furaha ya wazazi pale wanapomchukua mtoto mchanga na kumleta nyumbani baada ya mama kujifungua. Na furaha hii huendelea hata pale mtoto anapozidi kukuwa. Furaha hutuzidi pale mtoto anapoanza kunyoosha viungo vyake na hata kucheka. Vidole vidogo miguuni, magoti ya kitoto yaliyojikunja, hatua ya kwanza ya kutembea; na wakati ule wa kwanza mtoto anapotamka “Mama” au “baba.”

Haya yote hutusimua. Kwa kweli mtoto ambaye amezaliwa, akiwa na uwe zo wake wa kukuwa ni mwujiza ambao hata mwanadamu hawesi kuelewa. Sawa na kuzaliwa mtoto mchanga, pale mtu mzima anapozaliwa mara ya pili hili nalo pia ni tukio kuu. Pale mtu anapopiga hatua ya kwanza kutoka wakati wa kuzaliwa kiroho na kufikia kiwango cha kuwa kama mtu mzima kiroho: haya yote ni matukio ambayo ni kama mwujiza.

La kusikitisha ni kwamba maisha hayafuati mwendo wa furaha kutoka kuzaliwa mpaka kuwa mtu mzima. La kusikitisha zaidi ni kwamba pale tulipokuwa tunafurahia kuzaliwa kwa mtoto Dorothy, tulipokea habari kwamba mtoto wa rafiki yetu kule mji wa Cincinnati, jimbo la Ohio Marekani wa umri wa miaka 21 alikuwa ameaga dunia. Katika miaka hiyo 21, mtoto huyu alikuwa hajawahi kutoka katika hali ile ya utoto kimawazo, kimwili na hata kijamii.

## *Furaha ya Kila siku*

Hata ingawa wazazi wake walikuwa wamembatiza jina la kupendeza Carol Joy (maana yake jina hili katika lugha ya kiingereza ni: wimbo wa furaha) alipoaga dunia, Carol alikuwa bado ni mtoto. Uwezo wake wa kuzungumza ulikuwa ni ule wa mtoto mchanga. Sababu iliyoleta hali hii ni kwamba alikuwa anaugua. Uwezo wake wa kukua ulikuwa umedhuri wa na maradhi hayo.

Sawa na jinsi vile Carol alikuwa hawezi kutoka utotoni, ndivyo walivyo wengi kanisani hata leo. Hawawezi kutoka katika utoto wa kiroho. Ingawa wamekuwa wakristo kwa muda mrefu, bado hawajaweza kukua kiroho. Ingawa Mungu ametupatia chakula cha kiroho ambacho ikiwa kitatumiwa vyema chawenza kumkuza kila mtoto wa Mungu ambaye ni mtu aliye zaliwa mara ya pili ni sharti akue kiroho. Wako kati yetu ambao hata baada ya miaka kupita, wao bado hawajakua kiroho.

Biblia ni chakula kutoka kwa Mungu ambacho kazi yake ni kuhakikisha kwamba unakuwa vyema kiroho. Ikiwa unataka kukuwa kutoka hali ile ya kutaka tu kuchunguza mambo ya kiroho kama mtoto, hadi kiwango kile cha kutulia katika ujana na mwishowe kiwango cha kukomaa kama mtu mzima; ni sharti upate chakula cha kiroho ambacho kimetoka kwa Mungu. Chakula hiki kinapatikana katika Maandiko Matakatifu ambayo ni Biblia. Kusoma Biblia ni jambo ambalo Mungu amelitenga lisiwe tu kama kazi ya kila siku. Kusoma Biblia ni kazi ambayo inafaa iwe ni ya kufurahisha kila mkristo aliye na kiu na njaa, na anahitaji chakula hiki ambacho

## KUZA IMANI YAKO

aliyekiandaa ni Mungu. Ni kweli kabisa neno la Mungu litakuwa chanzo cha furaha kuu inayoendelea kukuwa pale unapojifunza jinsi ya kutumia chakula hiki, ili kikujenge na kuwa sehemu ya mwili wako.

Kupitia nabii Isaya, Mungu anawaalika wote walio na njaa na kiu cha Neno la Bwana wakaribie mezani ili wakashiriki pamoja katika meza ya Bwana.

*Haya kila aonaye kiu njooni majini, naye asiyeha na fedha, njooni nu nueni mle; Naam njooni nu nueni divai na maziwa, Bila fedha na bila thamani. Kwani kutoa fedha kwa ajili ya kitu ambacho si chakula? Na mapato yenu kwa kitu kisichoshibisha? Nisikilezeni kwa bidii, mle kilicho chema, na kujifurahisha nafsi zenu kwa unono. Tegeni masikio yenu, na kunijia; Sikieni, na nafsi zenu zitaishi; nami nitafa nya nanyi agano la milele, Naam rehema za Daudi zilizo imara (Isa. 55:1-3).*

Kwa vile watu wengi hawajui jinsi ya kupata chakula cha kiroho pale wanaposoma Biblia, wao huona kwamba ni kazi rahisi kusoma vitabu vinavyohusu Biblia kuliko kusoma Biblia ye nyewe. Kitabu hiki ulichonacho mkononi hakina maelezo kuhusu Biblia, ila ni kitabu ambacho lengo lake ni kukutia moyo usome Biblia kwa njia ile ambayo Biblia yenyeche itajifi chua na kujifafanua kwako. Matokeo ni kwamba utaweza kufurahia maisha ya kari bu na bila chochote cha kumfi cha baba yako aliye juu mbinguni.

## *Furaha ya Kila siku*

Kwa mara nyingi, nimewaambia wengi ambaao wameanza kusoma Biblia kama chakula cha kiroho hivi:

**Soma kile ambacho unakielewa, na baadaye utakutana na kile ambacho huelewi. Endelea kusoma. Baadaye utakutana na kile ambacho unaelewa. Na baadaye, kile ambacho unaelewa kitakusaidia kuelewa kile ambacho huelewi!**

Je, unaelewa haya ninayosema? Kwa kifupi tu, nasema, usikubali kushindwa!

Kote duniani, katika madarasa, na kumbi za masomo; na hata katika maktaba, watu wanapata masomo ambayo ni kama “chakula cha mawazo.” Sawa na hawa, sisi pia tukichukua maandiko matakatifu kuwa kitabu chenye maelezo ya kidini tu, basi tutapata “**chakula cha mawazo.**” Biblia inatuonya *Na kwa habari ya vitu viliviyotolewa sadaka kwa sanam u; Twajua ya majivuno, bali upendo hujenga (1 Kor. 8:1).*

Ni kweli kabisa tusipojua jinsi ya kusoma na kuelewa neno la Bwana, ujuzi wetu unaotokana na kujua neno hili waweza ukatufanya tuwe na ujeuri na hata maringo. Badala ya kupokea elimu na hekima kupitia kusoma Neno la Mungu, inafaa tuweze kupata chakula ambacho kitatujenga kiroho kutoka meza ya Bwana, ‘**nacho hiki ni chakula cha kiroho’.**

Kando na wasomaji wa kawaida ambaao husoma Maandiko Matakatifu kama kitabu cha busara tu,

wako wale ambaao wanatosha Biblia na kuchukua yaliyomo kuwa kama chakula cha kiroho, na wao

## KUZA IMANI YAKO

hutilia maanani yaleyaliiyomo na kuishi jinsi vile maandiko yanawaagiza walio na imani kuishi. Wakristo kama hawa wanaona ukweli wa kuishi maisha kwa kushiriki pamoja na Mungu, na kwa kupitia njia hii, wao wanagundua jinsi vile kuomba na kumhudumia Mungu. Kumkaribia Mungu na haki kila asubuhi na Biblia mkononi, na moyo ulio tayari kupokea ujumbe wake ni haki kuu ya kila mtu ambaye amezaliwa mara ya pili.

Swali ambalo labda unajiliza ni hili: Ni njia gani iliyo bora ya kusoma Biblia ili maandiko haya yaweze kuwa kama chakula cha kiroho cha kunisaidia kukuwa na upendo na hekima inayoelekezwa kwa Mwokozi wetu Yesu Kristo? Jibu la swali hili lapatikana katika kile ambacho tunakiita Wakati Wa *Kuwa Pamoja na Mungu*.

Kwa kweli Wakati *Wa Kuwa Pamoja Na Mungu* ni muda tunaoutenga ili tukaweze kuzungumza naye Mungu wetu aliye hai. Kupitia neno lake katika Biblia, Mungu huzungumza na watoto wake. Tunapoitikia yale anayosema nasi moja kwa moja kwa njia iliyo sawa, tunajifunza jinsi ya kuomba kiBiblia tukiwa na imani ilio na matarijio.

Ninaposema, ‘kuomba KiBiblia’, lile ninalo maanisha ni kwamba tunapoomba, tunafanya hivyo tukitumia lugha na maneno yaliyo sawa na yale Mungu mwenyewe ametumia ambayo yanayopatikana katika Maandiko Matakatifu. Kuomba kiBiblia hufu rahisha kwa vile huwa ishara ya wazi kwamba tunaomba kulingana na mapenzi yake Mungu.

## *Furaha ya Kila siku*

Na pale Roho Mtakatifu anapofanya Neno lake Mungu kuwa hai katika maisha yetu, sisi tunatumia matamshi ambayo ni maneno yanayopatikana katika Maandiko Matakatifu kueleza yale yaliyo katika roho zetu. Tukiomba kwa njia hii, basi tutaweza kuepuka mtego ule wa kuomba maombi ya kila siku yasiyo na tofauti siku baada ya siku. Badala ya hayo, tutakuwa na ushirika wa karibu sana na Mungu wetu pale tunapoingia katika hali ile ya kuelewa yale yanayomhusu na kusudi lake katika maisha yetu.

Maombi ya kweli siyo maombi ambayo kusudi lake ni kubadili nia au mipango ya Mungu. Maombi ya kweli ni maombi ambayo kusudi lake ni kubadili nia yetu sisi wanadamuiwe sawa na nia ya Mungu. Baada ya Yoshua kuwaongoza wana wa Israeli kupita katika mto Yorodani wakati wa mafuriko ya majira ya kati, yeye alikutana na mtu “asiyemfahamu.” Yoshua kutoka Kanaani kwamba agizo la Mungu kwake lilikuwa kupiga vita nchini na kuondolea mbali uovu wa dini zisizo za ukweli. Kwa hivyo, Yoshua alimwuliza huyu aliyekutana naye swalii moja tu, “Wewe uko upande wetu au upande wa maadui wetu?” Jibu ambalo Yoshua alipewa lilimstaajabisha. Yule mtu alisema: “Mimi siko upande wowote.” Na hapa Yoshua akachukulia jibu hili kuwa la maana kwamba mtu huyo hatakuwa katika upande wowote. Na hapo huyo mtu akaendelea kusema yale ambayo yalifafanua zaidi jibu hilo lake. Alisema: “*Kama kamanda wa jeshi la Mungu, sasa nimewasili.*”

Hapa Yoshua akajua kwamba badala ya kuwa mtu aliye katika upande wowote, yeye alikuwa amekuja

## KUZA IMANI YAKO

kuchukua mamlaka yote hapa. Yoshua aliinama, hii ikiwa ishara ya heshima ya kuonyesha utiifu kwa vile sasa alikuwa yuko mbele ya mkuu wa jeshi la Mungu.

Ikawa hapo Yoshua alipokuwa karibu na mji wa Yeriko, akavua macho yake na kuangalia na tazama mtu mume kasimama kumkabili mbele yake, naye alikuwa n aupanga wazi mkononi mwake; Yoshua akamwendea, na kumuambia Je! Wewe U upande wetu, au upande wa adui zetu? Akasema la, lakini nimekuja sasa nili amiri jeshi la BWANA. Yoshua akapomoka kiusouso hata nchi, naye akasujudu, akamwuliza, Bwana Bwana wangu aniambia nini mimi mtumishi wake? Huyo amiri wa jeshi la Bwana akamwambia Yoshua, vua viatu vyako miguuni mwako; *kwa kuwa mahali hapo usimamapo ni patakatifu. Yoshua akafanya vivyo* (*Yos. 5:13-15*).

Sawa na haya, katika maombi yetu, ni sharti tусиya chukue yale ambayo tunayaona kuwa ya muhimu na kuyapeleka mbele ya Mungu na kumtaka atutimizie haja zetu. Badala ya kufanya hivyo, tunastahili kuinama mbele ya utukufu wake, na kuelewa mipango, tumaini na nguvu zake katika maisha yetu lengo lake katika maisha yetu.

Kwa hivyo kuomba kiBiblia ni kuomba kwa njia ambayo inakubaliana na mipangoya Mungu katika maisha yetu. Kuelewa haya yote ni jambo ambalo laweza kuchukua muda kwani ni sehemu ya kukuwa kiroho kwa kila mtu pale anapozidi kujitahidi kuomba kulingana na jinsi vile Maandiko Matakatifu yanavyotutaka tuombe.



## *Furaha ya Kila siku*

Unaposoma Maandiko Matakatifu na moyo wa maombi, ukiwa na hamu ya kusikia sauti ya Bwana, wewe utapokea busara na hekima. Maandiko Matakatifu yanasema hivi: *Lakini, kueni katika neema, na katika kumjua Bwana wetu mwokozi Yesu Kristo. Utukufu una yeye sasa na hata milele* (2 Pet. 3:18).

**Jinsi vile tayari tumegusia hapo juu, nabii Isaya alisema tunapoyaweka masikio yetu tayari na kusudi la kusikiliza sauti ya Mungu, kwa kweli tutafurahi sana pale tutakaposikia yale atakayoyasema.**



## **Ichunguze Roho Yako**

1. Ni muda gani umepita tangu nilipompokea Kristo kama Mwokozi wa maisha yangu?
2. Niliwahi kufurahia ushirika wangu na Mungu zaidi wakati ule kuliko wakati huu?
3. Nikilinganisha maisha yangu ya leo na yale ya hapo miaka mitano iliyopita:

Je, n atumia kiasi gani cha muda wangu kumkaribia Mungu?

Je, n aweza kutosautisha kati yale Mungu anataka nifa nye na yale mimi mwenyewe binafsi nataka kufanya?





*Nifunze kusikiliza Mungu. Siku  
hizi ni siku za kelele, na masikio  
yangu yamechoshwa na maelfu  
ya sauti mbali mbali kubwa  
zinazonishambulia. Ni pe roho kama  
yule wa kijana Samweli ambaye  
alisema: zungumza, mtumishi wako  
anakusikiliza. Hebu nikusikilize  
ukizumgumza nami katika roho  
yangu. Hebu niwe zeshe kuzoea sauti  
yako, ili niweze kuizoea, na pale  
sauti za dunia zitakapokoma, niweze  
kuendelea kuisikia sauti yako. Amin.*

— A. W. Tozer



## *Kichwa na Moyo*

**K**atika miaka ya hapo nyuma, mimi na mke wangu Dorothy tulipata fursa ya kuwafunza makasisi na wake zao kaskazini nchini Kenya Neno la Bwana. Ili waweze kufika mkutanoni saa moja jioni, iliwabidii baadhi yao waamke na kufunga safari saa kumi asubuhi. Hamu ya kujifunza Neno la Bwana ilikuwa imewafanya waamke mapema hivyo na kutembea na miguu katika eneo hili la ukame, njaa na joto kali.

Tulishtuka kugundua kwamba kati ya asilimia 60 na 70 ya washiriki katika mkutano huu hawakuwa na nakala ya Biblia. Na ingawa wako wale ambao walikuwa wameamua kumfuata kristo yaapata miaka 2-3 iliopita, ushuhuda wao ulikuwa umesaidia katika ujenzi wa makanisa madogo madogo sehemu mbali mbali katika misitu ya bara la Afrika hapa nchini.

Pale mwanzo wa mkutano huu, tuliweza kumpa kila mshiriki Biblia mpya. Na baada ya hapo nikaendelea na siku kadhaa za mafunzo. Kichwa cha mafunzo yangu kilikuwa hiki: Kwa vile sasa una Biblia, haitaku waya faida kwako mpaka pale itakapotoka mkononi na kuwa katika kichwa **chako!**

## KUZA IMANI YAKO

Na hata hii haitakuletea baraka ambazo Mungu amekusudia kwamba ziwe zako siku hizi. Ni pale neno la Mungu litakapoanza kuishi katika moyo wako ndipo mkutano huu utakuwa we nye baraka kwako. Ni jambo la muhimu kabisa kwamba ujifunze jinsi ya kuondoa Biblia **mkononi** na badala yake iwe katika kichwa chako, na baadaye kutoka kichwani hadi katika **moyo** wako.

Juzi niliona nyumba kule Uingereza ambayo ilikuwa ni makao yangu pale nilipokuja kumjua Kristo mwisho wa ujana wangu. Karibu na nyumba hii kuna chuma ya kushika taa ya barabarani ambapo chini ya ke kijana wa miaka 14 Bob Flint alimpokea Kristo. Tukio hili lilimbadili Flint mara moja. Yeye hakuwa msomi: aliacha shule na wakati ule, alikuwa anafanya kazi ya ujenzi.

Hata ingawa alikuwa hana elimu ya kutosha, niliweza kumshawishi Bob awe akisoma Biblia yake kila siku kabla ya kwenda kazini. Na ingawa pia hakuwa akienda kanisani, Bob alijifunza jinsi ya kujilisha kiroho kupitia kushiriki na Mungu wakati ule wa *Kuwa pamoja na Mungu*.

Si ajabu kwamba akiwa na umri wa miaka 17, Bob aliweza kuijandikisha katika chuo cha Biblia kupitia njia ya posta na kupata alama za juu sana katika somo lililohusu Daniel! Lilikuwa jambo la kunifurahisha sana kusikia kwamba hata akiwa na umri wa miaka kumi na nane alipojiunga na jeshi wakati huo, yeye alikuwa na hamu ya kujua mengi kuhusu Mungu. Na hata akiwa mwanajeshi, katika wiki nane za kwanza aliweza kuwaongoza wenzake 17 kumjua Kristo. Na

## *Kichwa Na Moyo*

baada ya kumaliza muda wake wa kuhudumu jeshini, Bob alipokea wito wa kuanzisha huduma ya mafunzo ya kimishonari. Alipokuwa katika safari yake ya mwisho Ujerumanî, ndege yake ya kijeshi ilianguka, na Bob akaaga dunia.

Karibu na mahali pale alipoaga dunia, vijikaratasi vya kueneza injili vilitoka kwenye kapu lake dogo la mgongoni na kutawanyika ovyo ovyo mahali hapo. Kwa kweli neno la Mungu lilikuwa limetoka mkononi mwake Bob, na kuingia kichwani. Na kutoka kichwani, likafika katika roho yake, na hatimaye likawafikia wale walioku wa karibu naye. Pale alipoaga dunia, ye ye aliwa ameitwa kutoka maisha haya ya uhusiano wa karibu na Mungu wake, na sisi ye ye aliwa ameenda kuwa katika ushirika wa moja kwa moja mbele ya Mungu.

Wengi kama Bob wana nafasi ya kupata vitabu vya mafunzo ya Biblia ambavyo vyawenza kuwajenga na **kuwaendeleza**. Makasisi barani Afrika ambao walikuwa hawana cha kuwasaidia hadi kuwabidi watembee zaidi ya masaa 15 kwenye joto kuu la Equator kupokea mafunzo ya Biblia. Ingawa mafunzo haya *Kuza Imani Yako* ni ya muhimu, tunastahili kujua jinsi ya kubadili masomo ya Biblia ambayo tunapokea kuwa kitu ambacho tumekiona na kusikia na kinapatikana katika roho zetu.

Mimi mwenyewe namshukuru Mungu sana kwa ajili ya kunionyesha mapema tofauti ilioko kati ya kusoma Biblia, na kuwa na wakati fulani pamoja na Mungu. Ingawa yale tunasoma yako kichwani, na kwamba lazima tutumie kichwa na

## KUZA IMANI YAKO

moyo kuelewa mambo ya Mungu, ni wazi kwamba ukijua mengi kichwani, na ukose kuyaweka moyoni, yote hayatakuwezesha kukua kiroho.

### KICHWA

#### *Somo La Biblia: Lengo na Shida Zake*

*Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiyе na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli (2 Tim. 2:15).* Kujifunza Biblia, na hapo kujua yale yaliyomo ni jambo la kufurahisha na hata kusisimua. Pia hili ni jambo ambalo kila Mkristo anastahili kulitimiza. Ikiwezekana, tumia wakati wako kupokea mafunzo ya Biblia kutoka kwa mwalimu au kasisi mwenye ujuzi unaofaa na unaostahili. Tumia vitabu pia kuendeleza ujuzi wako wa yale yaliyo katika Maandiko Matakatifu. Haya yote yatakusaidia sana pale unapojitenga na kuijeweka kando ili uwe pamoja na Mungu.

Isitoshe, wachungaji ambao ni wa alimu wa injili wote ni baraka kutoka kwa Mungu kwa kanisa. Kazi kuu ya kasisi ni kuwafunza wafuasi wake yale yaliyoko

kwenye Maandiko Matakatifu, wakati haya yalipoandikwa na hali ya mambo katika mazingira wakati wa matukio hayo kutokea. Mafunzo haya yanahu kila kitabu cha Biblia, kila sura na kurasa katika Maandiko haya Matakatifu. Na kutoka hapa, Kasisi ana wajibu kuwatia wafuasi hamu ya kuishi maisha yanayo mfurahisha Mungu, hali ya kutosheka, na moyo wa kuwajali sana wale wanaoangamia.

## *Kichwa Na Moyo*

Mimi hivi leo nina nakala ya mafunzo tano ambayo yalitoka kwake mwalimu mmoja wa aina hii. Hapo nyuma Mchungaji William Still alikuwa bado anatoa mafundisho haya pale Inter-varsity Theological Student's Conference. Baada ya miaka 45 ya kuhudumu katika kanisa moja kule Aberdeen, Scotland ye ye bado alikuwa na hamu ya kueneza injili sawa na jinsi vile aliviyokuwa pale mwanzo. Huduma yake ilienea mbali kutoka hapo kanisani. Hata leo, kuna jeshi dogo la wale waliokuwa wanafunzi wake ambao bado wanendeleza kazi aliyoanzisha. Katika baadhi ya mafunzo yake, Mchungaji Still aliwahi kusema hivi:

Mchungaji ameitwa kulisha kondoo wake hata pale kondoo hawana hamu na chakula. Ni sharti asiwe mtu wa kuwfurahisha mbuzi wake. Acha mbuzi wawafurahishe mbuzi wenzao katika shamba la mbuzi. Huwezi kuwabadili mbuzi wakawa kama kondoo tu pale unapowafanya hivyo. Kazi kuu ya uchungaji ni kuwasaidia kondoo wa kila aina waweze kuishi pamoja, na kuwaonyesha jinsi vile wanavyostahili kuishi pamoja na kondoo bila kujaribu kujibadili kuwa kondoo.

Pale unapozaliwa mara ya pili, ni sharti ujiunge na kanisa ambapo utaweza kupokea baraka kutoka kwa wachungaji kama hawa.

## KUZA IMANI YAKO

La kusikitisha ni kwamba baadhi ya wale ambao wanasona kitabu hiki hawana uwezo wala nafasi ya kuwafikia waalimu kama hawa. Hata hivyo, ikiwa umebarikiwa kuwa na wachungaji wazuri, na hata kuwa na vitabu ambavyo ni vya kukusaidia kusoma neno la Bwana, ni sharti ujihadhari masomo na mafunzo haya yasije yakawa ni kikwazo hivi kwamba huna wakati wa *kuwa pamoja na Mungu*.

Ni sharti tujue mafunzo tunayoyapokea, na hata busara tuliyonayo kuhusu Maandiko Matakatifu haiwezi kulinganishwa na chakula cha kiroho ambacho tunapatawakati wa *kuwa pamoja na Mungu*.

Sawa na jinsi vile mafunzo hayawezi kuchukua nafasi ya chakula cha kiroho, lazima tujue kwamba chakula cha kiroho, pamoja na *kuwa pamojana Mungu*, haya yote yafaa yasikufanye uachilie mbali mafunzo ya Biblia.

Zifuatazo ni njia ambazo zaweza kukusaidia ili masomo ya Biblia yako yawe ya msaada kwako. Zamani hapo mbeleni, Myles Coverdale alishauri kwamba maswali haya yatumiwe katika mafunzo ya Biblia.

Maswali yenye ni:

- i. **Ukurasa huu** unazungumza juu ya nani?
- ii. **Ni nani aliyeandikiwa** hayo unayoyasoma?  
ni maneno gani ya muhimu ambayo  
yanatumiwa na mwandishi?
- iii. **Ukurasa huu** uliadikwa wakati gani?



## *Kichwa Na Moyo*

- iv. **Ukurasa huu** uliandikiwa wapi?
- v. **Ni nini** lilikuwa kusudi la mwandishi huyu?
- vi. **Ukurasa huu** uliandikwa katika mazingira gani?
- vii. **Yale yaliyo katika** ukurasa huu yanahusiana kwa njia gani na yale yanayotangulia, na yale yanayofuata?

Je, maswali haya hapa juu yanhausiana kwa njia gani na haya ambayo yanafuata?

Pale unapojizoesha kujibu maswali kama haya, wakati wa kusoma Biblia, utafurahishwa sana na ukweli ulio katika Biblia. Na baadaye utafurahishwa zaidi. na unabii ambao uko katika Maandiko Matakatifu. Na hata utagundua kuna sehemu za unabii ambazo tayari zimetimia; na sehemu fulani zangoja kutimia.

Ukifuata mwongozo huu, utabarikiwa sana kwa vile utaweza kuona; kusudi lake Mungu katika kutuumba sisi wanadamu. Macho yako yatafunguka zaidi ili uweze kuona kusudi lake hili; Sehemu na wajibu wake katika historia ya dunia; Mafunzo yake kuhusu wokovu; Kuja kwake Mungu akiwa Kristo; Na pia maelezo yake kwetu wanadamu wakati huu.

### **MOYO**

*Wakati wa Kuwa Pamoja na Mungu: Jinsi hali  
hii husaidia katika kusahihisha makosa yetu na  
kutupatia mawaidha.*

## KUZA IMANI YAKO

Kile Mungu anahitaji kutoka kwa kila amwaminiye ni kwamba amwabudu kwa *roho na kweli*. (*Yn. 4:24*), Kumuabudu na **moyo** na katika **akili** yetu kwenye ubongo wetu. Moyo na akili vikiwa vitu vilivyo kama kitu kimoja.

Kama somo lako la kibinafsi la Maandiko Matakatifu hukuacha tu ukiwa na ujuzi wa kawaida wa maandiko matakatifu, ujuzi kama huu utakuwa wa msaada mdogo sana kwako. Kwa kweli ujuzi ambao ni utaalamu wa kimafunzo tuu pasipo kuyaweka yale ambayo umesoma maanani na kuyatimiza jinsi vile Maandiko Matakatifu yanavyohitaji ni jambo ambalo ni shida kuu kwao wakriso wengi siku hizi.

La kusikitisha ni kwamba wako wengi sana ambao wamesoma na kuelewa Maandiko Matakatifu lakini hawashirikishi mafunzo yake katika maisha yao. Wao wanafungia ujuzi mkuu waliyo nao kuhusu Maandiko Matakatifu katika sehemuza nyuma kabisa katika mawazo yao, na badala yake kufuata njia za kidunia. Huu ni mkasa mkubwa, kwa sababu mafunzo ya Maandiko Matakatifu hayawezi kulingana na mawazo na mienendo maishani ya siku hizi.

Kuyachukua Maandiko Matakatifu na akili za kibinadamu na baadaye kuchukua Maandiko haya na kuyafanya yaende sambamba na yale ya ulimwengu huu wa sasa, na tamaduni zetu siku hizi ni kwenda kinyume na ukweli wa mambo, kujiondolea heshima na hata kujidanganya. Mwokozi wetu alilipa gharama kubwa sana kutuokoa kutoka dunia hii yenye dhambi nyingi. Ni wazi mawazo ya kibinadamu hapa duniani

## *Kichwa Na Moyo*

ambapo mwanadamu anap uuza yale kutoka kwa Mungu lazima yawe kinyume cha yale ya Mungu.

Na kwa vile Neno la Mungu kamwe halikubaliani na tamaduni za kibinadamu, pale tunaposoma na kujifunza kutoka Maandiko Matakatifu tukiwana hamu ya kufanya yale Maandiko haya yanatuhitaji tufanye, basi kunakuwa na mageuzi makubwa sana katika maisha yetu. Mungu anataka kuona mabadiliko haya katika roho, sio tu katika mawazo ya watoto wake.

Mwandishi wa Zaburi hakusema tu **kichwani** mwangu nimeliweka neno lako, *Nisije nikakutenda dhambi, bali alisema Neno lako nimeliischa katika moyo wangu ili nisije nikatenda uovu* (Zab. 119:11). Hata yule mtawala wa ki-imla Ujerumanii Adolf Hitler alinukulu vifungu fulani kutoka Maandiko Matakatifu wakati wa kutoa hotuba hadharani. Hata hivyo ujuzi wake kuhusu Maandiko Matakatifu haukuwa wa msaada akiwa mwanadamu. Yeye hakuamini yale aliyokuwa akiyanukulu. Ni wazi kwamba yale aliyokuwa akinukulu hayakuwa yamemwingia katika roho.

Labda huenda ukajjiliza, Mfalme Daudi alikuwa na maana gani pale aliposema hivi: *Moyoni mwangu nimeliweka neno lako*. Ni wazi wakati wa kusema haya, Mfalme Daudi hakumaanisha sehemu ile ya mishipa ya miili yetu ambayo ni chombo cha kusukuma damu. Kwa kweli hakuna anayeweza kuficha neno la Bwana katika kiungo hiki! Pale Daudi alipotaja **roho** yake, yeye alimaanisha sehemu ile ya ndani ambayo humuelekeza kutenda mambo fulani ambayo hakustahili kuyatenda. Pale tunaposoma na

## KUZA IMANI YAKO

kuficha Neno la Bwana katika sehemu hii ya ndani ya utu wetu, kupitia nguvu za Roho Mtakatifu, na Kristo kuwa ndani yetu, tunazidi kufurahia utukufu unaosafisha, na unapatikana katika Neno la Bwana.

Nilipowezeshwa kupokea mafunzo ya Biblia nikiwa mwanafunzi kamili katika chuo, nilijifunza jambo moja kwamba kupitia kujua mengi yanayohusu Maandiko Matakatifu: ujuzi huu hauwezi kuwa kitu ambacho chafaa badala ya wakati ule maalum wa *kuwa pamoja na Mungu*, na kusikiliza kwa makini yale ambayo anasema kupitia Neno lake. Nilijifunza pia kwamba ni rahisi siwezi kujaribu kutoa uamuzi fulani kuhusu Maandiko Matakatifu, kuliko kuacha neno la Mungu litoe uamuzi kuhusu maisha yangu.

Wakati wetu huo wa kuwa katika chuo, tulipendelea kucheka na kusema wakati wa masomo darasani ulikuwa ni wakati wa mwalimu kutoa mawazo kutoka kitabu chake na kuyaweka katika kitabu cha mwanafunzi pasipo hata kupitia katika kichwa chake.

Ni mkasa usio na kifani pale mafunzo kutoka Maandiko Matakatifu yanapotoka kwa mchungaji na kuwafikia waumini bila hata kuguza roho zao. Itakumbukwa Mungu anasema wazi hivi:

*Neno lile walilolisikia halikuwa ni la faida kwao;  
na hata kuchanganyika na imani ya wale amba  
walilisikia (Ebr. 4:2).*

Ni pale tu tunapoijihusisha na ushuhuda huu wa nabii Yeremia ndipo Neno la Mungu litakapoleta

## *Kichwa Na Moyo*

baraka ambazo zimepangiwa kutujia katika maisha yetu. Yeremia anasema hivi: *Neno lake lilikuwa katika roho yangu kama moto unaowaka na umewekwa katika mifupa yangu.* (Yer. 20:9). Katika maisha ya walio na imani wengi, hamu kuu ya kuwa na imani asili ya Kikristo haipatikani. Hakuna uhusiano wa karibu kati ya akili kwe nye ubongo wetu wa kibinadamu na maisha ya wale walio na imani. Matokeo ni kwamba kuna uhusiano wa kiwango kidogo sana kati ya yale tunayoyajua na yale tunayoyafanya!

Pale mafunzo ya Maandiko Matakatifu yanapokushika katika roho yako, bila shaka yatabadili maisha yako. Hali hii inapotokea, basi utajikuta hutegemei sana usaidizi wa wataalamu na hata mikutano ya hapa na pale inayohusu maisha ya jamii. Na hii ni kwa sababu utakuwa unajua na kufahamu lengo la Mungu kuhusu maisha yako, na utajua ni yapi Mungu anatarajia kutoka kwako, na pia ni yapi ye ye yuko tayari kukutendea kupitia neno lake. Na kupitia nguvu ya Roho Mtakatifu ambaye yuko ndani yako, utaweza kufuata na kutimiza maagizo ya mwokozi wetu Yesu Kristo.

Wakati fulani baada ya kuhubiri, wako wale ambaao hujitokeza na kunitia moyo na matamshi kama: “Umenipa jambo la kuwaza juu yake.” Pale ninaposikia usemi kama huu, najua wazi kwamba sijatimiza lengo langu kuu ambalo nilinuia kulitimiza siku hiyo. Kuna tofauti kubwa pale Neno la Mungu linaposifiwa kwa ajili ya kuweza kumfanya mtu awaze kuhusu maana yake ya ndani, na pale neno hili linapomfanya mtu abadili mienendo yake kutokana

## KUZA IMANI YAKO

na ukweli ambaao uko pale. Kwa kweli, ujumbe wa Maandiko Matakatifu unastahili kumwelekeza mtu **kufanya jambo fulani**, sio tu kumfanya mtu awaze kuhusu jambo fulani.

Sawa na haya, ikiwa wakati wa *kuwa pamoja na Mungu* hautamfanya mtu afanye jambo fulani kuhusu hali ya imani yake; labda kuwa mtiiifu, ama kutubu dhambi, ama kumfanya aamue kutumia wakati wake zaidi kuabudu, basi wakati huo wa *kuwa pamoja na Mungu* utakuwa ni wakati ambaao **hauna** faida.

Pia, pale mtoto wa Mungu anapokuwa na kichwa kilichojaa na Neno la Bwana, nayo roho yake inatetemeshwa na nguvu ya Roho Mtakatifu, ye ye atafurahi kuishi akiwa katika ushirika na Mwokozi.

**Hata leo, ninapotembelea vyuo vya Biblia kama mkufunzi wa muda mfupi, mimi huwaambia wanafunzi wangu: “Hauko hapa kusoma Biblia ili upate ufahamu wake: uko hapa kusoma Biblia na mafunzo yake ili uweze kumjua Mungu aliye katika Biblia.”**

Hali ile ya kutokomaa kiroho ni ushahidi wa kuonyesha jinsi vile nguvu inakosekana katika matamshi ya kawaida kuhusu imani. Chochote ambacho unawacha kichukue nafasi ile ya kuwa karibu na Mungu pamoja na kitabu chako cha Maandiko Matakatifu kitafanya uhusiano wako na Mungu udidimie, na hata baadaye ufe.

Ushirika wa kweli na Mungu hutokea tu pale Mkristo anapokutana ana kwa ana na mwanga kutoka

## *Kichwa Na Moyo*

kwa Mungu. Mwanga huu hufichua yote na huhitaji ukweli katika mawasiliano kati ya mwanadamu na Mungu wetu aliye juu mbinguni. Ikiwa pale unaposoma neno lake, roho yako inakubali ukweli huu, basi hapo ukweli huu unakuwa chakula cha kiroho na hapa utastawi kiroho, na hata kimawazo katika kumjua Mungu. *Mwandishi wa zaburi alisema katika nuru yako, tunaona nuru* (Zab. 36:9)

Msemo huu wa zamani una ukweli hata na leo, na ni huu:

Mwanga unaofuatwa huleta mwanga zaidi;  
Nao mwanga usiofutwa huleta gizaa kuu  
usiku.

Sina shaka umegundua, sawa na jinsi vile mimi nimegundua kwamba ni rahisi kutoa ushauri kuliko kufuata ushauri unaopewa. Hata hivyo, Kristo ambaye katika Isaya anaitwa *Mshauri wa ajabu* (Isa. 9:6) ni wa ajabu kwa sababu yeye hatoi ushauri, bali yeye anatuwezesha pia kutimiza yale yaliyoko katika ushauri wake.

Kila asubuhi, wakati wako *kuwa pamoja na Mungu* wawenza kuwa ni wakati wamuhimu wa kukuandaa kwa ajili ya yale ambayo yanakungoja baadaye. Na pale kupitia kusoma neno lake Mungu, yeye anapokushauri, pokea hakikisho kwamba Kristo ana uweo na atakuwezesha na kukuendeleza katika yale yote ambayo yako mbele yako.

## **Ichunguze Roho Yako**

1. Je, moyo wangu hukubali kwa haraka sawa na akili na mawazo yangu yale ambayo nayasoma katika Biblia?
2. Pale ninapokuwa naomba, je, mimi huwa nina mawasiliano ya moja kwa moja na Mungu.
3. Katika maisha yangu ya kiroho, je, mimi hutafuta ushauri kutoka kwa mwanadamu au kutoka kwa Mungu? (Hebu waza kuhusu onyo katika Maandiko Matakatifu: *Wakayasahau matendo yake kwa haraka, Hawakulingojea shauri lake* (Zab. 106:13)).
4. Katika huduma yangu ya kiKristo, je, ushauri wangu kwao wenzangu hutoka ndani yangu; katika moyo uliojaa upendo wa Mungu, na mawazo yaliyojaa neno la Mungu? (Hebu tena waza kuhusu onyo katika Maandiko Matakatifu: *wakimwasi kwa mashauri yao* (Zab. 106:43)).





## **DHAMBI KAMA HIZI**

*Dhambi zisizo na hesabu natubu; dhambi zinazozidii  
kipimo...*

*Kujali mambo ya dunia wakati wa maombi; kujijali zaidi  
wakati wa kufanya kazi; Maringo wakati Mungu napita  
karibu nami; Uzembe wakati wenye dhambi wanakuwa  
katika giza;*

*Kujaribu na kuona kwamba Mungu ni mwema, kutamani  
vyakula vye nye sumu; Kwenye chemichemi ya anga  
kutafuta vile viliviyotengenezwa na wanadamu.*

*Dhambi kama hizi roho yangu yanadanganya, Wewe -  
peke yako anayezijua unahuzuniika!*

*O jinsi nimekosa usingizi kwa ajili ya uovu wa kila siku  
ambao haujanitoa machozi, Kuamkia kazi ya kiroho na  
nguvu; Na doa la maradhi katika mwili wangu*

*Bado pumziko lao halijaniacha, Bado mkono wako  
unaoponya unaapatikana, Angalia huzuni yangu kwa ajili  
yako O nisamehe Baba, nisamehe kupitia mwanao kwa  
ajili ya dhambi dhidi yako.*

— William MacLardie Bunting (1805-1866)

*Adapted by R. A. B.*

## *Kujianaa na Maombi*

Pale nilipompokea Kristo kuwa Mwokozi wa maisha yangu, niliyajua machache sana kuhusu Maandiko Matakatifu. Hata hivyo, niliweza kuhisi kila wakati nilipofungua Biblia kwamba yale niliyokuwa nayasoma yalikuwa ni Maandiko ambayo ni **neno la Bwana**. Hata leo, bado najawa na furaha kujua kwamba Kristo anazungumza nami pale ninaposoma neno lake.

Hata pale nilipokuwa mkristo mchanga, nilifundishwa kwamba ninapofungua Biblia yangu, Roho Mtakatifu ana hamu ya kuingia katika roho yangu na kuishi hapo. Kwa hivyo, nilikuwa naanza wakati wangu wa *kuwa pamoja na Mungu* na maombi, ambayo yalikuwa ni ombi ambalo nilifundishwa likiwa kama wimbo:

Roho wa Mungu, kuwa mwalimu wangu,  
Yafichue mambo ya Kristo kwangu, Niwekee  
mkononi ufunguo wa ajabu, Ambao  
utanifungua na kuniweka huru

## KUZA IMANI YAKO

Kabla hajaondoka na kuwaacha wanafunzi wake kwenda juu mbinguni, Kristo alisema hivi: “Pale yeye, Roho Mtakatifu wa ukweli atakapokuja, yeye atawaongoza katika kujua ukweli: *Lakin yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakin yote atakayoyasikia atayayena, na mambo yajayo atawapasha habari yake (Yn. 16:13)*. Ukweli ni kwamba kuna mwalimu mmoja, naye ni Roho Mtakatifu.

**Na ikiwa roho mtakatifu hayuko huru kufanya kazi katika maisha yetu, kusoma kwetu kwa Neno la Bwana kutakosa ladha na kuwa ni kitu kisicho na maana.**

John Wesley ambaye anajulikana sana Uingereza kwa ajili ya kazi yake kubwa ya kuhubiri, na hata ufuluo uliotokana na mahubiri yake ukazuia mapinduzi ya kijamii nchini humo, hata yeye aligundua umuhimu wa kutenga wakati fulani kuwa pamoja na Mungu. Yeye alijifunza funzo kuu ambalo hata sisi tunastahili kuiga. Wesley alifanya kazi ya kujizoesha kuingia kitandani mapema ili aweze kuamka mapema. Juzi niliweza kupiga magoti kwenye kitu kidogo ambacho Wesley alikitumia kuomba sawa na vile Wesley mwenyewe alikuwa akifanya. Katika chumba kile, nilisoma maandishi haya katika kitabu cha Wesley: Nakaa chini peke yangu. Ni Mungu tu pekee yake ambaye yuko hapa. Nikiwa naye, nafungua na kusoma kitabu chake, na

## *Kujianada na Maombi*

yale ambayo nasoma, nayafunza pia.

Ili kuwatia moyo wale ambaao wa mezaliwa mara ya pili, Mtume Yohana aliwaahidi kwamba Roho Mtakatifu anatosha kuwaguza roho kupidia Neno lake Mungu, na hata pale ambapo hawana watu wa kuwasaidia kuelewa Maandiko Matakatifu. Kwao, aliandika hivi: *Nanyi mafuta yale mliyoyapata kwake yanaka ndani yenu, wala hamna haja ya mtu kuwafundisha; lakini kama mafuta yake yanavyowafundisha habari za mambo yote tena ni kweli wala si uongo, na kama yalivyowafundisha, kaeni ndani yake (1 Yoh. 2:27)*. Pale unapotegejemea mwanga utokao kwa Roho Mtakatifu unaposoma Maandiko Matakatifu, yeye atafanya ukweli ulio ndani yake kuwa hai katika moyo wako.

Ikiwa una hamu ya kuwa na maisha yenye utajiri wa kiroho, kupitia muda wako wa *kuwa pamoja na Mungu*, ni sharti utafute mahali pa utulivu. Pia inakubidi utenge kando saa maalum ya kuwa pamoja na Mungu. Hapa basi utafungua Biblia yako na kuwa pamoja na Mungu. Ingawa wakati huu wa kuwa pamoja na Mungu ni wakati ambaao utafurahisha roho yako na kukuridhisha, uko wakati ambapo familia ama shughuli za kazi na mambo mengine yatajitokeza na kufanya upate ugumu wa kuwa pamoja na Mungu. Siku kama hizi zahitaji kwamba uwe na uwezo wa kujilazimisha kufuata utaratibu ambaao umejiwe kea wewe mwenyewe ili uwe pamoja na Mungu. Kumbuka Biblia ambayo haitumiwi ni sawa na Biblia ambayo hauna.

Sawa na jinsi vile Waisraeli walilazimika kujianada kabla ya kupata chakula chao manna kutoka kwa

## KUZA IMANI YAKO

Mungu wakiwa safarini kuelekea nchi walioahidiwa, sisi pia tunahitaji kujiandaa kabla ya kuchukua neno lake Mungu kuwa chakula chetu.

Kwanza: huenda likawa ni jambo la msaada kwako kupiga magoti pale unapofungua Biblia yako kuwa pekee yako mbele ya Mungu.

Pili: Unapokuja kwake yeye ambaye ni mwanga wa daima, kuna haja kufungua roho yako mbele ya utukufu wake. Hakuna lolote ambalo unastahili kumficha, kwa hivyo hakuna haja kujaribu kuficha lolote.

Na pale unapokuwa uko tayari kukutana na Mungu, Biblia inakuwa na uhai kwako, na hapo utaanza kujigundulia jinsi vile neno la Bwana lilivyo na uwezo wa kusonga kutoka kichwa chako kuelekea moyo wako.

## PIGA MAGOTI

*Ushirika Ulio Hai Hauwezi kustawi Pamoja na Roho  
Wa Majivuno.*

Katika Biblia, tunasoma kuhusu watu wengi wa imani ambao walionyesha heshima yao na unyenyekevu kwake Mungu kwa kuitia njia ya kupiga magoti. Ingawa wa kristo na hata waislamu katika maombi wao hupiga magoti au kuinama, haya yote huwa sio ishara kwamba wote wana ushirika na Mungu. Hata hivyo, tunapokuja mbele ya Mungu wetu aliye juu mbinguni hali ya mawazo na moyo wako waweza kusaidiwa sana ikiwa utapiga magoti.

## *Kujianada na Maombi*

Katika shamba la Gethsemane, pale Kristo alipokuwa anakaribia saa ile ya kusulubiwa, ye ye aliwaona wafuasi wake wakiwa wamelala. Aliondoka hapo, akapiga magoti na kuomba: *mwenyewe akajitenga nao kama kiasi cha kutupa jiwe, akapiga magoti akaomba* (*Lk. 22:41*). Kristo alikuwa yuko peke yake mbele ya Baba aliye juu mbinguni. Na hapa, **akapiga magoti** na kuomba. Sawa na hapa, pale tunapo jitenga kutoka kwa marafiki wetu na jamii sisi pia tutaona haja ya kuonyesha heshima yetu na kujitolea kwetu kwake kupitia njia ya kupiga magoti.

Pale mtume Paulo alipokuwa anakaribia kumaliza huduma yake kwa watu wote, ye ye alichukua muda fulani kuwa aga wanachama wa kanisa ambalo alikuwa ameanzisha Efeso. Tunasoma, *akapiga magoti, akaomba pamoja nao wote* (*Mdo. 20:36*). Akiwa katika ufuuo wa bahari wakati fulani, Paulo aliwaaga wafuasi wa Kristo, wake zao na hata watoto. Maandiko Matakatifu yanasema kwamba watu wote, pamoja na wake zao pamoja na watoto wao wa k atusindikiza mpaka nje ya mji, *tukapiga magoti pwani tukaomba* (*Mdo. 21:5*). Wengi wetu siku hizi tunaweza kuchukuwa kuwa makosa pale tunapowaona kina mama na hata watoto wakipiga magoti kuomba katika sehemu za hadhara. Katika siku hizi ambapo wengi wanachukuliwa kuwa shupavu wa dini ambaao hawatumii akili, sisi pia tunajikuta kwamba tunatosheka kujihusisha tu na mikutano ya kawaida ya maombi. Ni wazi kwamba wakristo pamoja na wake na watoto wakati wa mtume Paulo hawakuwa na shida kupiga magoti. Sisi pia inatupasa tusiogope

## KUZA IMANI YAKO

wala kuona haya kupiga magoti wakati wa kuomba kisiri siri au katika hadhara wakati wa kuwa pamoja na Mungu.

Lazima ikumbukwe jambo lililo la muhimu kuhusu wakati wetu kuwa pamoja na Mungu sio tu jinsi vile tunasimama au kukaa wakati wa kuwa pamoja na Mungu. Lile lililo muhimu ni hali ya mawazo yetu. Biblia yatuonya ni jambo la muhimu kuwa na nia njema wakati wa kuomba: *Mungu huwapinga wajikuzao, bali huwapa neema wanyenyekemu. Baasi, mtuuni Mungu. Mpigeni Shetani, naye atawakimbia. Mkaribieni Mungu, naye atawakaribia ninyi* (Yak. 4:6-8).

Kwa ajili ya shida fulani katika miili yetu, wengine wetu huenda tusiweze kupiga magoti kwa muda mrefu. La kufurahisha ni kwamba Mungu mwenyewe anaangalia na kuona ndani ya mioyo yetu. Bila shaka Mungu ana hamu na yale yaliyo katika roho zetu, kuliko hali tuliyomo wakati wa kuomba. Hata hivyo, kupiga magoti ni njia moja kubwa ambayo humsaidia yeoyote anayeomba kujua kwamba yuko katika ushirika na yule aliyetuumba sawa na jinsi vile mtu hushirikiana na mwenzake kupitia mazungumzo. Kwetu sote, lile lililo la muhimu ni kwamba ni sharti *tunyenyekkee mbele ya Bwana*, na tunapotii wito huu, Mungu naye anaendelea kutimiza agizo lake jinsi vile neno lisemavyo: *Jidhilini mbele za Bwana naye atawatukuza* (Yak. 4:10).

***Kujiardaa na Maombi***

**JIWEKE WAZI MBELE YA BWANA**

***Ushirika na Mungu unaodumu huwa na chanzo  
chake katika kiti chake cha huruma cha Mungu***

Hata kabla Mwokozi wetu Yesu Kristo hajakufa pale juu msalabani, Mungu, katika utukufu wake na rehema aliamwa kwamba mwanawewe wa pekee asiye na kosa atakufa kifo ambacho ni gharama inayolipia makosa yetu sisi wanadamu wapotovu; na hii ilikuwa hivyo ili mwanadamu aweze kurudia upya ushirikiano wa hapo awali na Mungu. Kabla ya Mwokozi wetu Kristo kusulubiwa, tayari Mungu alikuwa amesema ni katika kiti cha rehema ambapo angekutana na wale wanaomhudumia. *Nami nitaonana nawe hapo, na kuzungumza nawe pale nilipo juu ya kiti cha rehema (Kut. 25:22).*

Leo hii, dhabihu au toleo kwa ajili ya dhambi zetu ni matukio ambayo yametokea na twaweza kutoa ushahidi wake sawa na jinsi vile wataalamu wa historia wanavyofanya. Damu yenye dhamani kubwa kutoka kwa Kristo imemwagika kwa ajili ya dhambi zetu, na kwa kupitia damu hii iliyomwagika, njia mpya iliyona uhai imefunguliwa ili tuweze kuwa na ushirika na Mungu Baba. Upendo wake usio na kifani unatufanya tuseme na furaha: *Basi na mkikaribie kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji (Ebr. 4:16).*

KUZA IMANI YAKO

**Neema ina maana kwamba Mungu ametupatia  
kile ambacho hatustahili kupata. Ni furaha ilioje  
kwamba tunaweza kuwa na ushirika na kutembea na  
Mungu mwenye neema na rehema.**

Kutoka Kwenye mawimbi yanayovuma,  
Kutoka kwa mawimbi makali ya shida,  
Kuna mahali pa kujificha,  
Na hapa ni chini ya kiti cha neema.

Kuna mahali ambapo kivuli cha Kristo  
kinapatikana,  
Mafuta ya furaha katika vichwa  
Mahali ambapo kwangu ni pa tamu;  
Hapa ni kiti cha neema ambacho kimenunuliwa  
na damu.

Kuna mahali ambapo Roho hukutana,  
Mahali ambapo rafiki huwa na ushirika na  
rafiki;  
Ingawa wanatafautiana, kupitia imani, wao  
wanakutana  
Katika kiti cha rehema.

Ah! Niwapi tunaweza kukimbilia ili tupate  
msaada,  
Wakati wa majoribio, kufa moyo na kuwa  
wanyonge,  
Au jinsi ya kumshinda yeye mwovu,  
Wakati watakatifu hawana kiti cha rehema.

## *Kujianadaa na Maombi*

Pale kwenye mabawa ya tai twapaa,  
Na saa na hata hali ya kuhisi haipo,  
Na mbinguni yakuja chini kusalimia mioyo yetu,  
Na utukufu kuwekwa kwenye kiti cha neema.

*H. Stowell*

### **Ushirika Ulio Hai Na Mungu Hauwezi kustawi Pamoja na Mawazo Ya Uovu**

Kijana ambaye amezaliwa katika familia fulani, ataendelea kuwa mtoto wa wazazi wake milele. Hawezi kuzaliwa tena ili awe mtoto wa wazazai tofauti. Lakini mtoto yule akiwa mtukutu, basi kuna wakati ambapo mawasiliano kati yake na wazazi wake yatavunjika. Uhusiano kati ya mtoto na wazazi ungalipo, lakini mawasiliano kati yao yamevurugika na hayapo. Hakuna ushirika kati ya mtoto na wazazi! Hii ni balaa kuu.

Ni jambo la ajabu na la kufurahia kwamba pale tulipozaliwa mara ya pili, uhusiano wa milele ulifufuliwa kati yetu na Mungu wetu aliye juu mbinguni. Tukimpokea Kristo katika mioyo yetu, sisi tutakuwa wana wa Mungu, na uhusiano huu utadumu milele. Hata hivyo pale tunapoteda dhambi, uhusiano huu unavunjika vibaya.

Kwa ajili ya kutokuwa watiifu, hatutafurahia kuona uso wake wa kicheko cha furaha; uso ambao tumezoea na kufuruuhia kuuona. Kuvunjika huku kwa uhusiano wetu hakuwezi kuwa ni kwa sababu ya Mungu; au hali yake ya kutojali. Kuvunjika huku kwa uhusiano wetu na Mungu ni kwa ajili ya kuchafuka



## KUZA IMANI YAKO

kwa roho zetu. Ni sisi wenyewe tumeharibu uhusiano kati yetu na Mungu.

**Dhamiri Chafu;** John Bunyan aliwahi kusema hivi: “Dhambi itanielekeza mbali na Biblia. Nayo Biblia itanielekeza mbali na dhambi.” Pale mtu anapomtia uchungu Roho Mtakatifu kupitia kutenda dhambi, na kuamua kutenda dhambi bila kumjali, yeye hypoteza hamu ya Neno la Bwana. Mkristo anahitaji roho safi na hii ndio itamu wezesha kuja kwa neno la Bwana. Biblia inasema hivi: *Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao (Ebr. 11:6).*

Hata hivyo, tukizidi katika dhambi, tunaposoma Biblia, imani yetu itapoeshwa kwa sababu dhamiri yetu haisikilizani na ile ya Roho Mtakatifu.

**Dhamiri Safi:** Ili kuanzisha upya ushirika wetu na Mungu baada ya kutenda dhambi, kuna haja dhamiri yetu ambayo imejaa dhambi isafishwe. Ili kuondolea mbali mzigo huu wa dhambi, Mkristo aliye na dosari la dhambi anahitaji kujifungua na kutubu mbele ya Mungu. Mtume Yohana anasema hivi:

*Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote (1 Yoh. 1:9).*

Katika sehemu hii ya Maandiko Matakatifu, nimeandika ombi ambalo lilikuwa ombi lake F.W.



## *Kujianada na Maombi*

Krummacher. Pale ninapogundua dhambi zangu, na jinsi vile nimelemewa na dhambi hizi, najaribu kutaja dhambi hizi mbele ya kiti cha rehema cha Mungu. Halafu baadaye naomba ombi lake hili Krummacher, nalo likiwa msingi wangu wa kutubu mbele ya Mungu;

O Mungu wangu, nimetenda dhambi mbele yako, na dhambi hii inanisikitisha. Najitolea hukumu mwenyewe, hukumu kali. Lakini rehema zako ni nyingi mno, na hapa ndipo naweka tumaini langu. Inyunyizie dhamiri yangu na damu ya utakaso, na uniwezeshe kwa njia ya imani kufanya yale ya kuniondolea mzigo wa dhambi hii, na mateso ambayo umevumilia kwa ajili yangu.

Tunapotenda uovu machoni pa Bwana, hatutendi dhambi hizi kwa kikundi; kwa hivyo, haiwezekani kutubu dhambi hizo zote na ombi moja tu. Kujaribu kuomba ombi moja na kupitia ombi hili kutaka kusamehewa dhambi zote ambazo tumetenda si jambo zuri. Upo uwezekano wewe kufanya hivyo kwa ajili ya maringo yanayokufanya usikubali kwamba umetenda dhambi. Ombi moja linalohusu dhambi nyingi huwa haliwezi kukuondolea vikamilifu mzigo wa dhambi. Pale Roho Mtakatifu anapokujulisha kuhusu dhambi - lazima tutaje dhambi ile na jina lake ambalo Biblia inatumia kutaja dhambi hiyo. Lile tunasema hapa ni kwamba lazima tuite ‘dhambi’ na jina lake hilo ambalo ni ‘dhambi.’ ‘Uongo’ tuuite

## KUZA IMANI YAKO

‘uongo’, ‘usinzi’ tuuite ‘usinzi’, ‘hasira’ na ‘uchoyo’ tuuite na jina hilo hilo mbele ya Mungu wakati wa kutubu dhambi hizi.

Kwa vile shida tuliyonayo ni ile ya kuwa watu walio na makosa na wenye dhambi, hakuna haja ya kutumia mawazo na akili kufanya dhambi ile isionekane, ama kutafuta sababu ya kufanya dhambi isijitokeze wazi pale tunapomkaribia Mungu. Unapotaja dhambi yako na unyenyekevu, Mungu naye, kwa ajili ya wingi wa rehema zake na huruma ataitikia ombi lako. Haya ndio maajabu ya neema ya Mungu.

Baada ya mfalme Daudi kutubu dhambi yake kuu, yeye alifurahi sana kuona wema wake Mungu kiasi hata akasema: *kiasi cha wingi wa rehema zako, uyasufe makosa yangu* (Zab. 51:1). Yale yaliyo katika Zaburi hii ya 51 yaonyesha kwamba mfalme huyu, alipomkaribia Mungu, yeye kweli alikuwa anaungama dhambi zake, akiwa amevunjika moyo na kunyenyekea. Pia alifanya haya akiwa anataja ukweli kabisa wa mambo jinsi vile ilivyokuwa katika roho yake, na pia toba yake ilikuwa ya kutoka ndani ya roho yake. Unapotubu, yaani, unapogundua kwamba umefuata barabara yako mwenyewe na kutoka kwa ile ya Mungu, na sasa una hamu ya kurudi kwa njia bora ya utukufu, basi hapa inakubidi utubu kwa ukweli ukitaja kila dhambi ambayo umetenda kwa jina lake mbele ya Mungu. Ukipanya hivyo, basi sawa na mfalme Daudi utafurahia kuona mkono wa neema ya Bwana unaokuondolea doa la dhambi. Ni baada ya hapo dhamiri yako itakuwa safi, na hivyo kuweza tena kurudi kuwa na ushirika na Mungu aliye mtakatifu.

## *Kujianada na Maombi*

Na hapo dhamiri yako itakuwa imesafishwa. Kupitia kumpenda Mungu, utajikuta kuwa na nguvu zaidi katika maombi.

*Basi ndugu, kwa kuwa tuna ujasiri wa kupaingia patakatifu kwa damu ya Yesu, njia ile aliyotuanzia iliyo mpya, iliyo hai, ipitayo katika pazia, yaani mwili wake; na kuwa na kuhani mkuu juu ya nyumba ya Mungu; na tukaribie wenye moyo wa kweli, kwa utimilifu wa imani, hali tumenyunyiziwa miyo tuache dhamiri mbaya, tumeosha miili kwa maji safi (Ebr. 10:19-22).*

Nguvu kamili mbele ya Mungu hutoka kwa dhamiri iliyo safi. Moyo ambao haufichi chochote, na ulio na ukweli huonyesha wazi imani iliyo na nguvu ambayo ni sharti kuu la kutimizwa ili uweze kufurahia maisha ya kuwa na ushirika wa karibu na Mungu.

Pale unajua wazi kwamba moyo wako hauna uchafu, basi dhambi zako za hapo nyuma hazitatatiza dhamiri yako. Ni wazi Shetani atajaribu kukushambulia, lakinji jibu lako lafaa liwe kama lile la Mungu kuhusu dhamiri yako iliyojaa uovu. Jibu lenyewe ni hili: kwamba damu ya Mwokozi wetu Yesu Kristo imeosha dhambi zako zote. Katika kitabu cha Ufunuo, wateule ambao walikuwa wanalaumi wa na shetani kwa ajili ya dhambi zao za hapo mbele ni ambazo tayari walikuwa wamepokea msamaha kutoka kwa Mungu, walielewa vyema nguvu kuu ambazo hupatikana katika damu ya Kristo iliyomwagika msalabani. Na kuwahuksu hawa,

## KUZA IMANI YAKO

twasoma hivi: *Nao wakamshinda kwa damu ya Mwana-kondoo* (*Ufu. 12:11*). Sio tu kwamba walifurahia baraka zilizotokana na dhamiri zilizosafishwa, ila pia walikuwa wamejifunza sisri ya kuwa na dhamiri ambayo haihangaishwi. Halleluya!

### **Ushirika Ulio Hai Hauwezi Kudumu Pamoja na Mawazo Yaliyopotoka**

Kuna sababu iliyojificha ambayo huwafanya wengi wasipende maziwa yanayofaa ambayo yanapatikana katika neno la Bwana. Je, umewahi kuwa na homa kali ambayo imekufanya hata upoteze hamu ya chakula? Haijalishi chakula ni kitamu kiasi gani; hamu ya kula chakula chenyewe huwa imepotea. Sawa na chakula kitamu wakati huna hamu ya kula, Biblia nayo haitakuvutia ikiwa mawazo yako yamepotoka. Mawazo yaliyopotoka hukuondolea kiu na hamu ya chakula cha kiroho.

Ingawa mtume Petro anatutia moyo tuwe na hamu ya chakula cha kiroho ambacho amekitaja kuwa ni *maziwa ya akili yasiyoghoshiwa* (*1 Pet. 2:2*), Yeye anaanza kwanza kwa kutuonya kuhusu mwelekeo na hali ambayo yaweza kuharibu na kutuondolea hamu ya chakula cha kiroho kutoka kwa Mungu. Ni wazi anatilia mkazo kwamba kuna njia moja ya kukumbana na vikwazo ambavyo hufunga uwezo na njia yako kuwa na wakati wa pamoja na Mungu. Kila kikwazo ambacho ni pingamizi inayozuia wewe kuwa na wakati wa pamoja na Mungu lazima kiwekwe kando. Mawazo yaliyopotoka ni lazima yabadilishwe kimsingi kabla ya hamu ya chakula cha kiroho kuturudia. Hii ni njia

## *Kujianada na Maombi*

moja ya kusema hivi, tubu dhambi! Ukitubu dhambi utaweza kuwa na wakati wa pamoja na Mungu. Katika waraka wa kwanza wa Petro tunasoma hivi:

*Basi wekeni mbali uovu wote na hila yote, na unafiki na husuda na masingizio yote. Kama watoto wachanga waliozaliwa sasa ya tamanini maziwa ya akili yasiyoghosishwa, ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu (1 Pet. 2:1-2).*

Maandiko Matakatifu yanasema hatutawahi kuwa na hamu na maziwa halisi ya neno mpaka pale vizuizi ambavyo ni sawa na ugonjwa wa kiroho vitakapokuwa vimeondolewa. Hebu tuchambue vizuizi vyenyewe.

**Nia Ya Kuwadhuru Wenzetu (Malice):** Hii yahusu dharau na hasira inayotokana na jinsi vile mtu ametendewa na wenzake. Hali ile ya kukosa moyo wa msamaha.

Corrie Ten Boom alivumilia taabu na maafa ya aina aina katika kambi ya wa NAZI ya mateso pale Ravensbruck. La kuhuzunisha sana lilikuwa pale aliposhuhudia dada yake mpendwa akififia kwa ajili ya mateso aliyokumabana nayo katika kambi ile. Akizungumzia kuwahuusu askari wasio na msamaha waliomtesa yeeye na wenzake, Corrie Ten Boom alisema hivi:

**“Kusamehe ni jambo ambalo latokana na nia ya mtu; unaweza kuwa na nia ya kusamehe hata pale roho yako imechafuka kiasi gani.”**

## KUZA IMANI YAKO

Ikiwa katika roho yako bado umeweuka hasira na hujawasamehea wliokukosea, hata kama ulikosewa kiasi gani, hali yako ya kukosa kusameheea mwenzako haitamdhuru yeye aliyekukosea, ila itanyonga maisha yako ya kiroho. Utakuwa mfungwa kwa huyo ambaye hujamsamehe mpaka pale utakapokuwa na nia ya kumsamehe. Ni baada ya hapo utaweza kuomba ombi ambalo Bwana wetu alitufunza: *Utusamehe dhambi zetu, kwa kuwa sisi nasi tunamsamehe kila tumwiaye* (*Lk. 11:4*). Ikiwa unajua una roho ya kutosamehe, jiandae na ujitalidi kumsemehe uyo aliyekukosea katika wakati wako wa kuwa pamoja na Mungu na hapo utaweza kueleza upendo wa Mungu kwao wanaokukosea bila kuwa mtu ambaye ni mwongo.

**Ujanja (Guile):** Hali ya kuficha pale kukosa kwetu kuwa na uwezo fulani badala ya kukubali na kutubu dhambi zetu - kuishi maisha ya uongo pasipo ukweli.

**Udanganyifu wa Moyo au Kujisingizia Wema (Hypocrisy):** Kujisingizia wema kwa ajili ya kiburi na majivuno lengo likiwa kutaka kuonekana kuwa tofauti na jinsi vile ulivyo.

**Wivu au Kijicho (Envy):** Kujifanya kwamba umesurahia yale mazuri ambayo yamemjia mwenzako.

**Matamshi ya Uchafu (Evil Speaking):** Matumizi ya ulimi kuwatia uchungu wenzetu, au kuwachafulia sifa, ama kusikiliza matamshi ambayo lengo lake ni kuchafulia mwenzetu sifa, kujaribu kuficha uovu

## *Kujianada na Maombi*

wetu kwa kumwelekezea kidole mwenzetu na kuzungumzia juu ya uovu wake.

Haya yote ni mambo ambayo tunahitaji kuyaweka kando ikiwa kweli tuna hamu kulishwa na neno. Sawa na jinsi vile mtoto mchanga hahitaji kushawishiwa ili anyonye pale anapokuwa na njaa, pale unapofungua Biblia yako, *utatamani maziwa ya akili yasi yoghoshiwa* (*1 Pet. 2:2*).

### **Ushirika Ulio Hai Hauwezi kukaa pamoja na hali ya Kujidhamini Kuliko Vyote vingine**

Juzi nilisoma barua kutoka kwa dada mmoja ambaye amekuwa mmisionari nchini Japan kwa muda wa miaka mingi. Yeye huwahudumia watu ambao sio rahisi kuwafikia, na hasa katika ngazi za juu serikalini na katika mazingira ya kidiplomasia. Aliandika hivi:

“Sijui ni nini kimetokea kuhusu mafunzo yale ya kujitoa mhanga na kuubeba msalaba wako mwenyewe. Nilipokuwa napanga vitabu vilivyohusu maisha ya kikristo, jambo mmoja lilijitokeza - kwamba vitabu vingi ambavyo vimechapishwa miaka ishirini hivi iliyopita vinahusu jinsi vile mtu anavyoweza kujisaidia na kujiendeleza binafsi katika maisha ya kiKristo. Nakumbuka wakati wa ujana wangu vitabu vingi vilibusu kujitoa, kuubeba msalaba kila siku, na kuishi maisha ya utukufu, kuitia

## KUZA IMANI YAKO

kujiweka kwake Kristo, na kumkubali aishi katika nafsi yangu. Je, mafundisho hayo yanapotea au ni mimi ambaye ninawaza kwa njia hii?”

Labda haya ndio kiongozi mmoja kutoka China alimaanisha pale aliposema: ‘Katika magharibi, na hata katika ulimwengu ulio huru, naona kanisa likijumuika zaidi na ushindi ulio katika kufufuka kwake Kristo. ‘Wao wanataka uhusiano wa aina hii. Wana hamu na ushindi, na utajiri na vyote ambavyo ni vizuri kutoka kwa mwana wa Mungu. Wachache sana wanataka kujihusisha moja kwa moja na mateso na shida ambazo mwokozi alipitia. Hata hivyo naona hali tofauti katika kanisa la Asia, na sana sana katika sehemu ambapo hakuna uhuru wa kutosha. Walio na imani huku wako tayari kuwa na ushirika na kuwa sehemu ya mateso ya Kristo aliyesewa. Kwao, *ushirika ambao unahusu mateso ni kama zawadi kuu kwao.*”

### ***Kufananisha na Kifo Cha Mwokozi***

Mtume Paulo mwenyewe aliomba hivi:

*ili nimjue yeye, na uweza wa kufufuka kwake, na ushirika wa mateso yake, nikifananishwa na kufa kwake (Flp. 3:10).*

## *Kujianada na Maombi*

Amosi aliweza kuelewa vyema maana ya kile ambacho Mtume Paulo anataja hapa aliposema: *Je! watu wawili waweza kutembea pamoja, wasipokuwa wamepatana* (Amo. 3:3). Ikiwa tuanataka kutembea katika nguvu zinazotokana na kufufuka kwake, basi ni sharti tuwe tayari kushiriki naye katika mateso na taabu alizokumbana nazo yeye aliye Mwokozi wetu. Makubaliano ya nusu tu sio makubaliano kamwe!

Katika sehemu nyingine, mtume Paulo aligusia yale yanayohusu mapenzi ambayo yanatatizika pale alipowaandikia wale ambaao alikuwa amewaongoza kuwa na imani walipokuwa wameanza kumfa nyia dharau. Yeye alisema hivi: Nami kwa furaha nyingi nitatapanya, tena nitatapanya kwa ajili ya roho zenu. Je! Kadiri nizidivyo kuwapenda sana, ninapungu kiwa kupendwa? (2 Kor. 12:15). Katika sehemu nyingine, alichambua swali hili la mapenzi na kusema upendo huvumilia, hufadhili; *upendo hauhusudu; upendo hauhusudu; upendo hautakabari; haujivuni; haukosi kuwa na adabu; hautafuti mambo yake; hauoni uchungu; hauhesabu mabaya...* (1 Kor. 13:4-5).

Upendo huu wa kweli, ambaao ulivumilia taabu, bila choyo, ulijifichua kikamilifu katika maisha ya mwokozi wetu Yesu Kristo. Pale Kristo alipokuja katika ulimwengu huu ambaao haukuwa na upendo, yeye alionyesha wazi mapenzi ya Mungu yakiwa mfano wa mwanadamu. Matendo yake, hata matamshi na kujitolea kwake kufa nya kila alichohitajika kufanya na Baba yake aliye juu mbinguni, huu ulikuwa mfano kamili wa mapenzi



## KUZA IMANI YAKO

ambayo sio ya kujitakia mema. Kutoka utotoni hadi pale aliposulubiwa, Kristo alikataa kutumia uwezo aliyokuwa nao akiwa mwana wa Mungu kujitimizia matakwa yake mwenyewe.

Katika muda wa miaka 33 alipokuwa hapa duniani, Kristo alijitoa *kwa kuwa yeye aliutoa uhai wake kwa ajili yetu* (1 Yoh. 3:16) kwa ajili ya kuendeleza wanadamu. Na pale alipokuwa katika hali ya uchungu pale msalabani...:

*Yesu, hali akijua ya kuwa saa yake imefika, atakayotoka katika ulimwengu kwenda kwa Baba, naye ali amewapenda watu wake katika ulimwengu, aliwapenda upeo (Yoh. 13:1).*

Ni kweli, upendo wa ke ultaabika kwa **muda mrefu**. Tukitaka kweli kuwa na ushirika na Mwokozi wetu, swalii kuu ambalo lazima tujiulize ni hili:

**Je, natumia faida inayotokana na uhai niliopewa na Mungu kwa ajili ya kuendeleza nafsi yangu; au niko tayari kuyatoa maisha yangu kwa ajili ya upendo halisi niliyo nayo kwa wenzangu, hata kama upendo huu unaweza kutuletea taabu na mateso.**

Upendo wa Mungu unatafautiana sana na mtindo wa siku hizi ambapo lile ambalo linatiliwa umuhimu sana ni mtu kujijali yeye mwe nyewe kwanza: na kwamba haki za mtu zina umuhimu kuliko mambo yanayowahusu watu wengine. Ni hii kuabudu ubinagsi moja ya ishara ya siku za mwisho:

## *Kujianada na Maombi*

*maana watu watakuwa wenye kujipenda wenyewe, wenye kupenda fedha, wenye kujisifu, wenye kiburi, wenye kutukana, wasiotii wazazi wao, wasio na shukrani, wasio safi, wasio wapenda wa kwo, wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziaji, wasiojizua, wakali, wasiopenda mema, wasaliti, wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu (2 Tim. 3:2,4).*

Si ajabu hata Alexander McLaren alisisitiza kwamba barabara ya kuelekea wokovu ulio wa hali ya juu imeja na nyayo zenyne damu inayotokana na maumivu ya upendo wa kibinafsi.

Dhambi inayojitokeza na kitendo au mawazo ni ishara inayoonyesha hali ile ya kujipenda. Oswald Chambers aliwahi kusema kwamba uchoyo ni sawa na kusema: “una haki juu yako mwenyewe.” na kwamba kuna hatari kuwa na imani ya aina hii. Ni vizuri kushutumu uchoyo na unyama unaotendewa watu wakati wa wizi na dhuluma mbali mbali, hata hivyo lazima tukumbuke kwamba dhambi ya uchoyo hujitokeza kwa njia ambayo ni yakujificha. Si ajabu chanzo kikubwa cha mafarakano katika familia, jamii na hata makanisani ni ule moyo wa mtu kujali mambo yake mwenyewe kuliko yale yanayowahusu wenzake. Mawazo kama haya: muda wangu ni haki yangu, pesa zangu, tamaa yangu, kusudi langu... haya yote ni mambo ambayo yamekuwa ni chanzo cha shida nyingi mno. Chochote ambacho hakionyeshi upendo wa Mungu, ambacho kina hamu ya kuendeleza ubinafsi - hii ni njia moja inayooonyesha wazi uchoyo wetu sisi wanadamu.



## KUZA IMANI YAKO

### JINSI NIONAVYO MBINGUNI

Njia moja ya kutuwezesha kuona uchoyo wetu ni kupidia kujiangalia kana kwamba ni Mungu anayetuangalia. Swali tunafaa tujiulize ni hili: Je, Mungu ananiona kuwa mtu wa aina gani? K atika kitabu *Letters to the Young Churches*, J.B. Phillips anagusia ombi la Mtume Paulo kwa wa Kristo Kolosai kwa njia hii:

*Tunamuomba Mungu kwa mba awawezeshe kuona yote kulingana na jinsi vile yeye anavyoona kupitia kupokea uwezo wa kiroho wa kuona (Kol. 1:9).*

Ni pale tu tunapofuata mfano wa Paulo na kuomba Mungu atufungulie macho ya kiroho ndipo tutakapoanza kuona na kuelewa hali yetu ya maisha, na sawa jinsi tulivyo na uchoyo, na jinsi vile Mungu anavyotuona. Ni kwa njia hii tutaweza kuona ukweli wa maisha yetu na hasa jinsi tulivyo machoni pa Mungu.

Usiku mmoja, Bii Silence ambaye ni rafiki wetu wa zamani mimi na mke wangu Dorothy alipata utulivu mkubwa pale alipoomba na kwa utulivu akatilia maanani maombi hayo wakati alipopatwa na msiba. Ilikuwa ni karibu saa nane ya usiku mama huyu alipopata simu. “Je, Unajua ni nani amekuwa akiendesha gari lako?” afisa wa polisi alimuuliza. “Ndio najua. Watoto wangu wawili vijana. Wanatoka mkutano wa injili.” Mama akajibu. “Nina habari za kukuhuzunisha,” Afisa yule akaendelea.

## *Kujianada na Maombi*

“Dereva wagari lenyewe alishikwa na usingizi; na gari likagonga mti. Dereva huyu amekufa, naye mwenzake huenda asipone.” Habari hizo zilimshtua sana mama huyu ambaye daima alikuwa na mapenzi yasiyo na kifani ambayo aliya elekeza kwa watoto wake hawa wawili.

Mama huyu aliweka chini simu ile, na akaanza kuomba hivi: Mungu wangu, mama mzazi kama mimi anaweza kufanya nini wakati kama huu? Uzuri ni kwamba mama huyu alikuwa anajua jinsi ya kufikiria na kuwaza kulingana na jinsi vile Biblia humpasa mtu kufanya. Aliniambia baadaye kwamba kile alichoweza kuwaza juu yake wakati ule ni ukurasa mmoja katika Maandiko Matakatifu unaosema *shukuruni kwa kila jambo* (*1 The. 5:18*). “Lakini Mungu,” mama yule aliendelea. “Unajua kwamba wakati huu moyo wangu hauwezi kukushukuru. Noyo wangu uko baridi, umeshtuka na hauna chochote ndani yake. Hata hivyo, usiku huu mgumu, mimi nitatii neno lako. Na ninapokutii wakati huu, tenda mwujiza katika maisha yangu. Ninapokutii na kukushukuru, ni lazima nione mkono wako kwa sababu wakati huu wa msiba, naona ni vigumu sana mimi kukushukuru.” Na kwa ajili ya kuomba hivi, mama huyu alikuwa ametumia imani yake na hapo akaanza kuomba.

Mama huyu aliniambia hata pale alipomshukuru Mungu mara ya kwanza, moyo wake ulikuwa bado ni mgumu, baridi na wenye upweke. Lakini pale alipoendelea na maombi, roho mtakatifu akatenda muujiza wa ajabu. Akajaza moyo wake na utulivu

## KUZA IMANI YAKO

na uwezo wa kushukuru kwa njia ya kweli kabisa. Kwa kweli, usiku huo, Roho Mtakatifu alijibu ombi lake mama huyu kwa ajili ya imani na utiifu wake. Roho Mtakatifu akamhakikishia kwamba upendo wa Mungu kwake na familia yake ni wa milele na haubadiliki. Ilipokaribia asubuhi, bado machozi yalikuwa yakimtoka machoni, lakini wakati huo, ye ye aliweza kuhisi kitulizo cha Mungu kikiwa katika roho yake.

Kwa kweli huu ni ushuhuda wa ajabu; kuona upendo na neema ya Mungu ikimzingira mama huyu wakati wa msiba. Bii Listen alisema usiku ule amani ya Bwana ipitayo ufahamu ilimjaa na kububujika. Na jinsi vile Bii Silence alithibitisha kupitia kutegemea Mungu wakati wa msiba, kuna tofauti kubwa sana jinsi vile wanadamu wa kawaida na wale walio na Roho Mtakatifu hukumbana na shida.

Unapozidi kuwa na uhusiano wa karibu sana na Mungu, hata wewe utakuja kujua kwamba shukrani na imani ni vitu ambavyo huwa ni vya pamoja. Pale shukrani inayotokana na imani yako ya kweli hujaa katika roho yako, Mungu atakusaidia kuweza kuona vyema mabadiliko ambayo yanajitokeza katika maisha yako - yawe mazuri au mabaya kulingana na jinsi vile Mungu anayaona. Yeye atakuonyesha *katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema, yaani, wale walioitwa kwa kusudi lake* (Rum. 8:28). Faraja iliyo katika Maandiko haya Matakatifu haifai kuwa ni ukweli ambao ni kitu kilicho baridi, kilcho pweke na cha kutajwa. Mungu

## *Kujianada na Maombi*

ametupatia agizo hili ili liwe kama muujiza ambao tumepokea katika miyo yetu na kuelewa. Kwa hivyo msifu Mungu pale unapohisi hali kama hii. Msifu pia pale hauhisi hali kama hii. Endelea kumsifu Mungu mpaka pale utakapohisi hali kama hii. Hakutawahi kutokea wakati maishani pale ambapo itakuwa ni vigumu kumsifu na kumshukuru Mungu.

Juzi, mimi pamoja na Dorothy tulipokea barua kutoka kwa wamishonari wazee ambao kwa muda mrefu wamefanya kazi ya huduma ya kueneza injili katika taifa moja mashariki ya kati. Katika barua yake, Stan alisema: "Ni sharti, tena lazima nimshukuru Mungu kwa ajili ya sifa yake, sio kwa ajili ya mazuri ambayo yamenijia." Kutilia nguvu yale ambayo Corrie Ten Boom alisema kuhusu msamaha, twaweza kusema pia kwamba kwa vile kumshukuru Mungu ni jambo linalogusia nia ya mtu, twaweza kuamua kumshukuru Mungu bila kujali hali ya moyo wetu. Na pale tunapochagua kumsifu Mungu, ye ye atatupa utulivu wa ndani ya roho, amani na uhakikisho wa jinsi vile mapenzi yake hayabadiliki katika kila hali ya mambo.

Inafaa kuangalia na kujua kwamba hatujahimizwa kusema **ahsante** kwa Mungu kwa ajili ya matukio fulani tu; ila kutoa ahsante katika kila hali.

**Shukrani ya kweli ambayo inatokana na kuona na kuelewa jinsi vile Mungu naye anatuona ni sehemu ya imani ambayo hutofautisha kati ya kujionea huruma na huzuni. Kumbuka kwamba hali**

## KUZA IMANI YAKO

**hii ni ya kweli na hajjalishi kama tuko kanisani ama katika hospitali.**

Hata pale tunayumbishwa na shida na michafuko maishani, moyo wa yule ambaye ni wa hapa duniani hujikuta kwa haraka ukiwa katika hali ile ya kujionea huruma. Moyo wa yule ambaye nyumbani ni mbinguni mara nyingi humshukuru Mungu katika kila hali ya mambo.

Wengi wetu huanguka na kuzirai pale tunaposhikwa na uchungu, tunakaa karibu na kiti cha enzi chake Mungu na kuhuzunika. Hata huruma inayotoka kwa wakristo pia huzidisha hali hii. Lakini katika mapenzi yake, Mungu kamwe hafanyika hayo. Yeye huja na mkono uliounjika Mungu anaweza kufanya yale anayonua yatendeke kuja kutimia hapa duniani, basi ni vyema kumshukuru kwa ajili ya kukuvunja moyo. (Oswald Chambers, *My Utmost for His Highest*)

Tilia Maanani upendo wa Mungu ambao ndio sababu ya “*kila jambo*” maishani. Msitari unaofuata unatuonyesha wazi kwamba kusudi ni hili: “*tuweze kuwa kama yeye.*” (*Rumi 8:29*)

Ni kweli kama inafaa kuelewa jinsi vile Mungu ametupatia uhuru uliyo na neema kutoka kwa miili

## *Kujianaa na Maombi*

yetu, ni bora tujifunze kuangalia maisha yetu na macho sawa na yake yeye aliye juu mbinguni.

Mungu hujibu yule ambaye anaishi maisha ya kujali nafsi yake; sio kuititia kujiendeleza ama elimu, ila ni kuititia kifo! Pale tunapokumbwa na mvuto wa hamu ya kutaka kulinda na kuendeleza nafsi yetu hapa duniani, imani ya kweli itatuwezesha kufurahia ukweli wa milele kutoka kwake Mungu *Kwa maana mlikufa, na uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu* (Kol. 3:3).

Na kwa vile **tumefichwa pamoja na Kristo katika Mungu**, kuititia kifo, kuzikwa na kufufuka (Rum. 6:2-4)—tumetolewa kabisa kutoka maisha haya ambayo mwisho wake ni hapa duniani na hali ile ya kujali nafsi zetu. Sasa tunaweza kufurahia mwenendo mpya maishani!

Kwa vile hali yake ya zamani imekufa, mkristo halisi amekuwa kiumbe kipywa cha Mungu. Wokovu wetu unahu su mabadiliko kama haya.

Katika Kristo nilikufa, na katika yeye niliamka tena,

Katika Kristo niliwashinda maadui zangu,

Katika Kristo, mbinguni nilitwaa kitu changu,

Nayo mbinguni wakafurahia kwa ajili ya ushindi huu.

Tunapochunguza na kuelewa hali yetu sisi wakristo kama watu ambao wamesulubiwa na Kristo. Maisha yetu hapa duniani yatabadilika kutoka kuwa ya yale ya mtu ambaye anajijali mwenyewe kuwa yale ya mtu ambaye anamjali Kristo maishani.

## KUZA IMANI YAKO

Ili kufurahia maisha ya kuwa na ushirika wakaribu sana na Mungu, lazima tujifunze na tujue jinsi ya kukabili hali ile ya kujijali kuliko kumjali Mungu; na hii ndio shida yetu hapa duniani.

## SHIDA YANGU HAPA DUNIANI

**Kuna haja kujiuliza swali hili: “Je, maisha yangu ya hapa duniani ni yako kujitegemea mwe nyewe au kumtegemea Mungu katika kila hali?”**

Bila shaka maisha ya kujitegemea na kujijali hufanya mtu kukasirishwa au jambo lolote ambalo linatisha majivuno, starehe ama hata raha yake. Mwandishi G. Campbell Morgan alisema hivi: “Kupenda nafsi yako ndiyo msingi wa dhambi, chanzo cha uadui na hii ni sehemu kuu ya jehenamu.” (*Hosea: Moyo na Utukufu wa Mungu.*)

Jioni moja, katika mkuutano wa maombi, nilimsikia mama mmoja akiomba na moyo wa unyenyekevu na upole kabisa. Ni wazi kwamba alikuwa yuko katika hali ya kukutana na Mungu. Katika maombi hayo, alikuwa akisema: “Kristo, iweke mikono yako ya upendo inizingire, nifunge msalabani, na unipende hadi kufa. Sitaki tena kuwa eti ni mimi aishiye, bali awe ni wewe Mungu anayeishi ndani yangu.”

Maombi ya mama huyu yalinifurahisha sana. Ingawa yeche alifahamu vyema kwamba alikuwa ameokolewa kuitia kifo cha mwokozi wetu Yesu Kristo, na kufufuka kwake ili awe mmoja wa wale wanaoishi mbinguni, bado yeche alifahamu kwamba

## *Kujianada na Maombi*

mwili wa ke ulikuwa ungali uko hapa duniani. Ni wazi kwamba kuperia ombi lake hili, mama huyu alitaka Mungu amsaidie katika uovu wake akiwa katika duniani hii. Kwa kweli maombi kama haya ya huyu mama yalionyesha wazi hamu kuu aliyokuwa nayo ya kuwa na ushirika wa karibu sana na Mungu wake. Nilipokuwa na wazaa abaadaye kuhusu ombi hili, niligundua kwamba hata Mtume Paulo aliwaahi kupeana msingi wa kiBiblia katika ombi kama hili la kutoka ndani kabisa aliposema: *kwa maana kama mkiishi kwa kufuata mambo ya mwili, mwataka kufa; bali kama mkiyafisha matendo ya mwili kwa Roho, mtaishi* (*Rum. 8:13*).

Kati ya wale wanaosoma kitabu hiki huenda wakakuta baadhi ya mawazo yaliyoko mbele yetu hivi sasa kuhusu kifungu hiki cha Maandiko Matakatifu kuwa ya msaada na ambayo ya naweza kutimizwa. Wale ambao wanaelewa lugha ya kiGiriki wanatusaidia kuelewa vyema ukweli unaoweka mtu huru ambao unapatikana katika kifungu hiki cha Maandiko Matakatifu:

*Kwa maana kama mkiishi kwa kufuata mambo ya mwili, mtakufa, bali mkiyafisha matendo ya mwili kwa Roho, mtaishi* (*Rum. 8:13*).

Kwanza: Katika lugha ya kiGiriki, neno “**wewe**” ndio jambo kuu linalohusu **kuuawa** na limeandikwa kwa njia ya kitu ambacho kinatendeka.

Ukweli wa Biblia: Nikitaka kukombolewa kutoka uovu wa mwili wangu, lazima nijitoe kushirikiana na Mungu.



## KUZA IMANI YAKO

Pili: Msitari huu wa **Maandiko Matakatifu unatueleza** wazi kwamba ni kupitia Roho Mtakatifu mwenyewe anayetuwezesha kushinda uovu wetu wa kujipenda, na kutenda mengi yaliyoya dunia hii.

Ukweli wa Biblia: Ingawa nahitajika kuyaa cha maombi yahusike katika shughuli ile ya kupigana vita na dhambi ilioko katika nafsi yangu nikiwa hapa duniani, **ni Roho Mtakatifu ambaye anaweza kunitenga kabisa kutoka kwa maovu yanayonihu mimi.**

Tatu: Ni jambo la kustaajabisha kuona kwamba msitari huu umeandikwa kwa njia inayoonyesha kwamba haya yote **yanayozungumziwa yanatokea wakati huu**. Hii ina maana kwamba yale ambayo yanayotajwa hapa ni mambo ambayo yana stahili kuwa yakiendelea kutendeka.

Ukweli wa Biblia: Ingawa ni jambo ambalo laweza kuleta mabadiliko makubwa katika maisha ya Mkristo, pale mtu anapomuuliza Roho Mtakatifu kupenda uhai wake hadi kifo, hili si jambo ambalo linastahili kufanywa mara moja tu. Kamwe sivyo! Pale unapohisi kwamba moyo ule wa kibinagsi unajitokeza, kuna haja Mkristo kuomba mara moja akimtaka Roho Mtakatifu afanye ile kazi ya kumsaidia na kumuondoa katika mtego huu. Na pale tunapoendelea kutegemea nguvu za Roho Mtakatifu, matendo yetu ya ubinagsi na uchoyo yatauliwa. Mungu anataka kwamba moyo huu, na imani utaendelea na kuwa kitu ambacho kiko ndani yetu daima.

## *Kujianada na Maombi*

Kusudi la Mungu ni kwamba kwetu sisi, tunafaa kuwa na roho ile ya imani ambayo yaendelea kukuwa, na iko nas kila wakati.

Kwa mfano, hebu waza kuhusu mahakama. Hapa kuna mtu ambaye ameshtakiwa kwa kosa la kuua. Ushahidi umechunguzwa, na imebainika wazi kwamba mshtakiwa ana hatia mbele ya koti. Na sasa jaji ana jukumu kubwa la kutoa hukumu. Kila mtu yuko kimya katika chumba hiki, naye hakimu ananyanya kutoka kiti chake na kusema: "Mtu huyu amepatikana na hatia ya kuua, na hukumu yake ni kifo!"

Kupitia matamshi hayo, kazi yake hakimu imeisha. Na ikiwa hakimu atajaribu kutimiza hukumu ile mwenyewe tuseme achukue bastola kutoka pale ameketi na kumuua mtuhumiwa na risasi pale, basi hakimu huyu atakuwa ametenda kosa kubwa la uuaji!

Baada ya kupitisha hukumu ya kifo, kazi yake hakimu yule ni kumuelekeza muuaji katika mikono ya wale ambao kazi yao ni kutimiza hukumu yake.

Sawa na haya, maisha yetu ya ubinafsi hayana kile yanaweza kufanya ila tu kukiri kwamba sisi tuna roho mbaya ya ubinafsi ndani yetu. Sawa na hakimu yule kortini, lile ambalo tunaweza kufanya ni kupitisha hukumu, hata hukumu ya kifo kwa yale yote ambayo ni ya kujipenda, na kutowajali wenzetu. Sawa na vile hakimu yule hawezি kutimiza hukumu ile yeye mwenyewe, sisi pia hatuwezi tukatimiza hukumu ile inayohusu hali yetu ya kujipenda. Hata hivyo, ni jambo la kumshukuru Mungu ametupa yule ambaye

## KUZA IMANI YAKO

anaweza kutimiza hukumu yenyewe, naye ni Roho Mtakatifu. Ni yeze Roho Mtakatifu ambaye ana uwezo wa kuharibu na kuondoa hatari inayotokana na ubinaksi wetu sisi wanadamu.

Kweli kwa ajili ya utukufu wake Mungu, na Roho Mtakatifu, tumewezeshwa kuua matendo mabaya ya miili yetu. Pale tunapotambua na kuchukua msaada huu mkubwa tuliopewa, tutaanza kufurahia sana uhuru unaotokana na maisha ambayo yanamuweka Mungu katika sehemu ya muhimu.

Kwa ajili ya mafunzo ya Maandiko Matakatifu kama haya, na mafunzo yanayotokana na maombi kama ya mama yule katika mkuutano ambao nimeutaja hapo mbeleni, mimi pia nimeweza kuwa nikiomba kama mama huyo:

**Mungu, kupitia Roho wako Mtakatifu, nifanye nizingire msalaba ulikosulubiwa, na yapende maisha yangu kufikia kifo. Nataka nisiwe ni mimi tu aliye hai: bali awe ni wewe Kristo aishiye ndani yangu.**

Ni jambo rahisi kuamini kwamba kile ambacho tunataka kutimiza wakati wa kulishwa na kuendelezwa katika neno la Bwana ni kwamba tuwe na raha maishani. Wazo hilo sio sahihi. Ni kwa nini makuhani wa agano la Kale waliendeleza na kukuza kusanyiko la wale walio wake. Je, wao walifanya haya ili wawe na kundi kubwa la kuwaonyesha watu? La sivyo! Jinsi vile William Still anadokeza, kundi hili la makuhani lilihitajika kwa ajili ya kuchinjwa! Tangu

## *Kujianada na Maombi*

walipozaliwa, ilikusudiwa kwamba watachinjwa na kuwa dhabihu.

Mara nydingi, wakristo huamini kwamba uwezo wao wa kuimba ama kuhubiri utamfurahisha Mungu pale wanapo jitahidi kuwa hodari na washindi wa medali katika mambo haya mbele ya wenye imani! Pale Mungu anapotuwezesha kukua katika imani kupidia neno lake, lengo lake sio kwamba tuweze kuwa washindi mbele ya umati, ila maisha yetu yawekwe mbele ya madhabahu kama dhabihu. Kabla hatujaku wa walio hai kabisa katika mambo yake, lazima sisi wenyewe tuwe hatuko hai katika mambo yetu wenyewe. Ubinafsi wa kila aina lazima uwe haumo ndani yetu tena. Ubinafsi kama ule wa kujionea huruma, kujipenda, kujiweka kuwa nambari moja katika kila jambo, kujifurahisha, na kujiondolea makosa: haya yote ni mambo ambayo yamejitokeza sana. Kwa kweli utaratibu wa yale ambayo ni ya ubinafsi ni makubwa sana.\*

Huku akiwa na uchungu mwingi roho ni, mtume Paulo alikiri kwamba, kando na Timotheo, haku weza kumuona ye yote ambaye anajali sana kanisa pale

---

\* Katika Maandiko Matakatifu, kifo sio mwisho wa yote; ila kifo ni hali ile ya kuwa na utengano kati ya wale ambao wameachwa na yule ambaye ameondoka. Kwa mfano, kufa kimwili ni hali ile ya kutengana kwa roho na mwili. Nacho kifo cha milele ni utengano wa milele wa Roho kutoka kwa Mungu. Sawa na haya, kufa kutoka nafsi yako ni utengano wako na nafsi yako ya matendo ya kujipenda na mienendo ya kiutu. Na jinsi vile tayari tumeona, hali hii inaweza kutokea tu pale Roho Mtakatifu wa Mungu anapoingilia jambo hili na kulifanya litokee.

## KUZA IMANI YAKO

Kolosai, kwa sababu waKristo wengi katika mji huu hawakuwa na upendo ule ambao haushughulikii kila mmoja nafsi yake. Tunasoma jinsi vile mtume Paulo alivyoohuzunika: *maana wote wanatafuta vyao wenyewe, sivyovya Kristo Yesu (Flp. 2:21)*.

Wako wapi wakristo ambao **wanajali** kanisa linalosumbuka katika sehemu nyingi hapa duniani. Je, tunashugulikia tu yale yanayotuhusu kiasi kwamba hatu jali yale yanayohusu wale ambao hawana wale wa kuwajali? Na lazima tukumbuke ni upendo wa Mungu ambao unatuwezesha kupenda wenzetu hata zaidi ya nafsi yetu ambayo huvumilia uchungu mkubwa. Na sawa na jinsi vile kikombe ambacho kimejaa siki lazima kitolewe siki ile kabla kile ambacho ni kitamu kama maji ya mchungwa kuwekwa ndani yake, maisha ya ubinafsi lazima yauawe kabla upendo wa Mungu kutiwa ndani yetu. La kushukuru Mungu ni kwamba haya yote; yaani kuondolewa roho yule wa ubinafsi na kujazwa roho wa upendo ni mambo yanayofanywa na kuendelezwa na roho mtakatifu katika maisha yetu. Hatuwezi kuyafanya wenyewe. Ni jambo la muhimu tuzidi kumuomba Mungu ayaue matendo yote ya ubinafsi na badala yake atujaze na upendo wa Mungu unaozidi kipimo: na tumaini halitahayarishi; *kwa maana pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika miyo yetu na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi (Rum. 5:5)*.

Na pale ukweli wa aina hii unapoanza kujitokeza na kuwa wazi katika moyo wako wakati wa *kuwa pamoja na Mungu*, Roho Mtakatifu atakufichulia ukweli zaidi kutoka neno la Mungu.

## *Kujianada na Maombi*

Ni jambo ambalo limewahi kusemwa kwamba kila mwenye imani lazima aweke utaratibu wa yale yanayomhusu na Mungu. Lazima tuhakikishe kwa mba hakuna jambo lolote ambalo litawenza kuzima uhusiano na ushirika tulio nao na Mungu.

## **Ichunguze Roho Yako**

1. Nikiwa mbele yake Mungu, je ninajua dhambi zangu ambazo sijakiri mbele ye Mungu?
2. Je, nina shida ya aina hii: Roho wa kutokuwa tayari kusamehe wale wanaonikosea?  
Kuwapenda wale ambao siwapendi? Kuwadanganya wenzangu ili nionekane kuwa mwema?  
Kuonea kijicho kile cha mwenzangu ambacho ni kama zawadi au mali yake?  
Mtu aliye mwenye manung' uniko na kukosoa?
3. Naweza kuwa na roho inayotabasamu na kungoja yaliyo mazuri kwa ajili dhamiri yangu imesafishwa?
4. Je, maisha yangu hapa duniani yanmezengirwa na Kristo, ama yamezingirwa na yale ambayo yananihusu.

*(Sasa labda litakuwa jambo bora kurudi kwa ombi lake William Maclardie Bunting katika ukurasa wa... na kuomba tena ukiwaza kuhusu yote yanayotajwa katika ombi hili.)*





*Tunapotembea na Mungu  
Katika Mwanga wa Neno lake,  
Utukufu wa kiwango gani anaouelekeza kwetu!  
Pale tunapofofanya yale yaliyo ya muhimu kwake,  
Yeye anakuwa karibu nasi  
nao wote ambao wanamuamini na kumuitikia*

*Hakuna giza linaloweza kujitokeza,  
Hakuna wingu katika anga,  
Na kicheko chake huondolea mbali  
Hakuna tashwishi wala cha kuogopa,  
Hakuna kilio wala chozi  
Laweza kuwako pale tunapoamini na kumuitikia.*

*Lakini hatuwezi kuonyesha wazi  
Furaha ya mapenzi yake  
Mpaka pale katika madhabihu tunalala;  
Kwa ajili ya wema anatutendea  
Na furaha anayotuletea  
Ni yao wale wanaoamini na kumuitikia.*

*Na katika ushirika mtamu  
Tutakaa miguuni mwake,  
Ama tutatembea katika upande wake kwenye njia hiyo;  
kile asemacho ndicho tutafanya,  
Pale anatutuma ndiko tutaenda-  
Usiogope, ila amini na kuitikia.*

—John H. Sammis

## *Wakati wa Kuwa Pamoja na Mungu*

**U**kiwaza juu yake, hakuna jambo ambalo ni la majivuno sawa na lile la kujiona kwamba unawenza kukumbana na matukio yanayojitokeza maishani kwa nafsi yako pasipo uwezo wa Mungu, Maandiko Matakatifu, na moyo uliyo tayari kupokea yale ambayo yanayomhusu Mungu.

Mfalme Daudi alijua ni mbegu gani ambayo ingeweza kuzaa roho mwema maishani. Yeye alisema yeoyote ambaye angetumia wakati wake kuwaza kuhusu neno la Mungu ndiye ataweza kuzaa tunda lililobora... *Naye atakuwa kama mti uliopandwa, kandokando ya vijito vya maji, uzaao matunda yake kwa majira yake, wala jani lake halinyauki; na kila alitendalo litafanikiwa* (Zab. 1:3).

**Je, huyu ni mtu wa aina gani? Yeye ni yule ambaye sheria ya Bwana ndiyo impendezayo, na sheria yake huitafakari mchana na usiku** (Zab. 1:2).

## KUZA IMANI YAKO

Kuna wakati ambapo mimi huwaambia wale ambao wamempokea Kristo maishani mara ya kwanza kwamba “Kurasa moja ya Neno la Bwana kila siku inaweza kumuweka shetani mbali.” Soma sehemu ya Maandiko Matakatifu, na baadaye urudi kusoma sehemu hiyo tena. Pale unapofanya hivyo, utaweza kuwaza kuhusu yale **unayosoma** msitari baada ya msitari. Je, umewahi kuona ng’ombe akitafuna cheuo? Katika kutafuna cheuo, nyasi huliwa ikamezwa, na baadaye ikarudishwa mdomoni kutafunwa tena mpaka pale sehemu zote za manufaa zimetolewa. Kwa kweli, huu ni mfano mzuri sana unaonyesha jinsi vile kuwaza kwa undani kuhusu maandiko matakatifu huweza kuwa wa msaada mkuu kwa Mkristo.

Niliwahi kumjua mtu mmoja ambaye aliamua kupokea wo kovu akiwa na umri wa miaka 70. Wakati ule, yeye aliyajua machache sana kuhusu Biblia. Kabla ya kupokea wokovu, yeye hakuwa akienda kanisani. Pia hakuwa na masomo ya juu. Lakini pale alipozaliwa mara ya pili, alikuwa na hamu sana ya kumjua Mungu na kukua katika imani yake hivi kwamba pale alipoaga dunia akiwa na umri wa miaka 83, tayari alikuwa amesoma Biblia kutoka mwanzo hadi mwisho mara 13. Haijalishi umri wako wala masomo ambayo umepitia, kilicho wazi ni kwamba wewe pia unaweza kusoma Biblia kila siku.

Biblia iliyofunguliwa, moyo ulio safi, na roho yaunyenyekevu na kupiga magoti; pamoja na ombi lake Daudi, *Unifumbue macho yangu niyatazame maajabu*



## *Wakati wa Kuwa Pamoja na Mungu*

*yatokayo katika sheria yako (Zab. 119:18), haya yote yatakutengenezea barabara ili uwe na wakati mzuri wa kuwa pamoja na Mungu.*

Sawa na jinsi vile tayari tumegusia, watu wengi hawajagundua kwamba wakati wa *kuwa pamoja na Mungu* ni wakati wa mazungumzo ya njia mbili - wewe na Mungu. Mungu anasema nasi pale tunaposoma na kuwaza juu ya neno lake takatifu. La kusikitisha ni kwamba wengi wetu hatujaelewa kwamba baada ya Mungu kukubali kuzungumza nasi kuititia roho zetu, ye ye anangoja tumjibu kuititia maombi. Tunapoyangalia Maandiko Matakatifu na **kuwaza** juu yake, Maandiko Matakatifu haya yanabadilika kuwa **sehemu ya mawa zo yetu**. Na pale tunapochukua hatua ya kuweka mambo haya kuhusu yale ambayo ni Maandiko Matakatifu katika maombi, basi haya yote yanakuwa **sehemu ya uhai wetu**.

Mimi mwe nyewe nimeona kuwa ni jambo bora kuwaza juu kila msitari katika maandiko matakatifu nikiwa na maswali fulani katika mawazo yangu pale ninapokuwa nikisoma Biblia. Baadhi ya maswali haya huwa yale ambayo niliwahi kuijuliza zamani. Mimi huacha maswali haya yaniongoze pale ninapokuwa niko katika ushirika na Mungu. Hebu nichukue nafasi hii hapa kukushauri kwamba hata wewe waza kuhusu neno la Bwana kwa njia hii unaposoma maandiko matakatifu. Yakumbuke maswali ambayo umekuwa ukiwaza juu yake pale unaposoma Maandiko Matakatifu na wakati wa kusoma Maandiko haya, tafuta majibu ya maswali haya unposoma kila msitari wa Biblia.

## KUZA IMANI YAKO

Na kwa vile nimetumia maswali haya kwa muda mrefu, maswali yenyewe sasa yamekuwa ni kama sehemu ya utu wangu pale ninapokuwa namkaribia Mungu na maandiko matakatifu. Utakuja kugundua kwamba baadhi ya maswali haya yanahitaji uwe mtiifu, mengine yatahitaji majibu yanayohusu imani, nayo mengine yatakuonyesha wazi baadhi ya hatari na maonyo ambayo yanatokana na maombi na sifa mbele ya Mungu na hata kukusaidia kuweza kujua hila na njama zake adui wako shetani, na pia kukuwezesha kuelewa jinsi vile ushindi wake Kristo waweza kuwa ushindi wako pia.

### ***Kuitikia Kwa Utiifu***

Sawa na jinsi vile tunahitaji kuwa na Mungu kila wakati, hatustahili kuwa na mengi ambayo katika mawazo yetu hatungependa ayajue. Hali ya kutokuwa na yale ambayo tunamficha Mungu wetu itatuwezesha kumsikiliza kwa urahisi wakati wa kuwa pamoja na ye ye. Tunastahili kuyafanya yale yote yanayohusu nia yetu kwa utiifu kwa Neno lake Mungu kila mara tunaposikia sauti ya Roho Mtakatifu ikienea nasi.

Pale unapokuwa ukisoma maandiko matakatifu wakati wa kuwa pamoja na Mungu, ni bora kuijuliza maswali haya: Je, katika msitari huu amba o nasoma kuna yafuatayo:—

Amri ya kutaka niwe mtiifu?  
Dhambi ya kuepuka?  
Mfano mwema wa kufuata?  
Mfano wa lile la kuepuka?

## *Wakati wa Kuwa Pamoja na Mungu*

Je, unaona jinsi vile maswali kama haya yanavyoweza kukuelekeza kuwa na uhusiano wa karibu na Mungu wako? Bila shaka maswali haya hayatakuacha tu ukiwaza kuhusu ukweli ambao umesoma. Unapojobu maswali haya mbele ya Mungu, basi utakuta kwamba kuna haja ya kuitikia katika moyo wako yale ambayo Mungu amesema.

Kila wakati kumbuka Roho Mtakatifu yuko nawe kila mara unaposoma Neno la Bwana, na ukimtegemea, yeye atasukuma Neno lake umbali wa nchi tisa kutoka katika kichwa chako hadi katika moyo wako.

Tunaishi siku mbaya ambapo dunia inaelekea kwa kasi katika hali ya uasi na kutotii neno la Bwana na amri zake. Ili tuweze kuwa na usemi mkubwa katika jamii enzi hii ambapo wengi wanapuuza Mungu, lazima tuwe watifiu, na tufanye yote tunayostahili kufanya na moyo wetu wote. Ni pale tu tutakapoanza **kutii** ukweli ambao Mungu anatuonyesha ndipo tutakapoanza kujifungua ili nguvu zake zitoke kwake kupitia kwetu na kuingia katika dunia hii inayomhitaji.

Juzi, mimi na mke wangu tulisoma pamoja sehemu ya kitabu cha Oswald Chambers kiitwa cho *My Utmost for His Highest*. Haya ndio aligusia katika sehemu tuliyosoma:

Mtii Bwana katika kile ambacho anakuonyesha, na papo hapo kile ambacho kinafuata kitafunguliwa ... Nataraji siku moja nitaelewa haya yote!" unasema, lakini hebu ngoja dakika moja tuu!

Waweza ukaelewa haya yote wakati huu. **Sio**

## KUZA IMANI YAKO

**masomo** ndio huleta hali hii ya kuelewa kwa undani; ni **utiifu** ndio utakuwe zesha kuelewa kwa undani mambo haya. Hata sehemu ndogo kabisa ya utiifu itakufungulia madirisha ya mbinguni ili ukweli wa ajabu wa Mungu uwe pale na uweze kuuona. Lakini Mungu hatafichua ukweli wa ndani zaidi kumhusu yeye Mwenyewe mpaka pale utakapotii yale ambayo unayaelewa.

Imewahi kuripotiwa kwamba usiku moja, wamishonari wawili wa hapo mwanzo Charles T. Studd na Hudson Taylor walikuwa pamoja katika chumba kidogo, orofa ya juu kabisa. Siku moja, asubuhi na mapema, Taylor aliamka akamkuta mwenzake anasoma Biblia yake ambayo ilikuwa inaangazwa na mwanga wa mshumaa hafifu, na hapo akataka kujua amekuwa hapo kwa muda gani. Studd naye akamjibu na kusema:

“Usiku wa manane niliamka maneno yake Bwana Yesu yakiwa katika kinywa changu *mkinipenda, mtazishika amri zangu* (Yn. 14:15). Nilijiuliza kama kweli nilikuwa nimethibitisha kwa Mungu wangu kwamba nampenda Kristo na utiifu wote unaostahili. Niliichukua Biblia yangu na kwa muda uliobaki usiku ule, nikatumia muda huo kusoma Injili takatifu. Na katika Maandiko haya, nikatafuta kila amri ambayo Kristo aliwapa wafuasi wake. Kila mahali ambapo ni wazi kwamba nimekuwa mtiifu kwa kila amri yake Bwana wetu, mimi nimeweka hapo alama na kusema “Halleluya!” Na pale ambapo nimekosa kutii, nimetubu dhambi zangu, na kupitia nguvu



## *Wakati wa Kuwa Pamoja na Mungu*

zake, nimejitoa kuwa mtiifu, na hivyo kuonyesha wazi kwamba kwa kweli nampenda.”

Msomaji mpPENDWA, pale unapotembea na Bwana katika mwanga wa neno lake, wewe pia utaungana na yule aliyeandika wimbo wa maombi usemao, hakuna njia pasipo “kuamini na *kutii!*”

### ***Kujitwalia Imani***

Biblia ni chombo ambacho kinatumiwa na Mungu kujenga imani. Tunapokuza imani ili imtegemee Mungu, na kumtii Kristo, basi sisi tuaweza tukasema wenyewe hatuwezi, lakini yeye atuwezeshaye kufanya yote.

Unaposoma maandiko matakatifu wakati wa kuwa pamoja na Mungu, ni vizuri pia kuijiliza: Katika msitari huu ninaosoma, je?

kuna ahadi

Kuna onyo

Biblia ina ahadi chungu nzima. Pale tunap owaza kuhusu neno la Bwana, ni jambo zuri kudai ahadi za Bwana. Wakati huo huo, ni jambo la muhimu kufuata maonyo yote ya kuhuzunisha anayoyatoa. Kukubali ahadi za Mungu, hukutuki wa hatujali maonyo yake Mungu sio “kuishi na imani” ila ni “kufabila kuamini!”

Pale unaposoma Biblia kila siku, chunguza na kutambua kila ahadi ambayo Mungu anakupa, na hapo dai ahadi hiyo kuwa haki yako hapo hapo. Pale unapojichukulia ahadi yako kutoka kwa Mungu,

## KUZA IMANI YAKO

nguvu za kukuwe zesha kutoka kwake Yesu kristo ndizo utakazohitaji kufanya kila kila hatua mpya ya utiifu unayochukua kuwa ukweli wa yale ambayo unayapitia mwenyewe.

Umepewa ahadi zake ili uweze kuishi katika ukweli wakati wa kutembea na Mungu. Pale unaposhikilia ahadi zake, imani yako itazidi kuongezwa nguvu, jinsi vile tunaambiwa *Basi imani chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo* (Rum. 10:17).

Je, umewahi kujiuliza ni nini kinyume cha imani? Jibu lake sio rahisi jinsi vile unafikiria. Kusema kwamba kutokuwa na imani ndio kinyume cha kuwa na imani ni kukwepa maana ya jibu halisi la swalii hili. Hebu waza kuhusu maneno ambayo yanahusiana kama kaka, tutayaita “kaka watatu wanatoa uhai.” Wa kwanza ni “imani,” wa pili ni “kutegemea,” na watatu ni “unyenyekevu.” “Sasa hebu waza kuhusu kakaa watatu hatarinao ni “kukosa imani,” “kuwa huru” na “kiburi.”

**Mtu aliye na imani** ni mtu ambaye anamtegemea Yesu Kristo kufa nya yale ambayo ye ye mwenyewe hawezi kuyafanya. Pale anaposoma Biblia, mtu mwenye imani huona na baadaye atajichukulia ahadi za Mungu ambazo haziwezi kuvunjwa.

Kristo aliwaambia wafuasi wake, *Pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lolote* (Yn. 15:5). Kabla mtu hajaamini kwamba Mungu anaweza kutenda lolote la kiroho kupitia kwake, lazima aamini kwamba ye ye kwa njia yake hawezi kutimiza lolote ambalo



## *Wakati wa Kuwa Pamoja na Mungu*

litahesabiwa katika maisha ya milele kwa nafsi yake mwenyewe. Hali hii ya kutegemea huzaliwa katika moyo wa unyenyekevu. Mtu kama huyu atawenza kusema sawa na jinsi Mtume Paulo anavyosema katika Wafilipi 4:13, “*Nayaweza yote kupitia Kristio anitiaye nguvu.*” (*Filipi 4:13*)

**Mtu ambaye hana imani** ni yule ambaye anajitegemea na haoni haja ya kutafuta usaidizi kutoka kwa Mungu katika lolote analokumbana nalo. La kusikitisha ni kwamba kuna mamilioni ya watu leo hii ambao hawategemei Kristo wanapotafuta wokovu. La kusikitisha pia ni kwamba wakristo wengi hawategemei Roho Mtakatifu ambaye yuko ndani wanapojitahidi kuishi maisha ya kiKristo. Kila aina ya maisha ya kuwa huru huzaliwa katika moyo wa kiburi, moyo usiyokubali kubadilika.

Kwa hivyo, tunaweza kusema kwamba kinyume cha imani ni kiburi; nakinyume cha cha kukosa imani ni unyenyekevu. Kinyume na imani ya kawaida, hali ile ya kujiona kwamba unajiweza katika mambo mbali mbali; hali hii ni kama dawa inayozuia moyo wako usipokee kiasi kinachofaa cha imani.

Kila tukio hapa duniani ambalo hufanya mtu ajione kuwa yeche ni bora sana kuliko wenzake, humfanya mtu asiweze kuhisi na kuona nguvu za ajabu zake Kristo ambaye alifufuka. Uwezo wa Mungu ambao hauna kifani uko nyuma ya kila ahadi ambayo amepeana, na yeche hajatuacha tutumie mbinu zetu wala kwenda njia zetu wenyewe katika safari yetu hii maishani.



## KUZA IMANI YAKO

G. K. Chesterton (1874-1936) aliwahi kutaja haya kuhusu kiburi kinachotokana na hali ya kujiona kuwa mtu anayejiweza:

Kile ambacho kinatusumbua wakati huu ni hali ya kujiona kuwa watulivu mahali ambapo hapafai. Utulivu umejiweka kwenye sehemu ya thibitisho ambapo haikuhitajika kuwa. Mwanadamu aliumbwu kustahili kuwa kiumbe ambacho hakijiamini, lakini sio kiumbe ambacho hakina uhakika kuhusu ukweli; haya yote yamefanywa kwenda kinyume.

Mkristo yejote ambaye atazidi kutegemea ushauri wa wanadamu, ama atakayeweka imani yake katika nafsi yake mwenyewe, na sio kwake Mungu - huyu kamwe hataingia katika ukamilifu ambaao ni baraka zake Mungu. Sawa na jinsi vile maji huteremka kwa haraka kuelekea katika sehemu iliyo chini kabisa, Roho Mtakatifu ambaye Kristo alimwita “*maji ya uhai*” *hatateremka na kuelekea kwake yule ambaye roho wake yuko juu kwa ajili ya kiburi* (*Hab. 2:4-5*). Hata hivyo, Roho Mtakatifu atajaa na kufurika kwa wingi kutoka kwa moyo wa yule aliye na imani ambaye kwa unyenyekevu atatambua kwamba anahitaji nguvu na uweza wake Kristo.

*Hata siku ya mwisho, siku ile kubwa ya sikukuu,  
Yesu akasimama akapaaza sauti yake akisema, Mtu  
akiona kiu, na aje kwangu anywe. Aniaminie mimi  
kama vile maandiko yalivyonena, mito ya **maji**  
**yaliyo hai** itatoka ndani yake (Yn. 7:37:38).*

## *Wakati wa Kuwa Pamoja na Mungu*

Kila siku unaweza kuanguka miguuni mwake Kristo na kunywa maji haya yenyeye uhai. Unapofanya hivyo, maisha yako hayataweza kuelezwaa kuhsusiana na uwezo wako, talanta na hata masomo; badala yake maisha yako yatajitokeza kuonekana kutoka ndani yako kwa Roho wake Mtakatifu.

Kumbuka kwamba kupitia utu wake Roho Mtakatifu, Bwana wetu aliyefufuka amejishusha kuvalaa vazi ambalo ni sawa na miili yetu sisi ambaa tumezaliwa mara ya pili, na tu watoto wa Mungu. Kwa hakika, leo hii, mwenye imani ndiye ngome kamili ya Mungu katika dunia hii ambayo haina Mungu. Kupitia kila Mkristo aliyepokea wokovu, Roho Mtakatifu anazidi kuendeleza kazi yake ya kuokoa watu.

*Katika Maandiko Matakatifu tunasoma hivi: Tena panamapatano gani kati ya hekalu la Mungu na sanamu? Kwa maana sisi tu hekalu la Mungu lai ye hai; kama Mungu alivyosema, ya kwamba, Nitakaa ndani yao, na kati yao nitatembea, nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu (2 Kor. 6:16).*

Sisi ni hekalu ya Bwana, na kupitia kwetu, yeye amenuia kuonyesha utukufu wake.

Katika kutambua jambo hili, Mtume Paulo anasema hivi basi, *wapenzi wangu, kwa kuwa mna ahadi hiso, na tujitakaze nafsi zetu na uchafu wote wa mwili na roho, huku tukitimiza utakatifu katika kumcha Mungu* (2 Kor. 7:1)

## KUZA IMANI YAKO

### ***Ukweli Wa Sala***

Chombo kittwacho “tuning fork” hutumiwa kurekebisha sauti kutoka kwa Piano. Chombo hiki hutumiwa kama kipimo cha kupima ubora wa sauti ya muziki kutoka piano.

*Nayo Biblia ni chombo ambacho Mungu anatumia kuboresha mio yetu sisi wanadamu ili iwe ya kupendeza sawa na sauti tamu kutoka piano hat juu mbinguni.*

*Na pale neno la Bwana linapoleta uwezo wa kuelewa upya utukufu na upendo wa Mungu, basi wewe utakuwa kiumbe kipyta katika jinsi vile unamshukuru na kumuabudu Mungu. Na hii ni kupitia kunena kwa undani kwa nyimbo na Zaburi (Efe. 5:19)*

Ili kutusaidia kumsifu Bwana wakati wetu kuwa pamoja na Mungu, ni bora kutilia maanani maswali haya: Katika msitari ninaousoma huu, je:

kuna wazo jipyta linalohusu Mungu Baba?  
kuna wazo jipyta linalohusu Mungu Mwana?  
kuna wazo jipyta linalohusu Mungu Roho  
Mtakatifu?

Ni jambo la kutia moyo kwamba siku hizi kuna muamko na hamu kati ya wale walio na imani wa kutaka kuabudu Mungu kwa kweli kabisa. Bwana wetu Yesu Kristo alitilia mkazo ibada ya namna hii aliposema hivi: *Mungu ni Roho, nao wamwabuduo yeye imewapasa kumwabudu katika roho na kweli.* (Yn. 4:24). Kile kinatajwa hapa ni kwamba ibada ya kweli lazima iwe ile ilio katika misingi ya Roho Mtakatifu



## *Wakati wa Kuwa Pamoja na Mungu*

na iwe na ukweli wa neno la Bwana. Ni ibada ya namna hii pekee itakayomletea Baba wetu aliye juu mbinguni furaha.

Pale Roho Mtakatifu anafichua wazi maajabu ya Mungu - na hasa mapenzi yake, nguvu zake, utukufu wake, utakatifu wake, uzuri wake na umaridada wake, miyo yetu itavutwa kuanza kuimba wimbo mpya wa ibada na sifa kwake Mungu.

Kupiga magoti ni mtindo wa maombi ambayo yanaweza kukuweka katika hali ya kuwaza yale yanayofaa wakati wa kuja mbele ya Mungu. Hata hivyo sina shaka unaelewa jinsi vile mimi pia naelewa kwamba tendo lile la kupiga magoti wakati fulani huwa si hali ambayo inakuwezesha kuonyesha upendo na kujitoa kwako kwa Mungu.

Ni jambo la ajabu kwamba hata Mtume Yohana alipokuja mbele ya Kristo aliyetukuka katika kisiwa cha Patmo, yeeye alishuhudia kwamba hakupiga tu magoti, *ila alianguka miguuni pake kama mtu akiyekufa. Akaweka mkono wake wa kuume juu yangu, akisema, Usiogope, Mimi ni wa kwanza na wa mwisho (Ufu 1:17).*

Hata hivyo ni jambo linalostahilli kutiliwa maanani kwamba kila mara kitu cha muhimu kinapojitokeza karibu na Mkristo, kuna kile ambacho ni cha uongo ambacho nacho hujitokeza kuwa hapo karibu. Kristo mwenyewe alituonya kuhusu mambo fulani ambayo yanaweza kuonekana na macho kuwa ni kama ibada, huku yakiwa mambo yaliyo mbali kabisa na ibda au maombi yakweli. Kuna wakati alimitia moyo mwanamke Msamaria awe akiomba

## KUZA IMANI YAKO

kwa "roho na ukweli," na akasema hivi: *Ninyi mnaabudu msichokijua; sisi tunaabudu tukijuacho; kwa kuwa wokovu watoka kwa Wayahudi* (Yn. 4:22).

Maombi au ibada ni kitu ambacho ni zaidi ya maono, lazima yaelekezwe kwake Kristo. Ikiwa lengo la maombi ni kuwaweka watu katika hali fulani, na sio kuwabadili mienendo, basi hapo maombi au ibada ya kweli haiko tena, na badala yake tuna ibada au maombi ya uongo. Kwa kweli, Mungu anahitaji zaidi ya msisimko wa kiroho ikiwa tunataka kujazwa na sifa za kutoka kwa Mungu. Kwa kweli sisi ni hekalu ya Bwana, na kupitia kwetu, yeye anataka kuonyesha na kudhihirisha utakatifu na utukufu wake kwa wale walio karibu nasi.

**Maombi au ibada ya kweli iko katika mawazo na moyo. Kwa unyenyekevu kulenga kwake Bwana wa mabwana, Mungu aishiye, Bwana wetu Yesu Kristo jinsi vile amefichuliwa katika neno la Bwana. Pale hali hii inapotokea, kutakuwa na kuanguka chini mbele yake kwa ajili ya kujitoea na kusifu.**

### *Silaha Ya Neno*

Ni kweli Mungu anabariki wakati wako wa kuwa pamoja naye. Dhamira yako imesafishwa. Pale unapokubali yale yaliyomkumba Kristo Msalabani kwa ajili yako, wewe umekana uhuru ulio nao juu yako mwenyewe au, umekana ubinafsi wako. Pia umekana hamu ya kutaka kuendeleza nafsi yako, na kujitetetea na kujilinda wewe mwenyewe. Sasa uko katika hali iliyo tofauti katika maombi na kutoa sifa

## *Wakati wa Kuwa Pamoja na Mungu*

kwa Mungu. Je, sasa umefikia kilele cha yale ambayo Mungu anakutakia kama baraka wakati wako wa *kuwa pamoja naye?* Jibu la swali hili ni: La, sivyo!

Yuko adui hapa nje ambaye amekasirika sana nasi. Shetani ameksirika sana kwa vile Mungu amekupa njia ya kuweza kuepuka madahara ya dhambi. Wewe uliyeokoka umeepuka madhara - umesamehewa dhambi zako. Naye shetani tayari ametupwa katika moto wa milele.

Kwa hivyo, katika safari yako ya kwenda mbinguni, shetani anafanya kila a wezalo kukuharibia safari hii; na has a kukuondolea imani yako na kuharibu uhsuhuda wako.

Unaposoma msitari wa Maandiko Matakatifu, jiulize hivi: Je?

Kuna mwanga mpya kuhusu utu wake shetani?

Kuna mwanga mpya kuhusu kuhusu malengo ya uovu yake shetani?

Kuna mwanga mpya kuhusu njia zake za kujifi cha ambazo anatumia kutimiza uovu wake?

Siku moja, nilielezwa habari kuhusu kijana mmoja mdogo ambaye alikuwa amerudi nyumbani kutoka shule ya somo la Jumapili. Usiku uliofuata, mama yake alimwona kijana yule akiwa amepiga magoti kando ya kitanda chake. Naye akamwuliza: ‘Unafanya nini?’ “Mimi namfa nya shetani atetemeke,” kijana yule akajibu kwa haraka.” Tuliimba wimbo katika

## KUZA IMANI YAKO

shule yetu ya jumaplili kwamba Shetani hutetemeka pale anapomwona hata mtakatifu mdogo akiwa amepiga magoti. Kwa hivyo, nimepiga magoti kumfanya shetani atetemeke!"

Kwa kweli tunahitaji kufanya zaidi ya kupiga magoti ili Shetani atetemeke. Shetani hutetemeka tu kwa jina lake Kristo anaponyimwa nafasi ya kujenga makao yake katika roho yako; na pia pale katika jina hilo lenye nguvu lake Kristo unatumia na Roho Mtakatifu kutwaa maisha yenyе thamani kutoka mikono ya muovu shetani.

Wakristo wengi wanaamini kwamba wakimuacha shetani, ye ye atawaacha. Wenye imani kama hii wamepotea njia. Kwa mfano, unapokuja kwake Mungu wakati wa maombi, umewahi kujikuta unakumbana na jambo ambalo lilikuwa la kukushinda na hata ingawa uliwahi kuomba msamaha na kutubu dhambi hiyo, na msamaha wako ukakubaliwa? Shetani hujitahidi kukushtaki kuhusu kosa ambalo ulifanya, ukatubu na kupokea msamaha pale msalabani.

**Kukosa uwezo wa kuamua, woga, kuchanganyikiwa, na kufa moyoni mbinu maalum ambazo shetani anatumia kuingilia uhusiano wako na Mungu.**

Pale Shetani anapokukumbusha yale ya zamani, basi wewe mkumbushe yale yanayokuja, yaani yale yanayomongoja huyu muovu. Ingawa Mungu



## *Wakati wa Kuwa Pamoja na Mungu*

hataki kukumbuka ule uovu ambao umetubu na akakusamehe, shetani naye anataka kukumbusha haya yote ili uanze kujiuliza kama kweli Mungu anakupenda kiasi cha kuweza kukusameheha dhambi hizo. Kushindwa kuamua, woga, kuchanganyikiwa na mambo na kufa moyo: hizi zote ni ishara za kazi yake shetani, jitihada za kutaka kuingia na kuharibu matembezi yako na Mungu. Yeye atafanya kila awezalo kuiba furaha na amani uliyo nayo. Lakini Mungu naye atakuwezesha kutambua ni wapi shetani amejenga makao yake katika roho yako ikiwa utalenga macho yako kwake, na kwa kutumia kila silaha ambayo Mungu amekupa, lazima ufunge mlango ili shetani asiweze kukuwingilia.

Katika vita kati ya wanadamu, kuna mbinu za kujikinga na zile za kupiga adui vita. Hakuna vita ambavyo ushindi waweza kupatikana tu kupitia matumizi ya mbinu za kujihani peke yake. Sawa na vita vya kawaida, katika vita vya kiroho, kuna haja ya kupigana kujilinda na pia kushambulia adui. Vyote vyahitaji silaha zile ambazo ni neno la Bwana. Jambo moja la kutia moyo linalohusu wakati wa *kuwa pamoja na Mungu* ni kwamba unapokumbana na shetani, utaweza kunukulu vifugu vya maandiko matakatifu na hapo utaweza kuomba kiBiblia.

Ni jambo zuri mno kujuu kwamba unapoomba kulingana na Neno la Mungu, unaomba kulingana na nia yake Mungu. Na ni nia yake Mungu kwamba ujue na kuona ushindi wa kumshinda shetani na mbinu zake za kuharibu maisha yako ya kiroho.

## KUZA IMANI YAKO

**Vita Vya Kujilinda Kiroho:** Je, unakumbuka jinsi vile Kristo alijaribiwa na muovu shetani? Katika mawazo yangu, mimi hupendelea kufikiria kwamba Kristo alikuwa amemaliza tu kuwa na wakati wake wa *pamoja na Mungu* kwa kusoma kumbu kumbu la Torati (Deuteronomy) Kwa kweli, sehemu ya maandiko matakatifu aliyo nukulu inapatikana katika kitabu hiki ambacho ni Kumbukumbu la Torati (Deuteronomy) Mara tatu Bwana wetu alinukulu yale ambayo yameandikwa katika Maandiko Matakatifu yaani: *Imeandikwa... Imeandikwa ... Imeandikwa...* (*Mat. 4:4,7,10*). Ni majoribu haya yaliyomjia Kristo amnbayo yanatuwezesha kuelewa yale mwandishi wa zaburi anayoyasema alipoandika “*Nitasujudu nikilikibili hekalu lako takatifu, nitalihrukuru jina lako, kwa ajili ya fadhili zako na uaminifu wako, kwa maana umeikuza ahadi yako, kuliko jina lako lote.*” (*Zab 138:2*) Nguvu kali za silaha ambazo ni neno la Mungu zilimfanya shetani atoroke kutoka kwake Kristo!

Sawa na haya pia, ukitaka kumshinda shetani, wewe pia lazima ujue jinsi ya kutumia Biblia kama chombo cha kujikinga usishambuliwe na adui shetani. Pale shetani anapopanda mawazo yake mabaya katika roho yako, unafaa kurudia neno la Mungu. Muda uliotengwa vyema wa *kuwa pamoja na Mungu* utakusaidia kuhakikisha kwamba Neno la Bwana linaishi ndani ya moyo wako katika saa kama hii.

Shairi hili ambalo limeandikwa na mwanasanaa ambaye jina lake halijukani lina msingi wake katika



## *Wakati wa Kuwa Pamoja na Mungu*

ukweli jinsi vile ulivyoandikwa katika Waefeso 6,  
kifungu cha sita.

### **Mbinu za Shetani**

Nilikuwa na vita vikali siku ya leo  
katika sehemu yangu ya maombi.  
Nilienda kukutana na kuzungumza naye  
Mungu,  
lakini nikampata shetani pale.  
Kwa sauti ya chini akasema hivi, “Wewe huwezi  
kuomba;  
ulishindwa zamani kabisa.”  
Unaweza ukatamka maneno ukiwa umepiga  
magoti, hata hivyo huwezi kuomba, unajua  
hivyo.

Kwa hivyo nikavuruta kofia ili inishike vyema,  
nikaivuta hadi kwenye masikio yangu;  
Na nikapata kwamba ilinisaidia kupunguza  
sauti, na kuniondolea hofu.  
Nikaangalia silaha zangu pia;  
miguu yangu ilikuwa imevaa amani  
Kiunoni nimefunga ukweli.  
Upanga wangu; Neno la Mungu.  
Kifuani nimevaa uadilifu' moyo wangu ukiwa  
unakinga upendo  
Ngao yangu ya imani hajaguzwa;  
mishale yake ya moto iliyo rushwa inarudi kule  
ilikoi toka.  
Nikamuita Bwana kwa jina la Yesu;  
nakuomba kuititia damu yake ya dhamana,



## KUZA IMANI YAKO

huku shetani akirudi nyuma na aibu,  
Nikakutana na kuzungumza naye Mungu!

**Vita Vikali Vya Kiroho:** Ushindi kamili unahitaji mbinu zaidi kuliko kujikinga tu! Wako wengi wanaotaabika huko nje. Nyumbani kuna mabilioni ya watu wenye thamani kubwa ambaao kwa ajili yao, Kristo alikuifa. Kila mahali, waume na wake wanaumia, wengi wameshikwa na kufanywa vipofu, na kufungwa na mwovu shetani. Naamini kwamba shetani anajua muda wake ni mfupi hapa duniani, kwa hivo anafanya kila awezalo kuhakikisha kwamba wengi ambaao hawajamjua Mungu wanaangamia kabisa.

Ingawa tunasoma jinsi vile Mungu ameandaa moto wa milele kumchoma shetani na wenzake, ni lazima tukumbuke Mungu hakuandaa moto huu kwa ajili ya wanadamu. La! Ni kwa ajili ya hawa wote waliopotea Kristo alikuifa. Hata hivyo, kwa ajili ya uadui wa shetani kwa yote yaliyo mema na yenye utukufu, ana hamu ya kuwachukua wengi kwenda kuwa nao katika maisha yale yake ya milele ya taabu. Katika vita vyake vya kukomboa waliopotea, Kristo *alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea* (*Lk. 19:10*). *Kupitia waKristo ambaao wamejitoa kumtumikia.*

Umewahi kujiuliza ni kwa nini watu ambaao wamekomaa na wana ujuzi wa kutosha wakati fulani hushindwa kuelewa ujumbe kutoka Maandiko Matakatifu? Katika Biblia, tunaambiwa ni nani



## *Wakati wa Kuwa Pamoja na Mungu*

ambaye anawachanganya katika mawazo yao, na ni kwa nini ni vigumu kwa watu fulani ambao hawana imani kupokea wokovu:

*Lakini ikiwa injili yetu imesitirika, imesitirika kwa hao wanaopotea; ambao ndani yao Mungu wa dunia hii amepofusha fikira zao wasioamini, isiw azukie nuru ya injili ya injili ya utukufu wake Kristo aliye sura yake Mungu (2 Kor. 4:3-4).*

Ni nani anayezuia mwanga wa upendo wa Mungu na ukweli kupenyeza mawazo ya yule ambaye hana imani? Ni shetani! Je, unatilia jambo hili maanani unapokuwa ukiomba ili watu - wake kwa waume - wapokee wokovu? Tunapoomba, lazima tufanye hivyo ili mawazo ya wale ambao hawajamjua Mungu yaweze kuwekwa huru kutoka kwa uongo wa shetani kuititia kulitaja jina lile kuu lililo na uwezo. Ni jina hili la ajabu, zuri, lenye nguvu na ushindi ambalo Charles alizungumzia aliposema:

Yesu! jina lililo juu kuliko yote,  
Katika jehenamu, duniani na katika anga;  
Malaika na wanadamu wanaanguka mbele yake,  
Shetani huogopa na kupaa kwenda mbali.

Ni kweli! Ushindi dhidi ya shetani na wenzake ulipatikana pale msalabani: *Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alidhihirishwa, ili azivunje kazi za ibilisi* (1 Yoh. 3:8). Hallelujah! Hatupigani vita ambavyo tayari tumeshindwa. La, kamwe! Tunazidisha mapambano ambayo ushindi wake ulipatikana kwa niaba yetu

## KUZA IMANI YAKO

yapata karibu miaka elfu mbili hivi iliyopita pale mwokozi wetu alikuwa msalabani.

Katika mashindano ya mchezo uitwao chess, unaweza ukachukua hatua kamili ambayo kutoka pale, kushindwa kwa mwenzako huwa ni wa wazi. Lakini ikiwa mshindani wako ni mchezaji ambaye ana ujuzi wa mchezo, ingawa ni lazima atashindwa, yeze anaweza akaendeleza mchezo kwa muda fulani kabla hajashindwa.

Shetani yuko hivyo. Ingawa hakuna namna jinsi vile anavyoweza kuibuka mshindi, yeze hujaribu kuzuia ushindi wa Kristo usije mara moja. Ni jambo la kumshukuru Mungu kwamba wakati huu anapoendelea na hila zake kabla hajafungwa na minyororo, sio tu yeze ni **adui ambaye tayari anashindwa**, ila yeze pia ni **adui ambaye anajulikana**. Biblia inasema: *kwa maana hatukosi kuzijua fikira zake* (2 Kor. 2:11). Ujuzi wa mbinu za adui ni kitu cha msaada mkubwa kwetu sisi walio katika vita naye!

Mtume Yohana aliandika nyaraka za maelezo kuhusu ushindi wa wale walio watukufu ambao walikuwa wamemshinda shetani, na sawa na ushindi huu, Mungu pia alikuwa ni mshindi *nao wakamshinda kwa damu ya Mwana-kondoo, na kwa neno la ushuhuda wao; ambao hawakupenda maisha yao hata kufa* (Ufu. 12:11). Hatupendi maisha yetu hadi kifo, kwa sababu *tukijua neno hili, ya kuwa utu wetu ulisulubishwa pamoja naye* (Rum. 6:6).

**Kweli, ni damu inayoosha dhambi inaleta kutubu kwetu na kutufanya kuwa waliosulubi wa**



## *Wakati wa Kuwa Pamoja na Mungu*

**pamoja na mwokozi wetu Kristo. Na hii ni thibitisho la ushindi wetu kupitia Kristo juu ya nguvu za shetani. Halleluya!**

Furahi pamoja nami kwamba Kristo amefanya yote ya kutuwezesha kuwa watu wazima ambao ni waKristo wanaoshinda adui. Wakati huo huo, lazima tujue kwamba ikiwa hatuna hamu ya kwenda mbele zaidi kupita kiwango kile cha darasa la kwanza katika mambo ya Mungu, Mungu hatalazimisha ukomavu wa kiroho kuingia ndani yetu. Uwezo wetu wa kiroho, na kiwango hikicha kiroho hutegemea muda ambao tunao hapa duniani, na jinsi vile tunakomaa kiroho katika Bwana. Kiwango hiki cha kukomaa kitatuletea furaha ambayo haina kizuizi chochote, na ushirika wa karibu sana naye Mungu mpaka pale tutakapofika juu mbinguni.

## **Ichunguze Roho Yako**

Jiulize maswali haya:

1. Ni nini mimi huwaza juu ayke pale ninapoenda kitandani kulala?
2. Ninaposoma Biblia, nataraji kusikia sauti yake Mungu au la?a
3. Ninaposoma Biblia, nina nia ya kufanya yale ambayo Mungu amesema au la?
4. Ninapozungumzia maisha yangu, mimi nayaona kuwa ni “yangu”au ya “Kristo aliye hai ndani yangu?”
5. Je, mimi ni mtu anayejitegemea? Kama ni hivyo, niko tayari kuachana na kiburi changu na kuanza kumtegemea Mungu?  
*(Wagalatia 2:20)*
6. Je, nafahamu kwamba kumsujudu Mungu ndilo jambo kuu ambalo naweza kujihusisha nalo?
7. Je, shetani amepta makao katika maisha yangu?
8. Je, nahitaji kujitwalia ushindi wa Kristo juu ya shetani?





*Imani yangu imepata mahali pa mapumziko  
mahali, sio katika chombo wala imani:  
Naamini yule ambaye daima yuko hai,  
Maumivu yake kwa ajili yangu nayatetea.*

*Moyo wangu umeinama kwa neno,  
Neno lililoandikwa la Mungu,  
Wokovu kupitia jina lake mwokozi,  
Wokovu kupitia damu yake.*

*Sihitaji mabishano,  
Sihitaji himizo lingine,  
Inatosha kwamba Kristo alikufa,  
Na kwamba alikufa kwa ajili yangu.*

*Lidie H. Edmunds*

## *Umuhimu wa Imani*

Katika mawazo yako, hebu waza kuhusu mtu ambaye inambidi avuke mto ambao umevurugika ili amfikie rafiki yake ambaye yuko upande wa pili wa mto huo. Hana mtumbwi ila tu tiara (kite) na uzi mkononi. Kila uzi una nguvu na nyuzi zinaweza kutengeneza kamba kubwa. Akitumia uzi mwembamba, mtu yule anapeperusha tiara yake kwa njia maalum hivi kwamba inatua katika mikono ya rafiki yake upande ule mwingine wa mto huu. Katika tiara ile ya mwanzo, sasa ye ye anaweka uzi ule na nguvu zaidi kuliko ule wa kwanza mpaka pale sasa nyuzi ni kamba ilio na nguvu sana. Na kamba hii sasa wanafunga kwa mti, na kutumiwa kuvuka mto ule na kumfikia rafiki wake.

Ukiwa mtoto wa Mungu aliyezaliwa mara ya pili, tayari umeweka imani yako katika kifo kile cha Mwokozi wetu Yesu Kristo kama kifo ambacho kilitokea mahali ambapo ulistahili kufa kwa ajili ya dhambi zako. Pale wewe ulistahili kufa, ni ye ye alikuwa kwa ajili yako. Lakini pale unapoanza kusoma Biblia,

## KUZA IMANI YAKO

imani yako huenda ikawa hafifu sawa na wakati ule wa kutumia uzi wa kwanza. Na hata uzi huo hafifu ulikuwa wa manufaa kwani ultiweza kuelekeza tiara hadi upande wa pili wa mto. Hata hivyo, kwa vile *imani chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo (Rum. 10:17)*, utagundua unapoendelea kusoma neno la Bwana, na kushikilia ahadi zake za thamani, imani yako itazidi kukuwa. Lengo lake Mungu ni kwamba kila mtoto wake azidi kukuwa katika imani yake. na hii inamaniisha kwamba lengo lake ni kila mwenye imani awe na uhusiano wa karibu sana naye Mungu mwenyewe.

Biblia yahusu jinsi vile kuna haja kujenga kutoka kwa msingi ule wa kwanza wa wokovu. *Bali ninyi wapenzi, mkijijenga juu ya imani yenu iliyo takatifu sana (Yud. 1:20).*

*Msitari huu unasisitiza kwamba katika msingi huu wa imani na wokovu, tunastahili kujijenga kiroho, na kuendeleza imani yetu kupitia njia kustawisha maisha ya maombi, upendo, matarajio, kuwa na huruma na kujitahidi kuwaleta wengi kwake Yesu. Twasoma hivi katika kitabu cha Yuda: Bali ninyi, wapenzi, mkijijenga juu ya imani yenu iliyo takatifu sana, na kuomba katika Roho Mtakatifu, jilindeni katika upendo wa Mungu, huku mkingojea rehema ya Bwana wetu Yesu Kristo, hata mpate uzima wa milele. Wahurumieni wengine walio na shaka, na wengine waokoeni kwa kuwanyakua katika moto; na wengine wahurumieni kwa hofu, mkilichukua hata vazi lililotiwa uchafu wa mwili (Yud. 1:20-23).*

**Kupitia kujenga maisha yako na msingi wa maombi, upendo, imani iliyo hai, moyo wa msamaha**

## *Umuhimu wa Imani*

### **na kujitoa kuwavuta na kuwaleta wengi kumjua Mungu.**

Na jinsi vile wokovu wetu ulipatikana kama zawadi ya bure kupitia imani, sawa na haya pia pale unapojichukulia uhai wa Mwokozi wetu na kuuweka ndani yeye aliye fufuka, maisha yako yatasimamiwa na Mwokozi huyu aliye hai. Ni kweli kabisa kwamba, *wenye haki wataishi kwa imani* (*Rum. 1:17, Gal. 3:11, Ebr. 10:38*) Ukiwa mbinguni au hata hapa duniani, lazima uishi kwa imani. Lazima uishi kwa kumuamini Mungu na ahadi zake, na kuwa tayari kutumiwa naye katika kufanya kazi yake. Hata utakapofika juu mbinguni, imani yako itakuwa kama barabara ambayo utafurahia na kushukuru katika ahadi za Mungu na lengo lake la kukuwezesha kuwa na upendo ambao unazidi kila kitu ambacho mawazo yako yenye wokovu yamewahi kuwaza na kuelewa

Ukiwa ungali hapa duniani, imani ya kweli lazima imtegemee Kristo ili afanye **ndani yako** yale ambayo hungeweza kuyatimiza mwenyewe. Tukiwa watoto wa Mungu, ni jambo la muhimu kukuwa katika imani. Lazima tuzidi kumtegemea yule ambaye ametupatia uhai na pia kupanga mienendo yetu ya kila siku.

Hata hivyo, mara nydingi, sisi hutumia busara yetu wanadamu ambayo hujitahidi kubadili yale yaliyo ya imani halisi na kuweka pahali pake yale yanayohusu sisi wanadamu wenyewe. Hali ile ya kujisikia kuwa huru tukiwa wanadamu hujaribu kubadili yale yanayohusu imani, na badala yake kuweka hapo mambo fulani ya kujitoa katika huduma ya Mungu. Hata hivyo, imani ya kweli haihusu moja

## KUZA IMANI YAKO

kwa moja yale ambayo tunafanya katika huduma ya kuendeleza mambo fulani ya kikristo. Hayahusu kuwa mfuasi halisi wa kasisi fulani, wala kupokea mafunzo maalum ya Biblia. Ingawa mambo kaama haya yanaweza yakawa ishara inayoonyesha kiwango cha imani mtu alicho nacho. Hata hivyo, haya yote yanaweza kutumiwa na mkristo kuwa mambo ambayo yamejitokeza kuwa mbele hata kuliko imani ya kweli.

Imani ya kweli inahusiana na jinsi vile tunavyomtegemea Kristo aliyefufuka. La kusikitisha ni kwamba wako wakristo wengi ambao wanafikiria kwamba wanawenza kufanikiwa maishani kupitia matumizi ya talanta zao, ama matumizi ya mbinu fulani fulani, ama hata kupitia matumizi ya pesa walizo nazo katika benki. Biblia inatuambia wazi kwamba sisi tukiwa wale waliozaliwa mara ya pili, tukitaka kufa nikiwa katika mambo yetu, basi kuna haja tuwe tunasimamiwa na kuongozwa na Roho Mtakatifu. Ikiwa hatutajizoesha kumtegemea Mungu, kazi yote ambayo tunaichukuwa kuwa kitu ambacho kinafaa kuliko imani - kazi hii yote itakuja kuharibika na kutoweka siku moja. Uwezo wetu kama Wakristo hautegemei jinsi vile tuna **hamu ya kufanya** mambo fulani wenyewe, lakini inategemea kile ambacho kilituelekeza au kilituongoza tukapokea wokovu.

Chochote kinachopatikana katika maisha yako ambacho kinakuweka katika hali ya kujiona kwamba wewe hauko pweke ni ishara kwamba maisha yanakosa mwelekeo. Pesa, elimu, marafiki, uwezo wako, kazi na hata maumbile yako - ikiwa chochote

## *Umuhimu wa Imani*

kitakufa nya ujione kuwa mtu ambaye si pweke, basi chunga huenda haya yote yakawa ishara kwamba hauna imani ya kutosha. Kile ambacho kinastahili kukutia moyo na kukufanya usiwe na woga, na kujisikia wewe ni kiumbe cha muhimu hapa duniani ni Wokovu ulio nao. Ikiwa hautaishi maisha ya kumtukuza Mungu ukiwa hai hapa duniani, basi utakuwa umenyimwa furaha kubwa inayotokana na kuishi na Mungu maishani, na huduma yake ya upendo kupitia ndani yako *kila tendo lisilotoka katika imani ni dhambi* (*Rum. 14:23*).

Kwa kweli, G. Keith alielewa umuhimu wa “kula” neno la Bwana ili kuchangamsha imani alipoandika:

Ni jinsi gani msingi ulivyo,  
Enyi watukufu wa Mungu,  
Umewekwa kwa ajili ya imani yenu  
Katika neno lake.

Kama sauti ya Bwana haitasikika katika miyo na maisha yetu, hatutaweza kuwa na msingi wa imani wa kukuwa kiroho, na hakutakuwa na simiti wala mchanga wa kujenga msingi huu mpaka pale mpango maalum wa kuwa pamoja na Mungu pamoja na Mwokozi katika ushirika wa karibu kabisa.

***Imani ni kitu ambacho kina uwezo wa kutembea; kitu ambacho hujenga ushirika wa karibu na Mungu.***

Ni miaka kadha hivi imepita tangu kisa kimoja kutokea. Nakumbuka nilikuwa nahubiri kuhusu ufufuo katika mkutano wa karibu makasisi mia moja hivi Uingereza. Mungu alikuwa tayari amefanya

## KUZA IMANI YAKO

kazi kubwa kati yetu. Tulipokuwa tunaelekea wakati wa maombi ya hadhara, kasisi mmoja aliamka na unyenyekevu huku machozi yakimdondoka, akaomba hivi: "Mungu, natubu leo hii kwamba kila mara nisimamapo mbele ya hawa wandugu wangu kuomba, mimi hutilia maanani theolojia kuliko yale yanayohusu utukufu wako amba o uko nasi wakati wa kuwa pamoja nawe."

Miyo yetu ina udanganyifu kiasi kwamba hata tunapokuwa tunaomba katikahadhara, huwa tunajificha nyuma ya matamshi yetu. Huwa hatufungi roho zetu na kupeleka mahitaji yetu mbele ya Mungu wetu aliye juu mbinguni." Kuomba na kutumia maneno kama haya, haimanishi kwamba kwa kwelitunawasiliana moja kwa moja na Mungu wakati wa maombi haya. Ni pale tu tunapofungua roho zetu, ili ziwe na lengo moja sawa na lile la Baba wetu aliye juu mbinguni, hapo ndipo baba wetu aliye juu mbinguni hufurahi wakati huu wakuwa katika ushirika naye.

Ni jambo gumu sana kuangalia na kuona jinsi vile mwenye dhambi anavyoweza kumletea Mungu hali ya kutosheka. Biblia nayo inasema wazi kwamba Mungu alimuumba mwanadamu kwa ajili ya sababu hii. Tupende tusipende, sisiwanadamu tumeumbwa tumtukuze Mungu!

*Mwenende kama ulivyo wajibu wenu kwa Bwana, mkimpendeza kabisa (Kol. 1:10)* Hili ni jambo ambalo lilikuwa lakumtia hamu kuu sana mtume Paulo wakati ulipofika wa kuhudumia kanisa la Kolosai. Askofu Handley Moule alitafsiri maneno haya hivi:

## *Umuhimu wa Imani*

*bila kutumai nia yake. Labda hilo ndilo tunamaanisha tunaposema: Jisurahishe mwenyewe. Kufurahisha kuna maana kutilia maanani mahitaji ya wenzako kuliko yale ambayo ni yako.*

Tukijaribu kujifurahisha wenyewe zaidi yakumfurahisha Mungu, hii yaweza kutufanya tujikwae vidole vyetu katika mawe, na kugonga vichwa vyetu katika ukuta, na kugonga vitu vya aina aina ambavyo viko katika barabara tunayopitia maishani. Lakini ni furaha ilioje katika moyo wa yule ambaye ana imani na katika moyo wa Mungu pale mtoto wa Mungu anaposhiriki pamoja na Mungu mwenyewe aliyuumba.

Biblia ni ya msaada inapofichua kwamba kuna uhusiano wa karibu sana kati ya ‘imani’, na ‘kumfurahisha’ Mungu, Njia ile ambayo imetumiwa kuandika ukurasa huu wa maandiko matakatifu unawezesha msomaji kuona wazi uhusiano ambaou uko kati ya imani na kumfurahisha Mungu: *Pasipo imani, ni vigumu kumfurahisha Mungu...* Msitari huu baadaye unaandikwa kwa njia iliyo tofauti na kuwa msitari ambaou ni wa kumtia moyo ye yeyote yule aliye na imani ya kweli. Msitari unatueleza kwamba ushirika na Mungu pia huleta zawadi kutoka kwa Mungu: *...Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu **amwendeaye Mungu** lazima aamini kwamba yeeye yuko, na kwamba **huwapa thawabu** wale wamtafutao* (Ebr. 11:6)

Zawadi za kiroho ambazo Mungu kwa ajili ya utukufu wake humpa yule ambaye anaishi akiwa na uhusiano wa karibu sana na Mwokozi wetu

## KUZA IMANI YAKO

hauwezi kuelezw na maneno matupu. Twaweza tu kuyaelewa pale tunapoona upendo na kuhisi upendo huu sisi wenyewe. Na kile ambacho chaweza kuleta ushirikiano ulio hai na Mungu, ushirikiano ambao utamfurahisha, na hata kufurahisha watoto wake ni **imani**.

***Imani ni gari ambalo Roho Mtakatifu hutumia kubeba ushindi wa Kristo aliyefufuka hadi kwa mtoto wa Mungu.***

Sawa na jinsi vile tayari tumegusia, inawezekana, na ni kitu cha kuhuzunisha kwamba tunaweza kukutana na ahadi za Bwana kuititia njia ya kusikiliza mahubiri ama kwa kusoma neno la Bwana, na haya yote yasiwe hayana faida ya kiroho kwetu sisi: *Lakini neno lile liliosikiwa halikuwafaa hao, kwa sababu halikuchanganyika na imani ndani yao waliosikia (Ebr. 4:2).*

Ni pale tu neno la Bwana linapotoka kichwani na kuteremka mpaka katika moyo likiwa linakorogwa na kijiko ambacho ni imani; hapa ndipo usomaji wa neno hili utakuwa wa faida kwako. Ni pale ambapo Roho Mtakatifu anaweka nguvu zake zenye utukufu wa Yesu Kristo katika maisha yetu ndipo tutaweza kuchukua kila nafasi inayojitokeza kumtumikia Bwana, na hapo kuonyesha wazi uweza wa nguvu **zake** wakati wa kukumbana na kila aina ya shida katika maisha yetu.

Jambo moja, nalo ni la hakika ni kwamba kila mtu aliye na imani lazima kuna wakati ambapo anakumbana na majoribio makali sana maishani. Shetani mwenyewe hutumia dunia hii na vishawishi

## *Umuhimu wa Imani*

vingi vilivyomo kujaribu kutufanya tutupilie mbali maisha yetu ya siku baada ya siku ya kuwa na ushirika na Mungu wetu. Hakuna kitu kibaya sana sawa na uhaini kwa shetani kama mtoto wa Mungu ambaye yuko katika ushirika na mwokozi wetu Mungu. Kwa hivyo, si ajabu kwamba mwovu hujitahidi kwa kila njia akifanya yale anayoweza kuwafanya wakristo ambaao ni watu waliozaliwa mara ya pili watupilie mbali uhusiano wao na Mungu, na kuacha kujenga imani yao kupitia njia ya *kuwa pamoja na Mungu*.

Katika yule aliye na imani hafifu, ambaye hajapevuka kutosha, dunia na utajiri wake ni vitu vyaa muhimu zaidi ya vyote maishani. Ukweli uko mbali sana na wazo kama hili. Ukweli ni kwamba Roho Mtakatifu ndiye wa maana sana duniani kuliko vyote. *Maana kila kilichomo duniani, yaani, tamaa ya mwili, na tamaa ya macho, na kiburi cha uzima, havitokani na Baba, bali vyatokana na dunia (1 Yoh. 2:16)*. Na kwa vile watu hudanganywa kwa urahisi sana, shetani ana kazi nyepesi ya kutumia mbinu mbali mbali kuwashawishi wa Kristo kupotea njia.

Biblia inatuambia wazi kwamba tunajaribiwa kupitia: Tamaa za miili yetu we nyewe (Yaani kutafuta raha na huku hatutaki kuwajibika) Tamaa ya macho yetu (kutaaka kuwa na vile ambavyo hatustahili kuwa navyo kwa ajili si vyetu) Kiburi maishani (kuwa na nguvu bila kuwajibika) Shetani anajua hila nyingi mno za kujingiza na kuwa changa nya waKristo na kuharibu yale ambayo Mungu amewapangia walio na imani. Yeye atafanya kila awezalo kuhakikisha kwamba anatuweka mbali na Mungu wetu. Mwovu

## KUZA IMANI YAKO

anajua tukiwa na upendo wa Mungu wetu, imani yetu itastawi na kukuwa kiroho na hapo kumfurahisha Mungu wetu zaidi.

**Tamaa Ya Mwili:** Ni kupitia dunia hii ya uovu ambayo imeja mengi yanayohusu dhambi ya uasherati Shetani amepata nafasi ya kuwajaribu wakristo kupitia tamaa ya mwili. Adui wetu anapata nafasi ya haraka sana kuingia katika maisha ya watu wake ambao wanajingiza katika mambo ya kuwafurahisha na kusisimua miili, na kutafuta mali. Hata hivyo, wale ambao wamedanganywa na mwovu shetani watakuja kuona kwamba yale yote yakuwafurahisha, yote ambayo ni dhambi yametoweka ghafla na kuwaacha wakiwa hawana chochote isipokuwa aibu!

**Tamaa Ya Macho:** Ikiwa tutavutiwa na vitu maridadi ambavyo ni matangazo ya biashara, ikiwa tunatamani vile ambavyo wenzetu wanavyo, basi hapa shetani anaweza kupata nafasi ya kupiga hatua mbele kuingia katika maisha yetu. Mwongo mkuu husema na ushawishi mkubwa: “Ikiwa tu ungekuwa na saa ya mkono mpya, ama kiasi cha eka moja cha shamba zaidi, ama nyumba kubwa, utaweza kufurahi.” Lakini kwa vile ...*mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu* (*Mt. 4:4*), tunagundua haraka kwamba, baada ya kujiingiza katika mambo haya yaliyo ya uovu kwamba yote ambayo tumejiongezea hayatatuletea furaha.

**Kiburi Maishani:** Mlango ambao hutumiwa na shetani kutuangamiza hufunguliwa wazi na majivuno

## *Umuhimu wa Imani*

yetu sisi wenyewe na maringo ya kujiona kuwa sisi ni watu wanaofaa kuliko wenzetu, na pia kwamba sisi tunaweza kutosheleza mahitaji yetu wenyewe pasipo usaidizi kutoka popote. Mungu anachukia majivuno ya kila aina!

Kwa kweli, kuwa na imani kwamba tuna uwezo wa kuamua na kusimamia ni wapi tunaelekea maishani ni kinyume cha kuwa na Imani katika Mungu - **imanı** kwamba Mungu Mwana Yesu Kristo ndiye atakayetutimizia yote. Na jinsi vile tayari tumesema, Mungu amesema kwamba njia kukabili nayo kiburi na majivuno yetu wanadamu ni *jidhilini mbele za Bwana, naye atawakuza* (*Yak. 4:10*). Ukikubali kwa unyenyekevu kwamba wewe ni kiumbe ambacho kinamtegemea Mungu, hii ni njia moja ya kumfungia Shetani mlango pale anapajaribu kukushawishi eti unajiveza mwenyewe. Mungu anatwambia wazi kwamba **huku ndiko kushinda kuushindaako ulimwengu, hiyo imani yetu** (*1 Yoh. 5:4*).

Lakini kabla hujaingia **kabisa** katika hali ile ya kuwa na imani ya ushindi kamili (pale shetani anapokujaribu na kila kitu ambacho kiko duniani), ni bora wewe kujifunza funzo ambalo Kristo aliwafunza wanafunzi wake. Alitoa onyo kuhusu pingamizi kuu ya imani. *Mwawezaje kuamini, ninyi mnaopekeana utukufu ninyi kwa ninyi, na utukufu ule utokao kwa Mungu aliye wa pekee hamwutafuti?* (*Yn 5:44*). Katika matamshi haya, Kristo aliwaonya wafuasi wake imani ya kweli haiwezi kustawi pamoja na hamu ya kutaka kupokea sifa kutoka kwa watu.



## KUZA IMANI YAKO

Pale unapofurahia wakati wako wa *kuwa pamoja na Mungu*, imani yako itastawi na kukuwa. Na baadaye unapokumbana na majaribu maishani, utajua jinsi ya kutumia imani yako iliyo na nguvu, na nyepesi ya kushinda hila za muovu.



## **Ichunguze Roho Yako**

1. Katika shughuli zangu za kila siku, mimi nafurahia imani inayofanya kazi?
2. Je, naona shida katika katika kila jambo ambalo lajitokeza, shida ambayo itaonyesha uwezo wake Kristo katika kila hali, na katika kila shida?
3. Je, nina hamu ya kuona mapenzi yake Bwana yakiendelea kutendeka au nina hamu ya kuona mapenzi yangu binafsi yakiendelea?
4. Je, maisha yangu yako katika ile hali ambapo siwezi kutishwa kwa urahisi kwa ajili natumia muda wangu mwangi kuwaza na kumtegemea Mungu?



*Mungu, sema nami, ili nami niweze kusema  
Jinsi vile wewe umetafuta, kwa hivyo niache niseme  
Watoto wako walio na dhambi, wamepotea na wako  
katika hali ya upweke.*

*O nifunze, Mungu, Ili nami niwafunze  
Mazuriya thamani ambayo wewe hutoa;  
Na yape mabawa maneno yangu, ili yafike  
Sehemu zilizofichika katika mioyo ya wengi*

*O njaze, Mungu  
Mpaka pale nitajaa na kufurika  
Na mawazo mazuri na maneno yanayo meta meta,  
Upendo wako kuutaja, sifa zako kuonyesha.*

*Frances Ridley Havergal*

# *Wakati wa Kufichua Siri*

Usiku mmoja, baada ya kazi ya kuhubiri, mzee mmoja alinikaribia, akanisihi nimwombee. Tulikuwa tumeona nguvu za Bwana katika njia iliyokuwa ya ajabu kabisa. Baba huyu aliniambia alikuwa na shida. Shida hii ilikuwa kwamba alikuwa anapata ugumu kutoa ushuhuda mbele ya wale anaofanya nao kazi na hata mara fikikwingi neko. Sawa na jinsi vile mimi hufanya kila wakati, ombi langu la kwanza lilikuwa kwamba Mungu anifunulie ili niweze kujuwa ni nini hasa mzee huyu alikuwa anahitaji maishani. Nikajikuta namjibu: “Sifikirii shida yako kuu ni hii ya kutoweza kutoa ushuhuda mbele ya wenzako kazini. Hebu tupige magoti hivi sasa na umwulize Mungu akueleze ni kwa nini unapata ugumu kushuhudia kuhusu imani yako.”

Bila kusita, mzee huyu alipiga magoti na akaanza kuomba. Alipokuwa akifa nya hivyo, ilibainika

## KUZA IMANI YAKO

wazi kwamba Mungu alikuwa anafichua shida kuu kuliko ile ambayo baba huyu alikuwa ameitaja hapo mbeleni. Kwa moyo wa unyenyekevu, baba huyu alikuwa anakiri mbele ya Mungu jinsi vile amekuwa mzee wa kimabavu nyumbani kwake, na jinsi vile alikuwa anawanyanya watoto wake. Akiwa na moyo uliovunjika kabisa, na ulio na hamu ya kutubu, alimsihi Mungu amsamehe.

Usiku ule, hatukuzungumza lolote kuhusu jinsi ya kushuhudia kwa ajili Kristo alikuwa amejifichua kwa baba huyu kwa njia mpya yenye uhai na iliyo ya ajabu kabisa. Siku iliyofuata, yeche alikuja mkutanoni akiwa na uso wa furaha akasema hivi: “Sijaweza kunyamaza hata kidogo na kuacha kuwaeleza we nzangu kuhusu Kristo siku ya leo.”

Hakuna popote katika maandiko matakatifu ambapo tunaelezwa eti kwamba tupeane mpango wa kujitengenezea wenyewe unaohusu wokovu kwao wale ambao hawajampokea Kristo. Hata hivyo, tunahimizwa kutembea tukiwa katika ushirika na Kristo kila mara ili tunapowaeleza habari ya wokovu, upendo ulio ndani yetu utaweza kujitokeza na kufanya roho zao ziweze kusikiliza Neno la Bwana.

Hata hivyo, siku zile ambapo mioyo yetu **haiko** katika laini moja ya ushirika ulio hai na Mungu, tutagundua mara moja kwamba kazi ile ya kushuhudia haizai matunda **wala** kuwa na nguvu. Kwa kweli, hata siku kama hizi, vinywa vyetu vitafungwa na hatutaweza kuzungumza lolote ambalo ni la kujenga mtu kiroho. Hata hatutaweza kusema lolote kwa wale ambao wanapuuza Neno la Bwana kati yetu.

## *Wakati wa Kufichua Siri*

Unapoamka na kitu cha mbele kiwe ni wakati ambaao umeutenga *kuwa Pamoja na Mungu*, hii itaondolea mbali vikwazo ambavyo vyawenza kujitokeza na kukufa nya usiweze **kueneza** ujumbe wa wokovu kwao wale ambaao hawajapokea Kristo. Kuna tofauti kubwa sana kati ya kuweza kuhisi na kuweza kuona maisha yanayofaa ya kikristo katika dunia hii ambayo haina Mungu. Pia kuna tofauti kubwa kati ya kuwa mtu sawa na kuwa mtu ambaye ni “muuzaji” wa injili. La! Mwenye imani hastahili kusimama mbele ya dunia na kusema maneno fulani ambayo **ni kama** mfano wa ushuhuda wa Kikristo. Badala ya hayo, ye ye ambaye amezali wa mara ya pili anastahili kuwa na uhakika kwamba **Kristo yuko ndani yake**, na akiwa katika hali hiyo, anataja mambo ya Mungu akiwa na furaha.

Sawa na jinsi vile Kristo aliwaambia wafuasi wake, *akaaye ndani yangu, nami ndani Yake, huyo huzaa sana; maana pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lolote* (Yn. 15:5). Kukaa ndani yake, na kuwaambia wenzako yale yanayohusu Kristo, hilo ni jukumu lako. Mazao yanayotokana na huduma yako, mazao hayo yanatokana na yale amefanya mwenyewe. Ni kazi yake!

Baada ya siku ya Pentekoste, wafuasi wa Kristo hawakuweza kuficha furaha waliokuwa nayo baada ya kuzungumza na kutembea na Mwokozi aliyefufuka. Kila mahali walikoenda, walieneza habari njema—hata kwa wale ambaao walikuwa na uadui na Kristo—*kuhusu matendo makuu ya Mungu* (Mdo. 2:11). Hamu ya kutaka kujua mengi kuhusu yale waliokuwa

## KUZA IMANI YAKO

wakisema hawa waKristo iliwaingia wengi wa wale waliokuwa wakiwasikiliza. Matokeo ni kwamba maelfu ya watu walijikusanya kusikiliza Mtume Petro akihubiri katika hadhara kuhusu vile Kristo ni Mungu. Alipokuwa akihubiri, makosa ya wale waliokuwa wakimsikiliza yalijitokeza wazi. Hao ambao walikuwa wamemsilibisha Kristo walilia wakisema, *tutendeje ndugu zetu?* (*Mdo. 2:37*). Siku hiyo, ushuhuda wa mitume na mahubiri ya Petro pamoja na wenzake yalileta mavuno makubwa ambayo ilikuwa ni ongezeko kubwa la wale ambao walipokea wokovu.

Baadaye, wakiwa wanaishi katika sehemu iliokuwa na maadui wengi, mitume hawa walikutana na Yesu katika mkutano wa maombi kwa njia ya ajabu kabisa. Watu waliojiita kwamba wao ni “watu wa dini” walikuwa wamewakataza mitume wasiendelee kutaja jina la Yesu. Mapema kidogo, wakiwa katika chumba cha juu (Upper Room), Kristo hakuwa amewafunza jinsi kueneza injili, lakini kwa vile sasa walikuwa wamejawa na roho mtakatifu, wakristo hawa waliokuwa na hamu kuu walijibu na kusema: *sisi hatuwezi kuacha kuyanena mambo tuliyoyaona na kuyasikia* (*Mdo. 4:20*). Wao tena walikuwa wamekuwa mbele ya Mungu wao! Miyo yao ilikuwa ina moto uliotokana na sababu kwamba walikuwa wamemuona Bwana wao ambaye alikuwa amefufuka. Hawangeweza kukaa kimya!

Katika miaka ya sitini, mimi na Dorothy tulikuwa tukifanya kazi ya kuhubiri katika inchi ambazo zilikuwa zimefungwa ili injili isiwafikie watu wake,

## *Wakati wa Kufichua Siri*

yaani. n chi ambazo zilikuwa zinaitwa “countries behind the Iron curtain.” Tulipouliza swali tukiwa tunataka kujua ugumu wa kufanya kazi katika nchi hizi ambazo hazikuwa zinawakubalia wainjilisti waendeleze huduma yao, kasisi mmoja alitujibu hivi: “Tuko wachache wakati huu, lakini la kutia moyo ni kwamba sisi tunajijua wenyewe. Sisi ambaa tumebakii tunamjua Kristo aliyefufuka hatuwezi kamwe kushindwa.” (Majaribu kama haya huenda yakawa yamewahi kuwakumba baadhi ya wasomaji wa kitabu hiki, na ikiwa mambo yataendelea jinsi vile yalivyo wakati huu, na kama Kristo hatarudi upesi, basi hakuna shaka wengi wetu itatubidi tujitokeze kumtumikia kwa njia ambayo inazidi hata ile ya wenzetu waliowahi kumhudumia katika mateso na shida.)

Juzi, Dorothy aliandika hivi katika kijitabu chake cha *Kuwa Pamoja na Mungu*: “Gharama ya kifo chake lazima ibebwe na kila pumzi ikiwa roho yake itatoka kwangu.” Ni wazi kwamba mitume wa hapo mwanzo walilipa gharama kubwa kwa ajili ya kujitokeza na kushuhudia bila woga. Na pale walipotishwa na kifungo kwa ajili ya kutaja Kristo, *Hata walipokwisha kumwomba Mungu, mahali pale walipokusanyika pakatikiswa ,wote wakajaa alikutana pamoja kwa ajili ya maombi wote wakajaa Roho Mtakatifu, wakanena neno la Mungu kwa ujasiri.* (Mdo. 4:31).

**Kazi kamili ya kueneza injili hutokana na mtu kujazwa na roho mtakatifu, mpaka roho akazidi na kuanza kumwagika. Roho mtakatifu amejaaa katika**

## KUZA IMANI YAKO

**mwenye imani mpaka sasa anamwagika nje na hapo kuonyesha walio kando ukweli wa Kristo kuishi ndani yao.**

Tunaposoma Agano Jipya, tutagundua kwamba kazi ya kueneza injili katika kanisa la mwanzo haikuwa kazi ambayo iliendeshwa kupitia njia ya kuwashawishi watu. Hakungekuwa na watu wa kumsikiliza Petro akihubiri siku ya pentekoste kama mitume kwanza hawangejitoa na kusema *matendo makuu ya Mungu* (*Mdo. 2:11*).

Pale usafi, maisha, na upendo wa Kristo unapojitokeza, kutoka kwa moyo wa yule mwenye imani na kuelekea katika dunia inayokufa moyo, watu huwa na hamu ya kusikiliza neno la Bwana lililo na ukweli. Na hii ndio sab abu tunahitaji kukutana na Mungu kila siku katika mwanga wa neno lake *ili tujazwe Roho* (*Efe. 5:18*).

### **(Kujazwa na Hamu ya kueneza injili) Maisha Ya Jamii**

Katika siku za ujana wangu, baada ya kupokea wokovu, niliku wa mmoja wa wanachama wa ushirika wa vijana wa kiKristo. Kwa kweli tulikuwa na hamu kubwa sana kuliko ujuzi unaohitajika. Hata hivyo, Mungu aliona ni vyema aweze kututumia kueneza neno lake kati ya wale ambao walikuwa hawajapokea wokovu. Hebu sasa nitaje kwa undani baadhi ya visa ambavyo tulipitia tukiwa vijana chipukizi wenye imani.

## *Wakati wa Kufichua Siri*

**Maisha Ya Kazi:** Wakati nilipokuja kumjua Kristo, nilikuwa nafanya kazi katika Ofisi ya mratibu mjini. Nikiwa nafanya kazi hapa, siku moja niliitwa nikahitajika kwenda katika ofisi kubwa na maridadi ya karani mkuu wa mji. Nikawa nimeitwa kuzomewa vikali. "Nimesikia yale unayoyafanya baada ya kazi," Afisa huyu mkuu akasema kwa ukali. Yale aliyokuwa akiyataja yalihusu kazi yangu ya baada ya kazi ya kueneza injili. Nikiwa pamoja na vijana wenzangu wa rika langu, kila jioni, muda tuu baada majumba ya starehe kufungwa, tulikuwana mtindo wa kuandaa mikutano ya injili katika sehemu moja ya mji huo. Pale mwanzo, hakuna aliyetujali, kwa hivyo tulifurahi sana pale mtu mmoja alipoanza kumfa nyia mzaha aliye kwa akihubiri siku hiyo. Na hapo alipoanza kufa nya hivyo, kuna wale ambaao walijitokeza kumuunga mkono, nao wengine wakajitokeza kuwapinga hao ambaao walikuwa wanatufanyia mzaha. Na baada ya muda mfupi, tukawa tunapata kikundi cha watu wa kuhubiria. Baadaye ikawa mtu mmoja au wawili wanajitokeza na kukiri kwamba wamemkubali Kristo kuwa mwokozi wao. Tukirudia kisa kile ofisini, karani mkuu yule alinionya kwamba mambo kama haya ya kueneza injili kwa njia hiyo kamwe hayatukabiliwa yasimamiwena mmoja wa wale ambaao ni wahudumu wa jumba kuu hili la mji. Alinitaka niache mambo hayo mara moja. Lakini kwa vile kazi yetu ilikuwa imeanza kuzaa matunda, sisi vijana tulionelea ni heri tuendelee na kazi hiyo.

## KUZA IMANI YAKO

Baadaye nikiwa katika chuo cha masomo ya Biblia, nilimsikia mkuu wetu siku moja akisema katika hadhara ya maombi “Ikiwa huwezi kuwashika na kugusa roho za wale walio nje na mahubiri yako, basi usithhubutu kuwachosha wale ambaao wako kanisani ambaao hawana jinsi ya kutoka kanisani humo wakati wa mahubiri.” Niliposikia haya, nilifurahi kwa ajili ya kazi ile tuliofa nya katika hadhara kuwahubiria wapita njia.

Mara tu baada ya kupokea wokovu, nilikuwa nimewashuhudia wenzangu ambaao tulikuwa tunahudumu nao kuhusu jambo hili. Hata hivyo nilimkumbuka mtu mmoja ambaye nilikosa kupata nafasi ya kuweza kumshuhudia. Yeye alikuwa mama mmoja ambaye kazi yake kila jioni ilikuwa kuja kusafisha sakafu. Siku moja, baada ya wenzangu kuondoka, niliona ndoo na vyombo vyaya kusugua sakafu katika sehemu moja ya chumba kile cha mikutano. Nikachukua vyombo vyenyewe na kusugua sakafu, na baadaye nikamngoja mama yule. Alipokuja, nikasema kwa sauti ya juu na furaha: “Kazi yako imefanywa!” Baada ya kugutuka na tukio hili, mama yule alikaa nami mezani, tukawa tuna kikombe cha chai mbele yetu: kila mmoja na chake. katika mazungumzo yetu, niliweza kumtaja Kristo. Kamwe sitasahau jinsi vile machozi yalimdondoka mama yule tulipokuwa tunazungumza na kuomba pamoja.

**Maisha Ya Jamii:** Nakumbuka pia wakati nilipotimia mwaka wangu wa 21. Nchini Uingereza, umri huu

## *Wakati wa Kufichua Siri*

ni umri ulio maalum kabisa. Wakati wa kufikia umri huu huwa wakati wa sherehe. Basi ikawa ni sharti pia sherehe iandaliwe kwa ajili yangu. Iliku wa ni desturi kwamba baada ya mlo huo, kile kilichofoata ni densi kubwa. Lakini nilipofikia umri huu wa miaka 21, tayari Mungu alikua ametoa densi kutoka miguu yangu na kuweka densi hiyo katika moyo wangu. Kwa hivyo nikaamua sherehe ile ya mwaka wangu wa 21 kuwa ni wakati wa kuwaeleza wenzangu kuhusu wokovu. Mimi nilimwalika mwinjilisti kuja katika karamu yangu hiyo. Kadi ya mwaliko niliyowapelekea marafiki wangu wa biashara na wengine ilisema “nina rafiki ambaye atatoa hotuba fupi baada ya karamu. “Wewe mwenyewe, na sio **zawadi** yako ndio inahitajika,” kadi ile ikazidi kueleza. La ajabu ni kwamba usiku huo, mmoja wa marafiki wangu alimkubali Kristo kuwa mwokozi wa maisha yake.

Na baadaye, nilipokuwa naibu wa kasisi katika kanisa moja la kibaptisti mjini London, hakuna hata siku moja ambapo vijana hawakuanda safari ya kutumia mashuwa, au michezo bila kufanya shughuli hizo za kuwavutia wengi ili hata waweze kuwaalika vijana marafiki wao ambao walikuwa hawamjui Mungu. Na kila wakati, shughuli zao hizi zilimalizika na ujumbe maalum wa injili. Vijana wale walijua wazi kwamba jukumu kubwa la ushirika wao ni kujieendezeza katika mambo ya imani yao, na tena kuwasaidia marafiki wao kumjua Kristo. Siajabu kwamba ushirika huu wa vijana ulinawiri kwa ajili ya baraka za Mungu.

## KUZA IMANI YAKO

**Maisha Ya Kiroho:** Sikuwahi kuwa na hamu ya kujifunza mambo ya Biblia mpaka pale nilipopokea wokovu nikiwa kijana wa umri wa miaka 19. Kwa hivyo, niki wa kijana wa umri huu, ni machache sana niliyajua kuhusu Maandiko Matakatifu. Lakini baada ya kumkubali Kristo kuwa Bwana na Mwokozi wa maisha yangu, kila jumatatu jioni, wachache kati yetu wakristo wapya tulikuwa tunakutana pamoja katika nyumba moja tukiwa na kusudi la kusoma na kujifunza kutoka Maandiko Matakatifu. Hamu yetu kuu ilikuwa ni kupata neno la Bwana kuititia vichwa vyetu na baadaye kuelekeza neno hili katika mioyo yetu haraka iwezekanavyo! Hata wakati huo, tuliendeleza masomo yetu ya Biblia tukitumia misingi ambayo tayari nimetaja hapo mbeleni katika kitabu hiki. Hatukuchukulia neno la Bwana kuwa kama kitabu cha dini, ila tulichukua kitabu hiki cha maandiko Matakatifu kuwa kama chombo cha kutuonyesha mahali pa kwenda maishani.

Baada masomo haya ya Biblia, vijana wengine wachache waliweza kupokea wokovu, na tukiwa pamoja tukaweza kubuni njia tofauti kueneza injili. Na kwa vile hakuna hata mmoja kati yetu ambaye alikuwa na gari, basi wazo lilitujia kwamba tunaweza kutengeneza aina ya mkokoteni inayotumia baisikeli kubeba mizigo yetu wakati wa huduma. Mmoja kati yetu ambaye alikuwa na ujuzi wa mambo ya ufundi akaweza kutengeneza chombo cha kupaaaza sauti yaani amplifier, na hata chombo cha kucheza sahani za santuri. Wakati fulani, na sana sana mwisho wa

## *Wakati wa Kufichua Siri*

wiki, tuliweza kuvuta mko koteni nyuma yetu pamoja na chombo cha kupaaaza sauti na kutembelea vijiji viliv yoku wa karibu nasi.

Nakumbuka kijiji kimoja ambako kanisa la kiMethodist lilikuwa limefungwa na mlango wake kuwekwa kufuli. Katika hamu yetu kuu ya kueneza injili, tuliweza kutafuta tukapata funguo zake, na hata tukapewa ruhusa ya kutumia kanisa hilo. Tulipangusa uchafu kutoka viti virefu mule kanisani, na baadaye tukatoka na mkokoteni kwenda kijiji cha Green na mashine ile ya kujitengenezea ya kupaaaza sauti. Inje ya jumba la pombe hapo kijijini, tuliandaa sehemu ya kuhubiri hadharani, tukaanza mkutano wetu kwa kucheza moja ya rekodi iliyokuwa mpya ya mwimbaji mashuhuri sana Beverly Shea. Ilikuwa ni juzi ye ye alikuwa ametembelea uingereza akiwa pamoja na muhubiri ambaye alikuwa wakati huo bado chipukizi katika kazi hii, jina lake Billy Graham. Na kila baada ya wimbo, tulitumia nafasi hiyo kusimama juu ya kijisanduku ambacho kilikuwa mimbara na kushuhudia kuhusu yale Bwana na Mwokozi wetu Yesu alikuwa amefanya katika maisha yetu. Kristo alikuwa ametutendea maishani akiwa Bwana na mwokozi wa maisha yetu. Baada ya hapo, wengine kati yetu walijaribu ku wahubiria wale waliotoka katika jumba hilo la ulevi kuona ni nini kilichokuwa kikiendelea. Na la ajabu ni kwamba, Mungu aliona ni heri ajaze kanisa lile kabla ya mwisho wa wiki hiyo. Mmoja wao baadaye alikuja kuwa mwalimu wa somo la Jumapili alikuja kumjua Kristo, na baada ya

## KUZA IMANI YAKO

hapo dada yake pia akamkubali Kristo. Na baadaye, milango ya kanisa ikawa haifungwi tena. Masomo ya jumapili na ibaada ya jumapili ikaorodheshwa.

Mtume Paulo alimwambia Timotheo hivi: *lihubiri neno, uwe tayari wakati ukufaa na wakati usiokufaa* (2 Tim. 4:2). Kama Mtume Paulo angekuwa anaendeleza huduma yake leo hii, ye ye labda angesema na Timotheo kwa njia hii: “Ukipata nafasi ya kueleza mtu kuhusu neno la Mungu, basi fanya hivyo: na ikiwa hutapata nafasi, wewe mwenyewe jitengeneze nafasi hiyo. Hakuna wakati ambapo si jambo la bu s a ra kuhubiri neneo la Mungu.” Sina shaka Mtume Paulo hangefurahia somo lililo la utaratibu fulani maalum la Biblia ambalo haliwezi kuwasaidia watu na upendo na pia na nguvu kujenga kanisa.

Pale utakapojuja siri kuhusu jinsi ya kuchukua neno la Bwana kutoka kichwa hadi katika moyo wako, utagundua kwamba haitachukua muda mrefu kabla neno la Bwana litakuwa sawa na jinsi vile Nabii Yeremia alivyosema, *moto katika mifupa yako*.

La kuhuzunisha ni kwamba ikiwa neno la Bwana litakaa katika kichwa chako, na lisifike katika moyo wako, basi kuna uwezekano kwamba wewe huenda ukawa mtu aliye na neno tu, na hana Roho Mtakatifu. Hutakuwa na moto kat ika mifupa yako! Lakini unapozidi kukutana na Mungu katika wakati wako wa *kuwa pamoja naye*, utakuja kugundua kwamba ni vigumu sana kuwa mtu aliye na Roho Mtakatifu pasipo neno la Bwana ndani yako!

Ni kweli kabisa Mungu anasema nasi pale tunaposoma neno lake, ye ye anatutaka tuweze



## *Wakati wa Kufichua Siri*

kuwaeleza wenzetu kuhusu hayo. Mungu alimuambia Ezekieli hivi basi, *wewe, miwanadamu, nimekuweka kuwa mlinzi kwa nyumba ya Israeli; basi ulisikie neno hili kinywani mwangu, ukawape maonyo yangu* (*Eze. 33:7*). Hata hivyo hakuna haja kuwaambia wenzetu yale sisi wenyewe hatujayasikia, na kuyaitika, maneno kutoka kinywa chake.

Kuna mawakili wengi wa ‘Ukristo’, la kuhuzunisha ni kwamba wako wachache sana kati ya mawakili hawa ambao wanaweza kutoa ushuhuda wa kweli kwamba wana uhusiano kamili na Mungu aliye hai.

Na baadaye, kutoka kwa yale aliweza kuyapitia, mtume Yohana aliweza kushuhudia kuhusu ukweli wa kuwa na ushirika ulio hai naye Kristo. Kwa hivyo, sawa na jinsi vile tunaweza kutarajia, ye ye aliwaalika wenzake waungane naye katika ushirika huu wa karibu: *hilo tuliloliona na kulisikia, twar wahubiri na ninyi; ili nanyi pia mpate kushirikiana nasi na ushirika wetu ni pamoja na Baba, na pamoja na Mwana wake Yesu Kristo* (*1 Yoh. 1:3*).

## **Ichunguze Roho Yako**

1. Je, natambua na kujua kwamba mahali ninapoishi, na mahali pangu pa kazi ni mahali ambapo nahitajika kueneza injili?
2. Je, mimi nawaona watu walio karibu nami kuwa watu ambao waaweza wakabadilishwa na kuwa na imani, ama mimi nawaombea n aupendo ili waweze kuja kwake Kristo?
3. Ni wakati gani wa amwisho niliwahi kupata nafasi ya kushuhudia pale nilipomsaidia yule ambaye kwa kweli alikuwa yuko katika hali ya kuhitaji msaada kutoka kwangu?
4. Je, kinywa changu kimefungwa kusema lolote linalohusu Kristo kwa ajili ya:  
Maisha yangu amekubali kuwa na dhambi- kazi yangu yaweza kuharibika  
kiburi changu na majivuno hayanikubalii kushiriki naye Kristo Mnazareti aliyedharauli wana kufanyiwa dhihaka.





### **Mwanga Wa Milele**

*Mwanga wa milele! Mwanga wa milele!  
Usafi wa jinsi gani unahitaji katika mioyo yetu,  
Pale, tunawekwa katika sehemu inayofikiwa na mwanga  
wako  
Hujikunja, kwa ajili ya furaha  
Yaweza kuishi na kuyaelekeza macho kwako!*

*Roho wanaozingira kiti cha enzi yako  
Waweza kubeba uzuri ulio kama moto;  
Lakini hayo ni yao tu  
Kwa vile hawajawahi kujua ulimwengu wa dhambi  
kama huu.*

*Je, itakuwaje, mimi ambaye mako yangu ya asili  
yametandaa na giza, na mawazo yake hafifu,  
Kabla hajajitokeza,  
na kwa roho wangu hafifu amulike nuru yake.*

*Kuna njia ya mwanadamu,  
kufikia pale makao ya juu:  
Na hapa kuwa zawadi na...  
Nguvu ya roho mtakatifu  
ambaye ni wakili mbele ya Mungu.*

*Haya yanatuandaa tuweze kuona  
utukufu ulio juu:  
Ili watoto wasio na akili na waishio katika giza  
Waweze kuishi katika mwanga,  
kupitia mapenzi ya milele!  
Thomas Binney (1798-1874)*

## *Tunda au Moto*

Rafiki yangu mmoja kwa jina Bengt kutoka nchi ya Sweden amehamia Marekani. Na huko akawa mfanyi biashara ambaye ameendelea sana katika kazi yake hii. Moja ya huduma ambazo alikuwa anaendeleza ilikuwa ile ya kutumia ndege kuwasafirisha wamishonari kwenda kufa nya kazi ya kueneza injili. Siku moja, yeye na rafiki yake walipata kazi na shirika la Mission Aviation Fellowship (MAF) wapeleke ndege moja hadi Alaska. Baada ya kukamilisha sehemu kubwa ya safari yao, Bengt aliachana na rafiki yake katika uwanja wa ndege wa Fairbanks. Hapa yeye akajiandaa kuendelea na safari fupi iliyobaki akiwa rubani wa ndege ile peke yake.

Na kabla hajaondoka, rafiki wake Bengt yule alimtupia kijifuko kidogo ambacho kilikuwa na vifaa vya kutumiwa wakati wa dharura katika ndege hiyo. Katika mfuko huo, kulikuwa na chocolate na blanketi. Akiwa katika sehemu ya mwisho ya safari hiyo, mvua kubwa ilianza kunyesha ghafla. Upepo mkali wa huko Alaska ulifa nya ndege hiyo ndogo ianze kuyumbayumba na kuvurutwa kuelekea chini.

## KUZA IMANI YAKO

Baada ya kupinduka, ndege ile ilisimama karibu na kilele cha mlima. Kwa muda wa siku tatu, theluji kubwa ilianguka, na kupitia maajabu ya Mungu, theluji ile ilitolewa kutoka sehemu hii ya chini ya ndege hiyo na upepo mkali, na hapo kufanya ndege ile isifichwe na theluji hiyo. Lakini kwa vile kulikuwa na theluji kubwa sana karibu na ndege hiyo, pale askari wa Coastguard walipokuwa wanaitafuta kutoka juu angani, wao hawakuweza kuona ndege hiyo.

Baada ya askari hao kuacha kazi hiyo ya kumtafuta kutoka hewani, mwanawewe Bengt kwa jina Bruce, pamoja na mwenzake ambaye alikuwa rubani wa shirika hili la MAF, walikuja pamoja na wakamsihi Mungu awaonyeshe mahali Bengt alikuwa yuko. Bruce alikuwa kijana chipukizi mwenye imani. Na pale Bruce alikuwa anafanya haya Bengt alikuwa ameanza kupungukiwa na nguvu, na hata akawa amechukua picha ya pole pole iliyoonyesha akiwapungukia mkono jamii yake. Haya yote aliya fanya kuwa kitendo chake chamwisho kabla hajaaga dunia. Macho yake yalikuwa makavu, yenyenye unyonge na yasiyo na nguvu; lakini uso wake ulionyesha ishara ya kuwa na tabasamu ya furaha. Hata hivyo, mipango ya Mungu ilikuwa ni tofauti kabisa. Pale Bruce na mwenzake walipokuwa wanapaa juu ya ndege ya Bengt wakimtafuta, miyale ya jua kutoka ndege hii ilikuwa inarushwa juu, wakaona miyale hiyo, na hapo wakawa wamepata fununu kuhusu pale alipokuwa yuko huyu mpendwa wao.

Ni kwa nini nataja kisa hiki? Ni kwa sababu, baadaye, Bengt aliniambia kwamba kwa muda wa

## *Tunda Au Moto*

siku kumi alipokuwa yuko pale, yeye alikuwa yuko karibu kabisa na kiti cha hukumu cha mwokozi wetu Kristo. Nilipokutana na yeye tena, aliniambia kwamba alipokuwa pale amekwama akiwa peke yake mlima ule wenyе theluji, Roho Mtakatifu alimpatia nafasi aweze kuyapitia matukio yote katika maisha yake hapa duniani pale alipokuwa anangoja kuitwa kupitia kifo kwenda juu mbinguni kuwa karibu Mungu. Alisema kwamba kwake ni kama kiti cha kuhukumiwa wenyе imani kilikuwa kimeletwa karibu naye mapema kuliko vile ilivyostahili. Bengt alianza kuwaza kuhusu miaka yake ya huduma ya kiKristo, na hakujuua ni kiasi gani cha huduma hii yake itatiliwa maanani katika maisha ya milele.

Akiwa anatilia mkazo kila neno alililokuwa akitamka, Bengt aliniambia akiwa katika hali ile ya wasi wasi, yeye aligundua kwamba mikutano ile yote ya kanisa, mikutano ya mabaraza ya wamishonari, na mambo mengi ya kanisa ambayo yeye alikuwa amejihuisha nayo - ingawa haya yote alikuwa ameyafanya na furaha na moyo wa kujitolea, yeye alikuwa amefanya haya akitumia nguvu zake na kulingana na vipawa vyake mwenyewe. Yote haya aliyafanya na uwezo wake na hakufanya hayo yote kwa ajili ya Roho Mtakatifu kujaa ndani yake na kufurika hadi kuonekana katika matendo hayo yote.

Bengt aliniambia katika siku kumi hizo, Mungu alikuwa amemwonyesha kwamba matendo haya mema ni kama kuni, nyasi na uchafu wa shambani, huu ukiwa mfano wa yale katika maisha yetu ambayo yatakusanywa jinsi vile Maandiko Matakatifu

## KUZA IMANI YAKO

yanavyosema, na kuchomwa mbele ya kiti cha hukumu, kwa hivyo ni mambo yasiyo ya muhimu katika maisha ya milele.

Yale yaliyomkumba Bengt yalikuwa sawa na ufufuo katika maisha yake. Wengi wetu ambao tulikuwa tunamjua hapo mbeleni na kumpenda kwa ajili ya wema wa matendo yake katika huduma ya Bwana kwa vile katika maisha yake ya baadaye, na katika miaka iliofuata, yeye alijitoa kumhudumia Bwanana nguvu mpya, na haya yote yakajitokeza kuwa baraka kuu. Nguvu ya Roho Mtakatfu alijitokeza wazi kila mahali alikoshuhudia.

Ni jambo la kumwamsha kila Mkristo kukumbuka kwamba siku ile ya hukumu, tutaenda mbele ya kiti cha hukumu tukiwa tayari kwa ajili ya **wote walio na imani**. Kiti hiki ni tofauti na kile kiti maalum cheupe cha hukumu. Kiti hiki maalum cheupe ni kiti ambacho **wale ambao hawana imani** watasimama yake siku ya kuhukumiwa. Na hapa wao watahuku miwa na kupelekwa mahali pa kupotea milele. Kiti kile cha hukumu ni mahali ambapo wale walio na imani watasimama kuhukumiwa, ambapo kila kitu kisicho cha imani kitacho m wa ,na kile cha imani kitastaw i s h wa ili kiwe cha kutukuza Mungu milele kwa sababu yeye mwenyewe amefanya kazi hiyo! Siku hiyo, wakristo wengi watakuja kugundua kwamba hata kazi ile wamefanya kanisani, na sifa yao katika huduma kanisani, sifa ambayo imewafurahisha maishani - haya yote na mambo ambayo kwake Mungu sio huduma kamili ya kiroho.



## Tunda Au Moto

### **Kurasa Nyeupe**

Mbele yangu nina karatasi safi nyeupe mbili. Karatasi hizi hazina alama yejote. Uki ziangalia, hutaona chochote. Maandishi wala michoro haione kani. Ukitazama vyema karatasi hizi, hutaona mawazo ya mtu wowote yakiwa yameandikwa katika karatasi zenyewe ama picha maridadi. Na tena, hutaona kosa la mtu yejote kwenye karatasi hizi! Sawa na jinsi vile hakuna chochote ambacho ni cha umaridadi katika karatasi hizi, hakuna pia chochote ambacho ni uchafu katika karatasi hizi. **Karatasi zenyewe nyeupe; hakuna kingine.**

Maisha yako na yangu yanaweza kuwa na siku nyingi ambazo ni kama karatasi nyeupe. Ingawa kuna wakati kulikuwa na uchafu wa dhambi; sasa, na kwa ajili ya utukufu na rehema zake Mungu, na kwa ajili ya damu ile iondayo dhambi, damu yake Kristo, kila ukurasa katika maisha ya Mkristo umesafishwa. Hakuna chochote ambacho kimebaki isipokuwa kile ambacho ni cheupe *kama theluji* (*Isa. 1:18*). Ninapotazama nyuma katika baadhi ya kurasa za maisha yangu ya Ukristo, nakumbuka na huzuni jinsi vile kwa kukusudia na bila kukusudia; kwa kujua au kutojua, kwa kuwa na unyonge nimeweza kutenda dhambi nyingi na kumhuzunisha Roho Mtakatifu. Kama asingekuwa Kristo, basi kurasa zile zingekuwa na uchafu wa dhambi na kujipenda. Ni msamaha wa ajabu, utukufu na upendo usio na kifani ambao Mungu ameelekeza kwango hivi kwamba hata kurasa hizo chafu sasa ni safi na nyeupe kama theluji!



## KUZA IMANI YAKO

### **Kurasa ina weupe; lakini msifu Mungu kwamba hakuna uchafu.**

Ni jambo linalostahili kutiliwa maanani kwamba kile ambacho Roho Mtakatifu **hajafanya** kupitia kwangu, yeze hahesabu kitu kama hiki kuwa katika maisha ya milele. Kulingana na yale Mtume Paulo alisema, siku hizo katika maisha yangu ni kama yeze *mwenyewe ataoolewa; lakini ni kama kwa moto* (*1 Kor. 3:15*). Pale ambapo Roho Mtakatifu hajafurika katika maisha yangu, na ingawa dhambi zangu zimefutwa na Mungu aliye mwingi rehema, hakuna chochote kimetimizwa ambacho kitahesabiwa katika maisha ya milele. **Kurasa nyeupe, na la kusikitisha kurasa isio na chochote!**

Ingawa kurasa fulani katika maisha daima zitabaki nyeupe, kuna kurasa ambazo daima zitakuwa na vitu vimeandikwa juu yake, vitu vilivyo na umaridadi na vimeandikwa na kuchorwa na mikono yake iliyoandikwa na kuchorwa na mikono ile ambayo ilichomwa na misumari - na hapo kumtukuza milele. Kwa kila mwenye imani, kurasa hizi maalum ni kurasa ambazo zina ujumbe unaohusu siku zile tumekuwa vyombo ambavyo Mungu wa milele ametumia kufanya kazi yake inayodumu milele. **Ndio, kurasa nyeupe, lakini msifu Mungu, kuna mengi zaidi!**

### *Miaka Ya Hasara*

Ni jambo la kuhuzunisha sana kwamba wako wale ambao wamealikwa na Mungu kuja “mezani” nao, wanaharibu miaka mingi ya maisha yao kwa mambo



## *Tunda Au Moto*

mengine badala ya kukuza na kuendeleza uhusiano kati yao na Mungu ili afurahi.

Moyo wangu hujaa furaha pamoja na huzuni pale ninapokumbuka mzee mmoja ambaye wokovu alioupokea ulikuwa ni wokovu wa huzuni kwa ajili ya nafasi nyingi ambazo zimlimpita akitumia wakati wake katika raha nyingi maishani. Baada yangu kumkubali Kristo maishani, tukiwa na vijana wenzangu ambaao wao pia walikuwa wamekuja kumjua Kristo, tulienda katika hospitali moja tukiwa na lengo la kuhubiri huko. Mara moja baada ya wiki mbili hivi, kila jumamosi, tuliwatembelea wagonjwa ambaao walikuwa ni wazee waliokosa tumaini la kuweza kutoka hospitalini. Jioni moja, nilimkaribia mzee mmoja kitandani, ambaye ilikuwa wazi kwamba ataaga dunia kabla hatujaweza kuwatembelea tena.

Baada ya kusikiliza kwa makini ujumbe wetu mfupi kutoka Biblia, kwa kweli ye ye aliguswa sana na neno lile. Na huku machozi yakimdondok a, ye ye alisema hivi: “Najua kwamba nimeokolewa na naenda juu mbinguni.” “Hilo ni jambo zuri mno!” nikamjibu mara moja. Na kabla sijasema lolote kuongezea hayo, mzee yule alianza kulia na uchungu sana, na sio kwa ajili ya furaha, lakini kwa ajili ya uchungu wa ndani kabisa. Kwa sauti ya chini na ya unyonge, akasema: “Niko na umri wa miaka 71, na miaka 70 imeenda hasara!”

Nikiwa mchanga katika imani, ningewezaje kumjibu Mzee huyu? Siwezi kukumbuka jinsi vile nilivyo jaribu kumtia moyo, lakini nakumbuka jinsi vile nilivyorudi nyumbani jioni hiyo, nikapiga magoti

## KUZA IMANI YAKO

nakumwambia Mungu maneno haya: "Mungu, hata sasa naangalia katika siku za baadaye, siku ambayo nitaikumbuka. Itakapofika wakati wangu kuja mbinguni, sitaki kuja huko na roho yangu iliopokea wokovu, lakini na maisha ambayo yamekuwa ni ya hasara. Usiku wa leo, nayweka maisha yangu katika mikono yako. Naomba kwamba utafanya maisha haya yawe ya faida hata milele."

Katika Agano la Kale, Habakuki alionya kwamba kuna uwezekano wa kutumia kiasi kikubwa cha nguvu, na baadaye ugundue na huzuni kwamba hujafanya lolote! Na ye ye aliwajulisha watu wa enzi hiyo, *lakini mwenye haki ataishi kwa imani yake* (*Hab. 2:4*). Pia aliwaonya kwamba wale ambao hawatatumia nguzo kuu ile ya imani kwamba wamtegemee Mungu katika kila jambo, *kazi zao, hayo wayafanyayo wanashugulikia moto* (*Hab. 2:13*). Kwa ajili hao watu walijenga mji wao bila kumtegemea Mungu na kile ambacho kilibaki kilikuwa tu ni majivu. Sawa na haya, kila jambo tufanyalo pasipo kumtegemea Mungu katika kila hali, hayo yote yatakuja kuchomwa siku moja.

Na katika Agano Jipy, Mtume Paulo naye anatuonya hivi:

*Lakini kama mtu akijenga juu ya msingi huo, dhahabu au fedha au mawe ya thamani, au miti au majani au manyasi, kazi ya kila mtu itakuwa dhahiri. Maana siku ile itaidhahirisha. Kwa kuwa yafunuliwa katika moto; na ule moto wenyewe*



## *Tunda Au Moto*

*utaijaribu kazi ya kila mtu, ni ya namna gani. Kazi ya mtu aliyoijenga juu yake ikikaa, atapata thawabu. Kazi ya mtu ikiteketea, atapata hasara; ila ye ye mwenyewe ataokolewa; lakini ni kama kwa moto (1 Kor. 3:12-15).*

Yule mzee mwenye umri wa miaka 71 alikuwa na furaha kwa ajili ya kupokea wokovu. Na pia alikuwa na huzuni kwamba wokovu huu alikuwa ameupokea kupidia moto. Moto ambao utachoma mti, nyasi na hata uchafu wa shambani, ambao ni sawa na maisha yake; na moto huu utasafisha dhahabu, fedha na mawe yenye thamani ambayo Roho Mtakatifu ametumia pamoja na mawe maalum ambayo Mungu hutumia katika kazi ya ujenzi.

### *Mwanga Wa Milele*

Mungu wa milele atafanya kazi yake ya milele kupidia Mkristo ambaye yuko ndani ya Kristo, anaendeleza na kustawisha imani yake, na kutumia neno la Mungu katika hali tofauti maishani. Walio na imani kama hawa wanawenza kuamka kila siku wakijua kwamba basi *kwa kuwa tunapokea usalme usioweza kutetemeshwa, na mwe na neema, ambayo kwa hiyo tumtolee Mungu ibada ya kumpendeza, pamoja na unyenyekevu na kicho* (Ebr. 12:28). Wakati wa kuwa *pamoja na Mungu* utakutia moyo kutembea katika nguvu za Roho Mtakatifu, na sio kupitia nguvu zako.

Siku moja, katika mwanga unaoangaza kila upande, mwanga utokao kwa Mungu; wale ambao wamekuwa wakijiweka tayari na kuendeleza huduma



## KUZA IMANI YAKO

ya Mungu aliye hai watakuwa na furaha kuu. Ni kweli kila mara tunapokuja mbele ya meza ya chakula cha kiroho, Mungu mwenye mwanga na upendo anatualika tumkaribie na kushiriki naye bila kufi cha lolote. Ni kupitia hali hiyo tutaweza kuwa vyombo vyenye mwanga na upendo katika dunia hii iliotanda giza la uchoyo.



## **Ichunguze Roho Yako**

1. Nikiendelea kuishi jinsi vile ninavyoishi hivi sasa, je kutakuwa na matunda kutoka maisha yangu pale katika kiti cha hukumu cha Kristo?
2. Pale ninapoomba, je, mimi humkaribia Mungu kama mwanga wa wa milele, au mimi humuona kuwa msaada wangu kutoka juu mbinguni?
3. Je, kuna haja mimi kuomba ombi sawa na lile la Mfalme Daudi: *Unihuishe sawasawa na neno lako* (Zab. 119:25).



*Nigawie Mungu,  
Mkate wa maisha,  
Sawa na jinsi vile  
Ulivyo mega mikate  
kando ya bahari;  
Hata mbele ya kurasa takatifu  
Nakutafuta wewe, Mungu  
Roho yangu ina hamu ya kukupokea  
kupokea neno lako lililo hai.*

*Wewe ndiye mkate wa uhai  
mkate wangu wa uhau;  
Neno lako takatifu ni la ukweli  
ukweli ambaa umeniokoa  
Nipe nikule kama chakula ili niwe hai  
Niwe hai na kuishi pamoja nawe kule uliko  
Nifunze kupenda ukweli wako,  
kwa vile ni wewe mwenye upendo.*

*Tuma Roho wako Mtakatifu,  
Mtume aje kwangu,  
Ili roho huyu aguse macho yangu  
nami niweze kuona;  
Nionyeshe ukweli niweze kuuona  
Nionyeshe ukweli ambaa umejificha  
katika neno lako,  
na kufichuliwa katika Maandiko yako  
ambapo mimi namwona Mungu.  
Mary Ann Lathbury*

# Karibu Mezani!

**K**atika ufuo uliojaa mchanga wa ziwa Galilaya, Kalisimama Mwana wa Mungu aliyefufuka, akiwa peke yake. Pia alikuwa hajulikani. Labda ni ukungu wa asubuhi ndio ulifanya utukufu wake usionekane na wafuasi wake ambao walikuwa na uchovu mwingi wasiweze kumuona. Au labda ni macho yao ya kiroho ambayo yalikuwa yameshikwa na giza kuu lilitokana na matukio yale ya kusulibiwa na baadaye kufa pale msalabani.

Karibu na hapo, wafuasi wake wakiwa wamekufa moyo walijikusanya pamoja katika mtumbwi mdogo wa kuvua samaki. Walikuwa wamekesha usiku wote wakijaribu kuvua samaki, nao hawakuwa wamefanikiwa kupata chochote. Sawa na kuwadharau, akawauliza, *watoto, mna chakula chochote?* Na baadaye kutoka kwa kinywa cha yule aliyejewa kwenye ufuo huo, kukatokea amri: *wekeni nyavu kwenye mkono wa kulia wa mtumbwi, nanyi mtapata kitu.*

Baada ya kuamka kutoka usingizini, Yohana alijibu sauti hiyo ya ambayo ilikuwa ni sauti aliyozoea

## KUZA IMANI YAKO

na hamu na furaha, akisema: “*Huyu ni Bwana!*” Wakiwa wametiwa moyo upya, wafiasi wake hawa walifanya jinsi vile walikuwa wameagizwa. Baada ya nuda mfupi, nyavu yao ikajaa samaki! Akiwa amejawa na furaha, Petro aliruka ndani ya maji, akaanza kupiga mbizi kuelekea kule Bwana alikuwa yuko. (Yn. 21:11).

Katika ufuuo huo, yeye mwenyewe, Bwana wa Utukufu alikuwa amewasha moto. Na pale wafiasi wake wote walipokuwa wamejikusanya hapo, yeye akaomba na kupewa samaki, naye akaandaa mlo murua. Kwa hao waliokuwa na njaa, na furaha, yeye akawapa mwaliko: *njooni mfungue kinywa* (Yn. 21:12).

Ni mwaliko huu ulio na utukufu bado unasiika hata hivi leo baada ya karibu miaka elfu mbili. Asubuhi baada ya asubuhi Yesu ambaye ni Bwana yungali anaturalika kwenye meza tushiriki pamoja mezani katika mlo ambaao ameanda kwa makini sana. Ni kweli kabisa: ni yeye mwenyewe Bwana na Mwokozi wetu ambaye ameanda chakula hiki. Ni chakula cha Kiroho cha kutujenga na kutuhifadhi. Chakula hiki ni neno la Bwana, nalo lapatikana katika Maandiko Matakatifu - Biblia.

Baada ya muda mfupi, nitakualika ukaribie na usikilize pale nitakaporudia neno wakati wangu *kuwa pamoja na Mungu*. Naandika ombi **hili langu hili** kwa ajili huenda ombi hili likakutia moyo, na kuwa la msaada kwa ko na kukusaidia kuitikia mwaliko wa Bwana kuja na kula naye. Kutoka sehemu mbili ambazo ni tofauti sana, nimeamua kujihusisha katika wakati wa *Kuwa Pamoja na Mungu*, tukiwa nawe.

## *Karibu Mezani*

Sababu zinazonifanya niamue kushiriki nawe katika sehemu hii ya Kuwa Pamoja na Mungu ni:

**Kwanza:** Rafiki yangu mmoja ambaye alisoma kurasa za hapo mwanzo katika kitabu hiki alinisihi nifanye hivyo kama njia moja ya kukamilisha kazi hii.

**Pili:** Kwa muda wa miaka mingi, nimebahatika kushuhudia kuhusu jinsi vile Mungu amewabariki watu mbali mbali kwa njia maalum sana pale nimeongoza vikundi mbali mbali makanisani katika shughuli ya *kuwa pamoja na Mungu* katika vikundi.

Wakati kama huu, yejote ambaye yuko mkutanoni anaweza kushiriki, hakuna akiyekubali kuuliza swal pasipo pale wakati wa maombi ya kisiri kwake Roho Mtakatifu; na pia hakuna mahuburi yalikubaliwa. Tulianza kila ushirika na maombi kwamba Roho Mtakatifu ndiyе atakayekuwa mwalimu wetu. Na kwa pamoja, sote tukasoma sehemu maalum ya Maandiko Matakatifu ambayo imechaguliwa kwa pamoja. Baada ya hapo tulikuwa tunarudi tena katika sehemu ya kwanza ya somo letu, na hapa tena kusoma kwa pamoja sehemu hiyo kwa sauti ya juu. Kabla hatujaelekeea katika ukurasa unaofuata, tulikuwa na wakati wa sekunde 30 kupumzika. Wakati kama huu kila mmoja wetu alihitajika kuwaza kwa undani na kimaombi kuhusu yote ambayo tulikuwa tumeyasoma na kuangalia kuona kama swal lolote ambalo tulikuwa tumelianda hapa lilikuwa ni la maana na la muhimu, na kama swal lenyewe ambalo

## KUZA IMANI YAKO

la patikana baada ya ukurasa huo laweza kujibiwa baada ya kusoma sehemu iliyotajwa ya Maandiko Matakatifu. Baada ya muda ule wa maombi na kutafakari, kila mshiriki alipata nafasi ya kueleza washiriki yale ambayo Roho Mtakatifu alikuwa ameshirikisha ndani ya moyo wa mshiriki. Na haya yalikuwa yanafuatwa na maombi ya kuitikia kutoka kwa yule ambaye ameongoza wakati huo ama kutoka kwa yeote aliye mshiriki wa mkutano huo.

**Mimi naamini kwamba njia hii ya kuendeleza somo la Biblia lisilo rasmi ndio njia iliyo bora na ya kufaidi washiriki. Wakati huu, nachukua anafasi hii kuwasih i wasomaji ambao wanatumia kitabu hiki katika kikundi, kutenga kando mikutano kadha na kusudi la kujaribu kutumia njia ambazo tumetaja katika masomo yao. (Kwa ajili ya kukusaidia, maswali zaidi yanapatikana pale mwisho wa kitabu hiki.)**

Wazo la kuwa na wakati wa *pamoja na Mungu* katika kikundi nililipata mara ya kwanza kupitia Mchungaji Marehemu Thomas B. Rees, ambaye alikuwa mwinjiliisti kutoka Uingereza katika mkutano wa Young People's Holiday Conference Centre. Ni katika mkutano huu nilimkubali Kristo maishani. Ma swali ambayo Tom alituuliza tukayajibu yalikuwa sawa na yale ambayo nimetaja katika ukurasa ulio na kichwa: *Kuwa Pamoja Na Mungu*.

Kwa muda wa miaka mingi tangu wakati huo, mikutano ambayo nimeendesha kwa njia hii imekuwa

## *Karibu Mezani*

ni mikutano ambayo uweza wa Bwana umejitokeza, na Roho Mtakatifu kufanya kazi ya kunena na roho za watu na katika maisha yao. Baada ya mikutano kama huu katika kanisa la Baptist, Victoria nchini Canada, mchungaji wa hapo alisema hivi: “Huo ndio umekuwa mikutano wa baraka kuu, na wa ajabu ambao nimewahi kuhudhuria tangu nianze kazi ya huduma ya Mungu.”

Baada ya siku kadha katika kanisa la Christian and Missionary Alliance, huduma kwa waarabu katika mji wa kale wa Jerusalem, (na katika wakati huo, nilitumia siku kadha kuwafunza waumini juu ya mambo haya na pia kuendeleza mikutano ya vikundi ya kuwa Pamoja Na Mungu.) Yule mkuu wa chuo ca Biblia nchini Canada ambaye wakati huo alikuwa akiishi katika mji huo wa kale wa Yerusalem alisema hivi: “Hatujawahi kuwa karibu na ufufuo wa kiroho jinsi hii hapa mjini Yerusalem!”

Katika mikutano ya kanisa, mikutano ya somo la Biblia nyumbani, na mikutano ya vijana; Mungu amebariki watu wake, kupitia njia yao ya kuelewa neno la Bwana.

Ningependa kutaja hapa kwamba hata ninapajaribu kuandika kuhusu wakati wangu wa kuwa pamoja na Mungu, nimegundua kwamba ni vigumu kushika kabisa ukweli, uzuri na hata roho ya kupanuka kimawazo katika kusoma, kuliko kwa njia ya binafsi na hata katika mikutano ya hadhara.

Ili niweze kukuandikia yale yaliyo ya muhimu kutoka kwa wakati wetu wa kuwa Pamoja na Mungu, mimi nimejiwekea sheria hizi:

## KUZA IMANI YAKO

**Kwanza:** Sitachagua sehemu ya Maandiko Matakatifu ambayo mwenyewe naielewa! Katika wakati wangu wa kuwa pamoja na Mungu kila siku. Hivi sasa nasoma waraka wa Pili wa Petro kwa Wakorintho.

**Pili:** Haya ambayo nimeyaandika kuhusu sehemu ya Maandiko Matakatifu si maneno ya kueleza kwa undanii Maandishi haya Matakatifu.

**Tatu:** Ili yale ambayo nimeandika kuhusu Kuwa Pamoja Na Mungu yaonekane kuwa maneno yasio ya ajabu, na kwamba ni ya kawaida, nishiriki nawe kutoka maandishi matakatifu ni mistari ambayo Roho Mtakatifu mwenyewe amenifunulia na kuweka hai katika moyo wangu.

**Nne:** Nitakueleza jinsi vile Roho wa Bwana aliwekwa wazi kwangu pale kuitia njia ya maombi nilipo tafakari kuhusu neno la Bwana nikitumia baadhi ya maswali ambayo yametajwa.

Ninapotaja yale ambayo nimetasfakari juu yake, utaelewa kwamba wakati wote wa *kuwa Pamoja na Mungu*, ni wakati wako binafsi; wewe na Mungu. Sina shaka kwamba hali yako wakati huu ni tofauti na hali yangu. Pia naelewa kwamba hali ya mambo wakati huu huenda ikawa tofauti sana na hali ya mambo baada ya miezi sita. Na kwa ajili ya upendo wake mkuu, Mungu hukutana nasi, na kusema nasi pale ambapo tuko, wakati ule ambao tunamhitaji; na sio mahali tutakuwa ama wakati wa hali ya mambo yatakayotujia. Mungu hukutana nasi, na kusema

## *Karibu Mezani*

nasi pale ambapo tuko wakati huo. Pale unapokuwa ukisoma haya yalioko mbele yako hivi sasa, huenda hali yako ikawa tofauti sana na hali yangu. Kwa vile Mungu husema nawe ukiwa katika hali yako binafsi na pia ukiwa na haja ambazo ni zako, wewe umepewa mwaliko ambao ni wako kutoka kwake Mungu. Karibia meza yake upate kula.

Kwa kweli, Biblia ni neno la Mungu ambalo liko **hai** na lenye **nguvu** katika mioyo yetu. Biblia ni neno lake Mungu kwetu sisi: kila mmoja wetu. *Maana Neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo* (*Ebr. 4:12*). Je, ni jambo gani ambalo laweza kuwa kuu na linalohusu nafsi yako kuliko hili?

Katika wakati wangu wa kutafa kari maandiko matakatifu siku ya leo, nasoma kutoka Wakorintho wa pili, kifungu cha pili, msitari wa kwanza.

**Ni saa kumi na moja asubuhi, nimefunga mlango wa chumba changu ili niwe na wakati wa Kuwa Pamoja Na Mungu.**

Baadhi mambo yanayohusu maisha yangu siku ya leo ninapokuja mbele ya Mungu nikiwa nimefungua Biblia yangu, na moyo wangu ukiwa wazi ni:

- Nimetiya huzuni sana na maumivu ambayo yamekuwa yakimsumbua Dorothy. Maumivu haya yamekuwa yakiongezeka siku baada ya



## KUZA IMANI YAKO

siku, uchungu wake umezidi katika muda wa wiki chache ambazo zimepita.

- Nina waza na kujiuliza kama huenda maumivu ambayo Dorothy anayo yatatulazimisha kubadili mipango tulio nayo ya huduma wakati huu. Hapo mbeleni, pale nimemuona Dorothy akisumbuliwa na maumivu haya wakati tunapokuwa katika safari ndefu kwenda kueneza injili ya kristo. Nami nimewahi kumuambia hivi wakati kama huo: “Kamwe sitakuacha utaabike kwa njia hii tena.” Hata hivyo, kupitia njia moja ama nyingine, Mungu ametu mimina na baraka zake kwa huduma yetu ya pamoja: na kwa pamoja tumesema, “limekuwa jambo la utukufu kwamba tumeyafanya haya.” Na je wakati huu mambo yatakuaje?
- Na jingine ambalo lajitokeza wazi katika moyo wangu lahusu hali ya mambo humu nchini. Mungu ameweza kubariki huduma yetu hapa katika siku ambazo zimepita. Hali ya mambo katika nchi hii huwa niya kutatanisha, gharama ya maisha imepanda sana. Tungependa tufanye mambo fulani zaidi kuwasaidia wenzetu wanaohudumu humu nchini.
- Wako wale katika familia zetu - upande wa Dorothy, na pia upande wangu ambao



## *Karibu Mezani*

wameondokewa na wapendwa. Pia wako wale ambao wanaugua maradhi ambayo hayana tiba. Na kwa ajili ya ratiba zetu katika huduma, ratiba ambazo ni ngumu, na hatuna mpangilio ulio rasmi wa kufuata, na kwa ajili maumivu makali ambayo hujitokeza mara kwa mara humsumbuu Dorothy, hali hii ya mambo imefanya kuwa ni vigumu kuweza kuwaeleza na kuonekana kwamba tunawajali hawa wapendwa wetu.

### ***Ombi***

*Baba, nakushukuru sana siku ya leo kwa ajili ya kuniamsha mapema. Najua lengo lako sio kwamba niweze kuwa pamoja nawe tu. Najua lengo lako ni kuwabariki hata wale ambao watanisikiliza wakati wa kushiriki pamoja nao neno lako siku ya leo.*

*Mungu unajua kwamba ni jambo gumu kwangu kuweka wale watakaosoma maandishi haya nje yafahamu zangu ili niweze kukufikiria tu wewe. Kwa hivyo, naomba kwa njia iliyo ya pekee ipake roho yangu, mawazo yangu na hata kalamu nitakayotumia mafuta ili niweze kuwa na wakati wa upendo mkuu nawe.*

*Na sisitiza tena mbele yako kwamba maisha yangu nimeyaficha ndani ya Kristo kwako Mungu. Ahsante sana kwa ajili ya hakikisho hili la ajabu. Nakushukuru sana pia kwamba ingawa yale ambayo nayaandika nikiwa hapa duniani huenda*

## KUZA IMANI YAKO

*yakawa yamejaa na maoni yangu ya kiutu, mbinguni wewe ndiye kuhani mkuu, na utapeana maombi yangu na sifa ninatoa kwake Mungu kulingana na ujuzi wako na nia yako. Kwa hivyo nikiwa natazimia na upendo, na rudi kwa neno lako asubuhi ya leo. Yafungue macho yangu siku ya leo ili niweze kuona maajabu yako hapa duniani.*

Mpendwa, siku ya leo narudi katika Wakorintho wa pili, kifungu cha kwanza, msitari wa kwanza kuendelea, na nasoma pole pole na kwa sauti ya juu kifungu chote. Nasoma haya yote na sauti ya juu ambayo inasikika vyema, bila kusitasita kwa muda. Nakualika fanya hivyo pia.

Niliposoma kifungu hiki kwa njia hii hapo mwanzo ni, niliweza kuona wazi jinsi vile Mtume Paulo alivyo kuwa na mwenendo bora akiwa mtumishi wa Bwana. Sasa ni wazi kwangu kwamba wakati mkubwa katika saa hii yangu ya Kuwa Pamoja Na Mungu utatumwiwa kujibu swalii hili: **Je, kuna sehemu katika msitari huu ambayo nastahili kutilia maanani?**

Baada ya kusoma kifungu hiki chote cha maandishi matakatifu, tayari moyo wangu umegeuzwa na Roho Mtakatifu na mfano wake Mtume Paulo. Nina hamu ya kuwa mtumishi bora wa wake Mungu Kabla sijaanza kutafakari msitari baada ya msitari katika kifungu hiki, lazima nimuambie haya.

### *Ombi*

*Mungu wangu, nina hamu kuu ya kutaka kuwa na uwezo wa kutafakari kuhusu maisha yangu*

## *Karibu Mezani*

*nikiwa mhudumu wako; na nitosheke sawa na jinsi vile Mtume Paulo ametosheka katika ushuhuda huu wake hapa katika maandishi matakatifu haya ambayo nimeyasoma. Kwa njia elfu moja, wewe umenimimi na na baraka. Ni jambo la kunihuzunisha sana kwamba kila mara, haya yote yametoka kwako kuja kwangu: njia imekuwa ni moja. Moyo wangu unachoka ninapokusihi kila mara kwamba unipe nafasi nishiriki pamoja nawe; na pale unaponipa nafasi ya kushirii nawe katika mateso yako, naogopa. Ninapojiandaa kutafakari kuhusu maandiko haya matakatifu, nijaze na uweza wako na nguvu zako ziniguze kwa njia ilio mpya kabisa ili tabia yangu mbaya ya uchoyo ibadilishwe kwa ajili ya jina lako zuri.*

Sasa nitarudia Maandiko Matakatifu, na kusoma kifungu kile msitari baada ya msitari, na kutafakari wazo baada ya wazo. Ninapofanya hivyo, nitaendelea kuomba kwamba Roho Mtakatifu aniwezeshe nisikose sehemu yejote ya ujumbe amba Mungu anataka niupate na kuweka katika moyo wangu ukiwa ni majibu ya maombi yangu. Kwa njia hii, mazungumzo ya njia mbili kati yangu na Mungu yatakuwa yameanza. Najikumbusha pia kwamba ninapotafakari kuhusu kila msitari wa maandiko Matakatifu, lazima niwe macho ili nisije nikaruka sehemu yoyote ya Maandiko Matakatifu; na hasa sehemu ile ambayo naichukua kuwa nimeizoea. Leo hii, Mungu anaweza kuwa anataka kufanya sehemu hiyo ya Maandiko Matakatifu iwe hai kabisa



## KUZA IMANI YAKO

katika Moyo wangu. **Je, kuna sehemu yejote katika ukurasa huo ambayo inahusu Mungu Baba?**

**Msitari wa 3:** *Na ahimidiwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba rehema.*

Leo hii naona kwamba yale yamegusiwa kuhusu Mungu kuwa Baba umetanguliwa na yale kuhusu Mungu Baba ayaliyoko katika msitari wa pili. Kupitia kuangalia katika maelezo yaliyo kando ya maandishi matakatifu, naona kwamba msitari huu wa pili unawenza kuchukuliwa kuwa na maana *Mungu ambaye ni Baba wa Mwokozi wetu Yesu Kristo*. Hebu fikiria kuhusu jambo hili: kwamba Mungu ambaye ni Baba wa Mwokozi wetu Yesu Kristo, yeche pia ndiye Baba, wa msamaha na mwingi wa faraja. Kwa ajili ya kunifariji, Baba yangu aliye juu mbinguni ameleekeza utukufu na amani yake kwangu.

### ***Ombi***

*Baba, nainama mbele yako nikiwa na ahsante na shukrani. Nakushukuru kwa ajili ya rehema zako ambazo umeelekeza kwa moyo wangu. Umeniwekea katika moyo wangu yale ambayo daima milele ni yako - amani yako! Kwa ajili ya rehema zako, amani, utulivu na hali ya mapatano ambayo daima huwa kwako imo ndani yangu hivi leo. Halleluya!*  
*Kupitia Roho Mtakatifu, ihudumie roho yangu iliyochafuka. Ninapoinama mbele yako wewe uliye mtakatifu, yajaze maisha yangu na utulivu na amani ambayo inatokana na wewe mwenyewe kuwa ndani yangu, naomba.*



## *Karibu Mezani*

**Msitari wa 4:** *Atufarijije katika dhiki zetu zote ili nasi tupate kuwasariji wale walio katika dhiki za namna zote, kwa faraja hizo, tunazofarijija na Mungu.*

Ninapotafakari kuhusu ushuhuda huu wa mtume Paulo, naona kwamba yako maneno fulani ambayo ametumia kumaanisha “kufariji” kule ambapo alikuwa amepokea kutoka kwa Baba wetu aliye juu mbinguni. Maneno haya ni kama “huzuni,” “taabu,” “mateso,” “hukumu ya kifo.” Ni kama Roho Mtakatifu anataka kunijulisha kwamba haya yote ni mambo ambayo kwa kawaida si ya kufariji kamwe.

Ninapoendelea kusoma, naona kwamba mtume Paulo alishuhudia kwamba shida zote duniani hukubaliwa na Mungu. Na sababu yake kukubali shida ni kwamba ili tusije tukaamini katika nguvu zetu sisi wenyewe, ila tuweke imani yetu kwake Mungu ambaye ana uwezo wa hata kuwatoa wanadamu kutoka mauti. Pia naona kutoka msitari wa nne kwamba sababu iliyomfanya Mungu amhudumie na kumfariji mtume Paulo sio kwa sababu alitaka awe mtu ambaye amefarijika kila wakati, ila ili yeye naye pia awe mtu anayeweza kuwasariji wenzake. Lazima pia nami niombe kuhusu jambo hili!

### *Ombi*

*Mungu wangu, unajua wazi ni wakati gani katika maisha yangu nimetaka kuwasariji wale ambao wana shida na wako karibu nami. Nimetaka mara nyingi sana kumfariji Dorothy pale ana pozidi kuumia na maumivu makali katika mwili wake.*

## KUZA IMANI YAKO

*Kila mara, mimi huonekana kana kwamba nachukua mengi sana kutoka kwake, nami ninamhudumia kwa uchache sana na upendo na utukufu wako nikiwa na nia ya kumtia moyo na kumfariji katika maumivu yake. Nisamehe makosa haya. Ta fadhalii nijaze upya na roho ya kutaka kuwa mhudumu na sio kuwa wa kuhudumia.*

*Na ninapowaza kuhusu mamilioni ya watu ambao wanataabika na kuishi maisha ya njaa, magonjwa, vifona upweke, naomba kwamba utukufu na amani yako itakuwa katika roho yangu kiasi kwamba nitatumia kuwaondolea wenzangu mizigo yao, na kuwafariji wale ambao wanaishi katika taabu nydingi.*

*Na hata ninapoomba, naelewa vyema jinsi vile faraja zako hushughulikia kila shida, hata iwe shida kubwa kiasi gani ambayo hukubaliwa na na moyo wako ili nisijiamini mwenyewe ila niamini wewe tu.*

Wakati huu, neno la Bwana linakuwa na nguvu kwangu. Najua kwamba hata mtume Paulo alihudumiwa kupitia njia ya kukumbana na taabu nydingi ambazo zilifanya ajue kwamba hawezikutegemea nguvu zake tu. Kwa hivyo, mbona ninung'unike ikiwa kwa ajili ya upendo wake Mungu amechagua kujibu maombi yangu kupitia kuniweka katika hali ya shida ili niondolee mbali maringo na kiburi nilicho nacho.



## Karibu Mezani

### **Ombi**

*Mungu wangu, nataka kukurudishia ahsante kwa ajili ya huduma yako ya upendo maishani mwangu. Ingawa ni vigumu kuandika chini ombi hili ili wasomaji wangu waweze kulisoma, nimetiwa moyo na mtume Paulo ambaye hakuwaficha wale aliowapenda shida ambazo alikumbana nazo. Ushuhuda wake haukuhusu tu yale yaliyokuwa mazuri maishani. Kwa hivyo kutoka ndani ya roho yangu, nitakushukuru pia kwa ajili ya hata nyakati zile najisikia kuwa katika hali ya upweke ninapokuwa niko katika huduma. Katika kila maumivu ya roho ninayokumbana nayo, kila mara pale naeleweka vibaya, kila ninapofanya kosa baya, na kutenda dhambi maishani, katika kila hali ambayo inanizidi, pale ninapofanya kosa kwa ajili ya kujitegemea mwenyewe, na sio kukutegemea - naomba unisamehe. Sasa Mungu, katika utukufu wako, natilia mkazo sawa na Mtume Paulo kwamba, sitaweka imani yangu katika nafsiyangu, ila kwako. Mungu, ni siku chache zimepitaa tangu nisome maneno yake Mtume Paulo uwemo wetu kwa kila njia ni katika Bwana.*

*Asubuhi ya leo, nasisitiza kwa imani kwamba ni wewe peke ambaye ananitosha katika kila hali. Mungu mpendwa, sawa na Maandiko Matakatifu yaliyoko mbele yangu, nakusifu kwamba umeniokoa na wewe huokoa, na kwamba utaniokoa kutoka nafsi yangu mwenyewe. Ahsante sana Yesu kwa ajili ya wokovu huu wa ajabu!*



## KUZA IMANI YAKO

*Sasa Mungu, Roho Mtakatifu anapozidi kutia nguvu katika moyo wangu na faraja kutoka kwako, nakusihii hikiwa na matumaini makubwa kwamba nitumie kwa njia iliyo wazi na ya upendo kuleta faraja na kuwa wa msaada kwao wote ambao wanahitaji upendo na ambao nitakutana nao leo hii.*

**Msitari wa 11:** *Ninyi nanyi mkisaidiana nasi kwa ajili yetu katika kuomba, ili, kwa sababu ya ile karama tupewayo sisi kwa msaada wa watu wengi, watu wengi watoe shukrani kwa ajili yetu.*

Sijui uso wake mtume Paulo ungekuwa ni wa namna gani ikiwa nyuso nyingi hazingeelekezwa kwa Mungu kwa niaba yake. Sawa na haya, sijui ningekuwa wapi katika huduma yangu pasipo maombi ya marafiki wengi ambao huwa nami katika kuomba.

### *Ombi*

*Baba, siwezi kuelewa upendo wako mkuu unaouelekeza kwangu, na kuuweka katika Roho yangu na roho za watu wengi ambao ni watoto wako ambao nao humuombea mwenzangu Dorothy, na pia kuniombea. Je, nitawezaje kueleza upendo huu?*

Sasa nawaombea baadhi ya marafiki hawa katika maombi maalum ya kuwaweka marafiki na wale ninaowajua mbele ya Mungu. Ninapofanya hivyo, najaribu kushirikisha yale ambayo nimesoma katika



## Karibu Mezani

Maandiko Matakatifu kuhusu maombi ya aina hii, na yale Roho Mtakatifu amekuwa akinidokezea kuhusu maisha yangu. Ninapoomba, namsihi kwamba awape hawa ninaowaombea faraja maalum katika maisha yao wanapojitoa kabisa kumtegemea yeye Mungu.\*

**Msitari wa 15, 17-18:** *Nami nikiwa na tumaini hilo nalitaka kufika kwenu hapo kwanza, ili mpate karama ya pili; na kupita kwenu na kuendelea mpaka Makedonia, na tena kutoka Makedonia kurudi kwenu kwenu na kusafirishwa nanyi kwenda Uyahudi. Basi nilipokusudia hayo, je? Nalitumia kigeugeu? Au hayo niyakusidiayo, nayakusudia kwa jinsi ya mwili kwamba iwe hivi kwangu, kusema Ndiyo ndiyo na siyo siyo? Lakini kama Mungu alivyo mwaminifu, Neno letu kwenu si Ndiyo na siyo.*

Natafakari kuhusu mawazo ya Mtume Paulo. Yeye alishuhudia kwamba jukumu lake kubwa lilikuwa kwenda katika mji wa Korintho, na katika safari yake ya pili, kazi yake kuu iliyompeleka ilikuwa ni kufariji na kutia moyo na pia kuwa wa msaada kwao watauwa ambao aliwapenda. Lengo lake kwenda huko halikuwa ili aweze kupokea chochote kutoka kwao; yeye alienda huko kuwapa kile alichokuwa nacho. Yeye pia alishudhudia kwamba hakufunga safari hii bila mpango maalum. Hakuna mahali ambapo ametaja mambo yanayohusu pesa alizotumia. Ni wazi

---

\*Soma ukurasa 176 na 177 upate maelezo zaidi ya kukusaidia katika maombi.



## KUZA IMANI YAKO

kwamba wakati wa kwenda, hakuna lolote lililokuwa ni la kumfaa nafsi yake wakati wa kufunga safari hii kwenda Korintho.

### ***Ombi***

*Kupitia Roho wako, na neno lako, Mungu mpendwa, nionyeshe wazi nia iliyo mbaya ambayo yaweza kufungia Roho wako Mtakatifu asifanye kazi yake wakati wa kuamua ni wapi nitaelekeza huduma msimu huu wa autumn. Naona ni kama kwamba ingawa wa Kristo Korintho waliiiona ni kama kwamba yeye alikuwa na nia fulani alipoamua kubadili mipango yake iliyohusu huduma yake hapa Korintho, ushawishi mkubwa uliomfanya abadili mipango yake hii uliongozwa na roho mtakatifu. Na ahsante sana Mungu kwamba ingawa Paulo alibadili nia, akaitikia kwanza, na baadaye akaamua hafungi safari hiyo, hata wakati wa kuwahudumia hawa ambao aliwatemebelea, ujumbe wake haukuwa wa kubadilika. Katika Kristo, yote ni sawa na hayabadiliki. Pia yote katika Kristo ni ya milele. Wewe hubadili mambo katika Roho wako. Kila neno ambalo mtume Paulo alihubiri lilichunguzwa narwe na huwa limechnugzwa milele. Ahsante sana Yesu kwa ajili a kuwa mwamba mkuu katika maisha yangu - maisha ya hapa duniania ambapo kuna vishawishi ambavyo huelekeza mambo kubadilika kwa haraka sana. Mungu, nahitaji kujua mipango yako. Niokoe ili nisje nikafanya mipango ambayo inafaa anafis yangu, ama ni ya kuniletea faida.*



## *Karibu Mezani*

*Niachenitembee katika ushirika wa karibu sana nawe kila siku, naomba.*

*Je, katika somo hili kuna ahadi ambayo nahitaji kuchukua?*

**Msitari wa 20:** *Maana ahadi zote za Mungu zilizopo katika yeye ni ndiyo; tena kwa hiyo katika yeye ni Amin; Mungu apate kutukuzwa kwa sisi.*

Ninapoona wazi kwamba ahadi za Bwana zikitimizwa kupitia sisi, naijuliza, Je, jkatika somo hili, **kuna ahadi ambayo ynaohusu, na nahitaji kuchukua?**

### *Ombi*

*Je, ni kupitia sisi, Mungu? Ahadi za Mungu kupitia sisi! Ahadi za Mungu katika Kristo? Ahadi zote za Mungu katika Kristo, Mungu? Ndio, ahsante sana Mungu. Asubuhi ya leo, nikiwa mbele ya utukufu wako, nataka kusema “ndio”, na “ahsante.” Siwezi kuona na kutaja yote ambayo umenipatia kupitia Kristo. Kwa kweli, ni vigumu mimi kuwaza jinsi vile maisha yangu yangkuwa ya upweke kama singekujua na kukutambua. Siku ya leo, natilia mkazo kwamba ni wewe pekee nahitaji nitakumbana na mahitaji mblai mbali, majaribu na kazi ya kutoa maamuzi.*

Sasa nachukua muda fulani kuomba na kusifu Mungu ili amani yake izidi kuingia katika roho yangu.



## KUZA IMANI YAKO

Sijui ni majibu ya aina gani ambayo nimepokea am nitapokea katika maombi yangu; lakini hayo yote hayajalishi; kwa vile nina amani ya Bwana katika moyo wangu.

Nimetumia muda ulio wa dhamani kubwa sana kwa ajili ya kuwa na wewe Mungu wangu. Pokea sifa. Na sasa ninapoingia katika siku hii, Mungu amenipa chakula chenye thamani kubwa kutoka neno lake ambalo mawazo yangu na hata moyo wangu utawaza juu yake ninapokumbana na mambo tofauti yaliyoko mbele yangu siku ya leo.

Kwa hivyo, na acha tukumbuke jambo kuu ambalo lazima tujishugulische nalo kila asubuhi; nalo ni “kuweka roho zetu katika hali ya kuwa na furaha mbele ya Mungu.”

Ni ajabu kiasi gani kujua kwamba kila siku, Kristo anaelekeza mualiko wake kwako. Yeye anakuita kwa jina, anasema ***njoo tushiriki pamoja!***

Ukweli wako haujabadilika;  
Unawaokoa wale ambao umewaita;  
kwa wale ambao wa nakutafuta, wewe ni  
mwema;  
Na wale ambao wanakupata, wewe ni mwema  
katika kila njia.

Tunakuonja wewe mkate wa uhai,  
Na kwa muda mrefu tutazidi kukutegemea



*Karibu Mezani*

kama kitoweo;  
Twapata kinywaji kutoka kwako  
Na kiu chetu unatuondolea na kutujaza.

Bernard of Clairvaux



## APPENDIX A

*Ingawa kutenga wakati wa kusoma Buiblia ni jambo la muhimu, si lazima kufanya hivyo kila siku: kile ambacho ni lazima kifanywe ni kutenga wakati ili uwe naye Mungu kila siku. Hii itakusaidia kukuwa kiroho.*

### ***Somo la Biblia***

Hapa kuna maswali zaidi ambayo unaweza kujiuliza kuhusu maandshi matakatifu ili uweze kuwa na wakati wa kukufaidi sana unapokuwa unasoma Biblia.

Je, haya yanahu su nani?

Je, haya yanaelekezwa kwake nani?

Ni manno gani maalum ambayo yanatumiwa na mwandishi wa maneno haya matakatifu?

Je, sehemu hii ya Maandiko Matakatifu iliandikwa wakati gani?

Je, Maandiko haya Matakatifu yaliandikiwa wapi?

Je, wakati wa kuandika haya Maandiko Maakatifu, kusudi la wenye kuandika lilikuwa lipi?

Je, hali ilikuwa ya na maana gani wakati wa kuandika Maandiko haya Matakatifu?

Je, haya ambayo yanemandikwa hapa yanahu su kwa njia gani yae yaliyoko mbele na nyuma ya Maandiko haya?

*Kitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halai neno la kueli (2 Tim. 2:15)*



## APPENDIX B

### ***Wakati wa Kuwa Pamoja na Mungu***

Hapa kuna maswali ambayo unafaa kuijiliza pale unapokuwa unatafakari kuhusu kila msitari wa Maandiko Matakatifu unaousoma kila siku:

Katika msitari huu, kuna:

Dhambi ya kuepuka nayo?

Onyo la kutiliwa maanani?

Amri inayo hitaji kutii?

Mfano mzuri wa kufuata?

Mfano mbaya wa kuepuka nao?

Wazo jipya kuhusu Mungu Baba?

Wazo jipya kuhusu Mungu Mwana?

Wazo jipya kuhusu Mungu Roho Mtakatifu?

Wazo jipya linalohusu utu wake shetani?

Ufafanuzi kuhusu uovu wake shetani?

ufafanuzi kuhusu mbinu za kisiri za shetani?

*Lakini iweni watendaji wa neno, wala si wasikiaji tu, hali mkijidanganya nafsi zenu... Lakini aliyeitazama sheria kamili ifu iliyo ya uhuru, na kukaa humo, asiwe msikiaji msahaulifu, bali mtendaji wa kazi, huyo atakuwa heri katika kutenda kwake.*  
*(Yak. 1:22, 25)*



## APPENDIX C

### **Mwongozo wa Maombi ya Kila Siku**

Ili kutusaidia mimi pamoja na mke wangu Dorothy katika maombi yetu ya kuwakumbuka wenzetu, tumeamua kufuata utaratibu kutoka kwake Mwinjilisti Thomas B. Rees. Nilikuja kumjua mwinjilisti huyu miaka hamsimni hivi iliyopita. Kila herufi ya wale au kikundi kinachohitaji maombi kinashugulikiwa siku ya wiki ambayo jina lake laanza na herufi hiyo. Kwa mfano “M” ambayo ni “Monday”ni siku ya maombi ya wamishonari yaani, “Missionaries” na kadhalika.

Baada ya kulisha roho zetu na neno la Bwana, na baadaye kuomba kuhusu neno lenyewe, maombi ya kusihii huwa na uhai. Badala ya kuomba maombi ambayo ni ya kawaida na kutumia matamshi ambayo ni mazoea, maombi ya kusihii Mungu kwa ajili ya wenzetu huwa ni maombi ya kweli kabisa, marefu, yenye shukrani, na kuwajali sana wenzetu. Ingawa hatuna orodha halisi ya maombi haya, sisi tunaamini kwamba Roho Mtakatifu ana uwezo wa kuongeza muda wetu wa maombi ili tuweze kushughulikia mahitaji yote ya maombi.

*Msijisumbue kwa neno lolote; bali katika kila neno  
kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja  
zenu na zifulikane na Mungu (Flp. 4:6).*

Kumbuka: **Mwongozo huu wa Maombi ya Kila siku** hauweki kando maombi ya n ayohusu mahitaji yetu sisi; au hata mahitaji ambayo yanaweza kujitokeza bila kutarajiwa kila siku.



## Mwongozo wa Maombi ya Kila Siku

**J**umatatu  
*Wamishonari*

Wa mishonari ambao kazi yao Mungu ametufa nya nasi tuwe na hamu ya kushiriki nao.

**J**umanne  
*Kushukuru*

Siku iliyotengwa kuomba na kumshukuru na kumpa utukufu Mungu kwa ajili ya yale ambayo yanamhusu yeye, na kwa ajili ya ke ambaye ni Mungu. Maombi kwa ajili ya yale amefanya, na kwa ajili ya yale atakayofanya; na pia kwa ajili ya vile vyote ambavyo ametupatia.

**J**umatano  
*Wa fanyi kazi*

Makasisi, wainjilisti, Waalimu wa Maandiko Matakatifu, na wafanyi kazi wote katika huduma ya Bwana.

**A**lhamsi  
*Kazi*

Kazi za nyumbani, kazi katika huduma, kazi zinazohusu matumizi ya pesa.

**I**jumaa  
*Familia*

Familia yetu wenyewe ndogo, pamoja na familia kubwa ya wale ambao ni wa ukoo wetu pamoja na wale ambao ni marafiki wa karibu sana wa Dorothy nami na pia watoto wetu na wajukuu wetu katika Kristo.


**J**umamosi  
*Watendao dhambi*

Kazi ya huduma ya kitabu *Kiu Cha Kumtafuta Mungu* kote duniani. Watu wale ambao tumekutana nao katika barabara mijini na tukashiriki nao katika neno la Bwana, wale a mabo wako katika familai yetu, na pia wako inje ya familia ya Kristo.

**J**umapili  
*Watauwa*

Wale ambao tunawajua ambao ni juzi tu wameupokea wokovu; wale ambao sisi hushiriki nao katika maombi, na pia kupitia maisha yao, sisi tumeweza kubariiwa sana. Wale ambao ni wanachama wa kanisa au waumini ambao wanapata mateso kwa ajili ya imani yao. Na ambao tuna hamu ya kujua hali yao. Ufufuo katika kanisa leo.





*Endapo ungehitaji  
maelezo zaidi  
kuhusu mpango  
wa Mungu  
wa wokovu,  
maelezo  
haya yako  
katika kitbau*

# *Kiu Cha Kumtafuta Mungu*

**Kiu Cha Kumtafuta Mungu chaweza  
kikawa chombo cha kukusiadia katika  
kazi ya uinjilisti.**

"*Kiu cha Kumtafuta Mungu ...* ni kitabu cha kukusaidia kujijenga KiKristo

*Rev. Stephen Boakye-Yiadom, Trans World Radio, Africa*

Zaidi ya nakala millioni tatu tayari ziemchapishwa;  
katika jumla ya lugha 50.

*Mkurugenzi*  
Trans World Radio - Kenya  
P.O. Box 21514 (00505)  
Nairobi, Kenya  
e-mail: info@twr.co.ke

[www.ccim-media.com](http://www.ccim-media.com)